# Ripoti ya Uchunguzi wa Ridhaa

## CAO Ilianzisha Uchunguzi Kuhusiana na Uwekezaji wa IFC kwa shule za Bridge International Academies (Bridge-04)

**SIRI KUBWA**

Bridge International Academies/Miradi ya IFC #32171, #38733, #39170, na #39224
Oktoba 3, 2023

# Yaliyomo

**Muhtasari Mkuu** ..... **4**
Maelezo ya Jumla ..... 4
Uwekezaji wa IFC ..... 4
CAO Ilianzisha Uchunguzi kuhusu Kuridhia ..... 5
Wajibu wa IFC Kimazingira na Kijamii (E&S) Unaohusiana na Unyanyasaji wa Watoto Kingono ..... 6
Matokeo ya Uchunguzi wa CAO ..... 8
Madhara ..... 11
Sababu Kuu za Kutoridhia ..... 12
Mapendekezo ya CAO kwa IFC ..... 13
Mapendekezo Kutegemea Mradi Mahususi ..... 13
Mapendekezo ya Ngazi ya Taasisi ..... 14
Hatua zinazofuata ..... 15
**1. USULI** ..... **16**
1.1. Muktadha Nchini na katika Sekta ya Elimu ..... 16
1.2. Uwekezaji wa IFC ..... 17
1.2.1. Kujiondoa kwa IFC na uamuzi wa kusitisha uwekezaji katika shule za kibinafsi za K–12 zinazolipisha karo ..... 18
1.3. Chanzo cha Uchunguzi wa CAO wa Bridge-04 ..... 19
1.3.1. Malalamishi, tathmini na uchunguzi wa Bridge-01 ..... 19
1.4. Ratiba ya Matukio Muhimu ..... 21
1.5. Ufafanuzi wa dhana ..... 23
1.6. Mbinu Iliyotumiwa na CAO Kufanya uchunguzi wa ridhaa wa Bridge-04 ..... 24
1.6.1. Upatikanaji na Ufichuzi wa Taarifa ..... 26
**2. Viwango, Sera, na Vigezo Vinavyotumiwa kuhusiana na Unyanyasaji wa Watoto Kingono** **28**
2.1. Viwango vya IFC vinavyotumika ..... 28
2.1.1. Kiwango cha kwanza cha Utendakazi cha IFC: Tathmini na Ushughulikiaji wa Hatari na Athari kwa Mazingira na Jamii ..... 29
2.1.2. Kiwango cha Nne cha Utendakazi cha IFC: Afya, Usalama na Ulinzi wa Jamii ..... 31
2.2. Sheria za Kenya zinazotumika katika nyanja ya elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini ..... 31
2.3. Mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa yanayotumika kwa Masuala Yanayohusiana na CSA katika elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini ..... 32
2.3.1. GIIP iliyokuwa inatumika wakati wa utafiti wa IFC wa kabla ya mradi ..... 33

2.3.2. GIIP iliyokuwa inatumika wakati wa usimamizi wa IFC wa mradi ............................ 33

**3. Uchambuzi wa Matokeo ya CAO na Kutoridhia: E&S ya IFC Utafiti wa Kabla ya Mradi 36**

3.1. Maelezo ya jumla ya E&S ya IFC ya Utafiti Wa Kabla Ya Mradi .................................... 36

3.1.1. Utafiti wa kabla ya mradi na ulinzi wa watoto ......................................................... 37

3.2. Matokeo ya Uchunguzi wa CAO...................................................................................... 37

3.2.1. Maelezo ya Jumla..................................................................................................... 37

3.2.2. Uwezo wa mradi kuwa na hatari za CSA ................................................................ 38

3.2.3. Kutoridhia kwa IFC ................................................................................................... 39

3.2.4. Athari za mapungufu ya IFC kwa ESDD .................................................................. 40

**4. Uchambuzi wa CAO na Matokeo ya Kutoridhia wakati wa Usimamizi........................ 42**

4.1. Maelezo ya jumla kuhusu usimamizi wa IFC ................................................................ 42

4.1.1. Usimamizi wa IFC kabla ya CAO kupokea taarifa kuhusu CSA inayohusiana na mradi Februari mwaka wa 2020 ................................................................................................. 42

4.1.2. Usimamizi wa IFC kuanzia Februari mwaka wa 2020 hadi ilipojiondoa kwenye mradi Machi mwaka wa 2022 43

4.2. 3. Uchambuzi wa CAO na Matokeo yake ...................................................................... 48

4.2.1. Uchanganuzi wa usimamizi wa IFC wa mradi: Tangu mwaka wa 2014 hadi Februari mwaka wa 2020 49

4.2.2. Uchanganuzi wa usimamizi wa IFC wa mradi: Tangu mwaka wa 2020 hadi Februari mwaka wa 2022 IFC ilipojiondoa.............................................................................................. 52

**5. Sababu Kuu za Kutoridhia ............................................................................................ 55**

5.1. Kushindwa kwa IFC kutathmini athari kwa mazingira na jamii ...................................... 55

5.2. Ukosefu wa Wataalamu wa Usimamizi wa Hatari za Kijamii wakati wa Usimamizi ......... 55

5.3. Ugumu wa Kupata Taarifa............................................................................................. 55

5.4. Ukosefu wa Maarifa kuhusu Mienendo Mipana ya Kitaasisi .......................................... 56

5.5. Ukosefu wa Uwazi kuhusu Kujiondoa kwa mradi.......................................................... 56

**6. Madhara......................................................................................................................... 57**

6.1. Mambo Yanayohusiana na Madhara............................................................................. 57

6.2. Matukio ya Kudhuriwa .................................................................................................. 58

**7. Mapendekezo ya CAO kwa IFC ..................................................................................... 60**

7.1. Mapendekezo Kutegemea Mradi Mahususi.................................................................... 60

7.2 Mapendekezo ya Ngazi ya Taasisi .................................................................................. 61

**Hatua zinazofuata ............................................................................................................ 62**

# Muhtasari Mkuu

## Maelezo ya Jumla

Ripoti hii inawasilisha matokeo na mapendekezo kutoka kwa uchunguzi wa ridhaa wa Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman (CAO) katika uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) katika shule za Bridge International Academies ("Bridge," "mteja," au "kampuni"), ambapo wakati wa kipindi cha uwekezaji wa IFC miaka ya (2014 hadi 2022) iliendesha mkusanyiko wa shule nyingi binafsi za gharama nafuu barani Afrika. Kufuatia tathmini ya ridhaa iliyoanzishwa mwezi wa Januari mwaka wa 2021 na Makamu wa Rais wa CAO, uchunguzi unazingatia matumizi ya IFC ya mahitaji yake ya kimazingira na kijamii (E&S) kuhusiana na hatari za unyanyasaji wa watoto kingono[1] (CSA) na athari zinazohusiana na uwekezaji kwa shule za Bridge. Ingawa IFC iliacha kuwekeza moja kwa moja kwa shule za Bridge mwezi wa Machi mwaka wa 2022, mahusiano yasio ya moja kwa moja kati IFC na Bridge kupitia Learn Capital, taasisi ya kifedha iliowaunganisha, yalikuwa yanaendelea wakati wa kuandika ripoti hii.[2]

CAO imegundua kwamba IFC ilishindwa kukidhi mahitaji yake ya Kimazingira na Kijamii chini ya Sera ya Uendelevu na inayohusiana na Viwango vya Utendakazi 1 na 4 wakati wa utafiti wa kutathmini athari kwa mazingira na jamii (ESDD) kabla ya uwekezaji na wakati wa usimamizi wake wa mradi huu. Usimamizi wa IFC wa hatari na athari za CSA uliboreshwa baada ya CAO kutoa taarifa kuhusu matukio yanayohusiana na CSA yanayohusishwa na Bridge na baadaye kutoa taarifa hizo kwa IFC mwezi wa Februari mwaka wa 2020. Hata hivyo, kutokana na hatari kubwa na zilizoenea kwa jamii zinayotambulika na dhahiri katika mradi huu, CAO inatambua kuwa juhudi za usimamizi za IFC zilishindwa kutekeleza wajibu wake. Kabla ya kujiondoa kwenye uwekezaji, IFC ilishindwa kufanya kazi na mteja wake kushughulikia hatari na athari za CSA kama inavyotakiwa na Sera ya Uendelevu.

Kwa kuzingatia matokeo haya, CAO inatoa mapendekezo kwa IFC kuchukua hatua za kukabiliana na hali hii ili kushughulikia madhara kwa waathirika wa CSA waliotambuliwa katika ripoti hii.[3] CAO pia inatoa mapendekezo ya ngazi ya taasisi ili kusaidia IFC kuzuia na kudhibiti ipasavyo hatari za CSA katika shughuli zake katika siku zijazo.

## Uwekezaji wa IFC

Madhumuni ya uwekezaji wa IFC yalikuwa kusaidia upanuzi wa msururu wa shule za Bridge kuanzia shule za chekechea hadi gredi ya 12[4] zinazohudumia jamii za kipato cha chini nchini Kenya na kufunguliwa kwake katika

---

[1] **Unyanyasaji wa watoto kingono** unafafanuliwa kama kushiriki kwa mtoto katika shughuli za kingono-ikiwa ni pamoja na "unyanyasaji bila kuguswa" kama vile unyanyasaji wa kingono kwa mtoto - ambao mtoto hauelewi kikamilifu, hawezi kutoa idhini kwa kuelewa, au mtoto hajakua vya kutosha na kwa hivyo hawezi kutoa idhini, au kitu kinachokiuka sheria au miiko katika jamii. Unyanyasaji wa watoto kingono unathibitishwa na shughuli hii kati ya mtoto na mtu mzima au mtoto mwingine ambaye kwa kuzingatia umri au ukuaji yupo katika uhusiano wa uwajibikaji, uaminifu au uwezo, shughuli inayokusudiwa kutimiza au kukidhi mahitaji ya mtu mwingine.

[2] Lengo la ripoti hii ya uchunguzi ni kuhusu uwekezaji wa moja kwa moja wa IFC katika Bridge kutoka mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2022. Hata hivyo, ripoti hii pia inazingatia kwa ufupi ushirikiano wa IFC na Bridge kupitia Learn Capital, uwekezaji mwingine wa IFC, haswa kwa sababu inahusiana na kipindi kilichofuatia uuzaji wa IFC wa hisa zake za moja kwa moja katika mwaka wa 2022.

[3] Kama inavyofafanuliwa katika Sera ya CAO, Madhumuni ya kitengo cha ridhaa cha CAO ni kutathmini kuridhia kwa IFC/MIGA kwa Sera za Kimazingira na Kijamii (E&S), kutathmini Madhara yanayohusiana, na kupendekeza hatua za kukabiliana na hali hii inapowezekana." (aya ya 76). Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf.

[4] Kikundi Kinachojitegemea cha Kutathmini Benki ya Dunia (IEG), Juni mwaka wa 2022, Tathmini ya Uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa katika Shule Binafsi za K–12. Inapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/sites/default/files/Data/Evaluation/files/IFCSupport_K12PrivateEducation_GS_and_MC.pdf.

nchi tatu mpya ("mradi").[5] Wakati wa uwekezaji wa IFC, Bridge iliendesha shule 211 za msingi na sekondari nchini Kenya, zilizohudumia takribani wanafunzi 57,000.[6] IFC ilifanya utafiti wa kutathmini athari za mradi kwa mazingira na jamii (ESDD) kabla ya uwekezaji katika mwaka wa 2013, na mradi uliidhinishwa na Bodi ya IFC mwezi wa Desemba mwaka 2013.[7] IFC iliorodhesha uwekezaji kwa Kundi B, kuonesha kuwa hatari zake mbaya za Kimazingira na Kijamii (E&S) zilikuwa chache, kwa kiasi kikubwa zinaweza kushughulikiwa, na zinaweza kupunguzwa kwa urahisi.[8] Katika mwezi wa Januari mwaka wa 2014, IFC ilifanya uwekezaji unaopendelewa wa hisa za Dola za Marekani milioni 10 katika Shule za NewGlobe (NGS), kampuni mama ya Bridge iliyo na makao yake Marekani (mradi #32171). Uwekezaji wa ziada ulifuatia Julai na Novemba mwaka wa 2016 (miradi #38733, #39170, na #39224). Jumla ya uwekezaji wa hisa za IFC kwa Bridge/NGS ulikuwa Dola za Marekani milioni 13.5.[9]

Mwezi Machi mwaka wa 2020, kutokana na malalamishi yaliyoibuka kuhusu shule binafsi za gharama nafuu, Rais wa Kundi la Benki ya Dunia (WBG) alisimamisha uwekezaji wa moja kwa moja wa IFC katika shule binafsi za K–12.[10] IFC iliacha uwekezaji wake wa moja kwa moja katika NGS mwezi wa Machi mwaka wa 2022[11] na ikafuatia na tangazo kwamba itaendelea kusitisha uwekezaji wa moja kwa moja katika shule binafsi za K–12.[12] Wakati wa ripoti hii, IFC ilikuwa na uhusiano usio wa moja kwa moja na shule za Bridge kupitia taasisi ya kifedha iliowaunganisha, Learn Capital Venture Partners Fund III (mradi #32429).[13]

## CAO Ilianzisha Uchunguzi kuhusu Kuridhia

Uchunguzi huu, unaojulikana kama "Bridge-04," ulianzishwa na Makamu wa Rais (VP) wa CAO kufuatia CAO kupokea taarifa zinazoonesha matukio ya madai ya unyanyasaji wa watoto kingono (CSA) nchini Kenya wakati wa uchunguzi tofauti katika Shule za Bridge International Academies (Bridge-01).

Kama sehemu ya uchunguzi wa Bridge-01, mwezi wa Februari mwaka wa 2020, wafanyakazi wa CAO walizungumza na wanajamii mjini Nairobi, ambao waliripoti kuhusu waathirika watoto kumi na tano wa[14] CSA katika shule za Bridge uliofanywa na walimu wawili wa Bridge. Taarifa kuhusu tuhuma hizi zilitolewa mara moja kwa IFC na CAO.

Taarifa hizi zilisababisha Makamu wa Rais wa CAO mwezi wa Septemba mwaka wa 2020 kuitisha tathmini ya ridhaa ya IFC ya utafiti wa kabla ya uwekezaji na ufuatiliaji wa hatari za Kimazingira na Kijamii (E&S) zinazohusiana na CSA na athari zinazoweza kutokea kutokana na shughuli za Bridge (kesi ya Bridge-04).[15]

[5] IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Taarifa za Uwekezaji (SII). unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies. Msaada wa IFC kwa Bridge ulitekelezwa kupitia kampuni mama ya Bridge ya jimbo la Delaware ya NewGlobe Schools, Inc. ("NGS"), ambayo ilianzisha Bridge mwaka wa 2011 kama tawi inayomiliki kikamilifu nchini Kenya.
[6] IFC, Oktoba 2013, Maelezo ya Mradi wa SII. Yanapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies.
[7] Ibid.
[8] IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Tathmini ya Mazingira na Jamii (ESRS). Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.
[9] IEG, Juni 2022, Tathmini ya Uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa katika Shule Binafsi za K–12. Inapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/sites/default/files/Data/Evaluation/files/IFCSupport_K12PrivateEducation_GS_and_MC.pdf.
[10] Benki ya Dunia (WBG), Machi 20, 2020, Barua kutoka kwa Rais wa Benki ya Dunia (WBG) kwa Katibu wa Hazina ya Marekani. Makala yaliyohaririwa yanapatikana hapa: https://democrats-financialservices.house.gov/uploadedfiles/malpass_ltr_mnuchin_3202020.pdf.
[11] IFC, Oktoba 2013, Maelezo ya Mradi wa SII. Yanapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies.
[12] IFC, 2022, Ushughulikiaji wa Wasimamizi kwa Ripoti ya IEG. Unapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/evaluations/evaluation-international-finance-corporation-investments-K–12-private-schools-7.
[13] Mradi #32429. Uwekezaji wa IFC katika Learn Capital Venture Partners Fund III ("Learn Capital") ulifanyika tarehe 2 Julai, mwaka 2014, na malipo ya kwanza yalifanyika tarehe 30 Juni, mwaka wa 2015. Uwekezaji huu unaashiria ushirikiano na shule za Bridge kwa sababu Learn Capital inamiliki hisa katika Shule za NewGlobe. Taarifa zinapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32429/education-innovation-fund.
[14] Ripoti hii inatumia istilahi ya tukio (matukio) kama tukio kuhusiana na CSA, na muathirika/waathirika kurejelea watoto walliodhulumiwa kupitia CSA. Kwa kuongezea, CAO inatumia istilahi zifuatazo katika ripoti hii.
[15] CAO, Desemba 23, 2020, Tathmini ya Ridhaa ya Bridge-04: Muhtasari wa Matokeo, uk. 16. Unapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/CAOAppraisalReport-BIA-04-Dec23.pdf.

Tathmini hii "ilionyesha kwamba kuna kiwango kikubwa cha mambo ya kusikitisha kuhusiana na matokeo ya Kimazingira na Kijamii (E&S) ya uwekezaji wa IFC kwa Bridge kwa kuzingatia: (a) madai maalum ya unyanyasaji wa watoto kingono yaliyotolewa wakati wa uchunguzi wa Bridge-01; na (b) uwezo mkubwa wa hatari za Kimazingira na Kijamii (E&S) kutokea shuleni kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi na uwezekano kwao kuwa hatarini zaidi."[16]

Kufuatia hali hii, CAO ilizindua uchunguzi wa ridhaa wa Bridge-04 unaoshughulikia utepetevu wa IFC wa maswala ya usalama na ulinzi wa watoto,[17] kwa kuzingatia haswa hatari na athari za CSA katika shule za Bridge nchini Kenya.[18] Hatari na athari hizi za CSA ziko katika mawanda ya unyanyasaji wa kijinsia (GBV)[19] dhidi ya watoto.[20] [21]

## Wajibu wa IFC Kimazingira na Kijamii (E&S) Unaohusiana na Unyanyasaji wa Watoto Kingono

Mfumo wa Kimazingira na Kijamii (E & S) wa IFC ulihitaji IFC iwekeze tu kwa Bridge ikiwa ilitarajia shughuli za Bridge kukidhi mahitaji yanayohusiana na Kiwango cha Utendaji (PS) cha kimazingira na kijamii ndani ya muda unaofaa, kulingana na Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii ("Sera ya Uendelevu") (aya ya 22). Ijapokuwa ni wateja wanaowajibikia ushuhgulikiaji wa hatari na athari za Kimazingira na Kijamii (E&S) kwa kuzingatia Viwango vya Utendakazi vya IFC, IFC huwajibikia utafiti wa kutathmini athari kwa mazingira na jamii (ESDD), ufuatiliaji, na usimamizi wa uwekezaji wake ili kuhakikisha kuwa shughuli za biashara zinazofadhiliwa zinafuata mahitaji ya PS (Sera ya Uendelevu, aya za 21 hadi 28). Zaidi ya hayo, ikiwa baada ya idhini ya Bodi kuna mabadiliko makuu katika hali ya hatari ya Kimazingira na Kijamii (E&S) ya mradi, IFC inahitaji kutathmini hali hii na, kwa kuzingatia hatari na mahitaji ya Viwango vya Utendakazi, na kumtaka mteja kurekebisha Mfumo wake wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESMS) ili kushughulikia hali (Sera ya Uendelevu, aya ya 25). Wakati wote wa uwekezaji, majukumu ya usimamizi wa Kimazingira na Kijamii (E&S) wa IFC yaliitaka kufuatilia mara kwa mara kuridhia kwa Bridge kwa Viwango vya Utendaji (PS) ambavyo vilikuwa muhimu kwa hatari na athari zinazohusiana na mradi wa CSA, na kushirikiana na Bridge kurekebisha maeneo yoyote ambapo mradi haukuridhia (Sera ya Uendelevu aya ya 45).

---

[16] Ibid.

[17] **Ulinzi wa watoto** unarejelea hatua zote ambazo kampuni huchukua ili kuwaweka watoto wote wanaojumuika nayo salama, na inajumuisha hatua zinazochukuliwa ili kuhakikisha watoto hawadhuruwi kwa kujumuika moja kwa moja au kwa njia isio moja kwa moja na kampuni. Ulinzi wa watoto unajumuisha uzuiaji wa unyanyasaji wa mwili, wa kingono na kihisia, kutelekezwa na kudhulumiwa kwa watoto na wafanyakazi na watu wengine ambao kampuni inawajibikia, ikiwa ni pamoja na wakandarasi, washirika wa biashara, wageni katika eneo na watu wanaofanya kazi bila malipo.
**Utunzaji wa watoto** ni sehemu muhimu ya ulinzi na unarejelea hatua ambazo kampuni huchukua kushughulikia wasiwasi wa kipekee kwamba mtoto fulani ana uwezekano mkubwa wa kudhuriwa kutokana na yeye kujumuika na wahusika katika kampuni, washirika wa biashara, bidhaa au huduma. Utunzaji wa mtoto ni muhimu ikiwa kuna wasiwasi kwamba mtoto anapitia unyanyasaji au usalama wake uko hatarini.

[18] CAO, Oktoba 21, 2021, Masharti ya Uchunguzi wa Ridhaa ya Bridge-04. Yanapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/Bridge-04%20ToR%20for%20Compliance%20Investigation%20FINAL.pdf.

[19] **Unyanyasaji wa kijinsia** ni unyanyasaji ambao husababisha, au unaoweza kusababisha, madhara au mateso kwa mwili, kingono, au kisaikolojia, dhidi ya mtu kutokana na ubaguzi wa kijinsia, matarajio ya wajibu wa jinsia, na/au dhana potofu za kijinsia, au kutokana na hali inayotofautiana ya mamlaka inayohusiana na jinsia.

[20] Angalia, kwa mfano, UNICEF, "Unyanyasaji wa Kijinsia dhidi ya Watoto," (inaelezea unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto kama aina ya "unyanyasaji wa kijinsia" na kubaini kuwa wavulana na wasichana hukabiliwa na unyanyasaji wa kingono). Inapatikana hapa: https://www.unicef.org/protection/sexual-violence-against-children.

[21] CAO inatambua kwamba madai ya unyanyasaji wa watoto kingono yaliyotajwa katika ripoti hii yanaweza kuchukuliwa kama uhalifu chini ya sheria ya Kenya, *lakini inasisitiza kwamba ripoti hii haijampata mtuhumiwa kuwa mhalifu wala kumtaka kulipia.* Mchakato wa kuridhia wa CAO hauhusiki na ushahidi, sio wa kimahakama, na "haujaundwa wala kukusudiwa kutumiwa katika kesi mahakamani au kutoa hukumu au kwa makusudi ya kuhusisha uhalifu kisheria au kuwajibikia hali." Sera ya CAO katika aya ya 9 na 117. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf. Kwa kuongezea, CAO inabainisha kuwa kwa sababu uchunguzi wa kitengo cha ridhaa sio michakato ya kimahakama, viwango vya ushahidi vinavyohitajika ili kuwa ushahidi wa kutosha kuunga mkono matokeo ya uchunguzi wa CAO havihusiani na mahitaji ya kumuhukumu mhalifu wala mahitaji ya kotoa ushahidi mahakamani.

Mfumo wa Kimazingira na Kijamii (E&S) wa IFC haushughulikii kikamilifu hatari na athari zinazohusiana na watoto mbali na ajira kwa watoto na watoto kuwa hatarini zaidi kukumbwa na usafirishaji haramu wa binadamu (PS2, aya ya 21 na tanbihi ya 13). Hata hivyo, mahitaji ya jumla ya kutathmini, kuepuka, kupunguza, na—pale athari zinaposalia baada ya mikakati kuwekwa—kufidia/kulipia hatari na athari za Kimazingira na Kijamii (E&S) za shughuli za biashara,[22] kama vile uendeshaji wa shule, ni mambo yanayofaa na ni wazi yanahusiana na hatari zinazohusiana na mradi na athari kwa watoto, ikijumuisha unyanyasaji wa watoto kingono na unyanyasaji wa kijinsia.

Wakati wa uwekezaji wa IFC kwa Bridge, sheria ya Kenya ilizungumzia wazi CSA, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya shuleni. Kwa kuongezea, mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa na Kenya, ikijumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, inapaswa kuzingatiwa chini ya sheria nchini Kenya (Katiba ya Kenya 2010, Kifungu cha 2(6)). Kwa ujumla, imethibitishwa kuwa CSA ni tishio kubwa kwa afya, ulinzi na usalama wa watoto, ikiwa na athari mbaya zaidi kwa maendeleo ya kijamii ya watoto na jamii. [23] [24]

Viwango vya Utendakazi vya IFC viwili vinaingiliana na kushughulikia unyanyasaji wa watoto kingono, ingawa havitaji wazi CSA: PS1 (Tathmini na Ushughulikiaji wa Hatari na Athari kwa Mazingira na Jamii) na PS4 (Afya ya Jamii, Ulinzi, na Usalama). Kuhusiana na uwekezaji kwa Bridge, Viwango hivi vya Utendakazi vinahitaji IFC:

- Kumtaka mteja kutambua na kutathmini hatari na athari zote za Kimazingira na Kijamii (E&S) kuhusiana na mradi, na kushughulikia hatari na athari hizo. Chini ya PS1, mipango ya ushughulikiaji wa hatari na athari inapaswa kutoa kipaumbele kwa uepukaji wa hatari na athari. Pale ambapo uepukaji hauwezekani, wateja lazima watafute jinsi ya kuzipunguza, na, pale ambapo athari zitasalia baada ya mikakati, wateja lazima wafidie/walipie kitaalam na kifedha inapowezekana (PS1, malengo, aya ya 5, na aya ya 14).

- Kumtaka mteja azingatie **sheria na kanuni za kitaifa** zinazohusiana na mradi **husika**, ikiwa ni pamoja na zile zinazotekeleza ahadi za kimataifa (PS1, aya ya 6).
- Kutaka michakato ya mteja kutambua hatari za Kimazingira na Kijamii (E&S) kurandana na **mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (GIIP)** (PS1, aya ya 7).
- Kumtaka mteja, pale ambapo mradi umebainisha vipengele ambavyo vinaweza kupelekea athari za Kimazingira na Kijamii (E&S): (1) kutambua watu binafsi na vikundi ambavyo **vinaweza kuathiriwa moja kwa moja na kwa njia tofauti au kwa kiasi kikubwa na mradi kutokana na hali yao ngumu au kuwa hatarini zaidi**, na (2) kupendekeza na kutekeleza **mikakati mbalimbali** ili athari mbaya zisikumbe watu hawa (PS1, aya ya 12).
- Kutaka hatua za kuzuia na kudhibiti zinazohusiana na afya, ulinzi na usalama katika jamii **zirandane na GIIP**, na kupendekeza hatua za kukabiliana na hali **kulingana na hali na ukubwa wa hatari na athari (**PS4, aya ya 5).

[22] IFC, 2012, Viwango vya Utendakai kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, ibara za 5 na 14. Tazama pia IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, ibara za 6 na 20. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/sp-english-2012.pdf.

[23] Tazama, UNICEF, 2014 Wazi ila Fiche: Uchambuzi wa Takwimu za Ukatili Dhidi ya Watoto, uk. 62. Tazama pia IFC, EBRD, CDC, na Maendeleo ya Jamii Moja kwa Moja (2020), Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu, uk. 1. Inapatikana hapa: https://data.unicef.org/resources/hidden-in-plain-sight-a-statistical-analysis-of-violence-against-children/.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/gpn-addressinggbvh-july2020.pdf.

[24] Tazama, kwa mfano, Kifungu cha 19 na 34 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (1989), na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (1981). Vinapatikana hapa: https://www.ohchr.org/sites/default/files/crc.pdf.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na hapa: https://www.ohchr.org/sites/default/files/cedaw.pdf.

Kwa kuongezea, GIIP na sheria za Kenya zinazohusiana na CSA katika sekta binafsi ya elimu ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini zilikuwa tayari zinatumika na zingefikiwa kwa urahisi na IFC wakati wa utafiti kuhusu mradi na zilitumika kipindi chote cha uwekezaji.

CAO pia inabainisha kuwa, sambamba na uwekezaji huu wa IFC, vitengo vya sekta ya umma vya Benki ya Dunia vilikuwa vikijihusisha na masuala yanayohusiana na GBV. Mwezi wa Aprili mwaka wa 2015, Benki ya Dunia ilitoa muhtasari wa sekta ya elimu uliojulikana kama "Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana," ambao ulielezea jinsi, pamoja na hatari zingine kuu katika jamii, mazingira ya shule yanaweza kuakisi sifa za jamii zinazoyazunguka, ikiwa ni pamoja na kanuni za kijinsia na ukatili. Mwezi wa Oktoba mwaka wa 2016, Rais wa Benki ya Dunia alianzisha kikosi kazi huru cha wataalam wasiofanya kazi na Benki ya Dunia ili kuimarisha mifumo, zana, na michakato ya Benki ili kuzuia na kupunguza hatari za udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono (SEA).[25] Ulifuatiwa na Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi unaohusisha Kazi Kuu za Kiraia (2018), Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia katika Sekta Binafsi (2020; iliyoandaliwa kwa ushirikino na IFC), na Kushughulikia Dhuluma na Ukatili wa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono (SEA/SH) katika Operesheni za Maendeleo ya Binadamu (2022).[26]

## Matokeo ya Uchunguzi wa CAO

Katika kukagua vitendo vya IFC dhidi ya mahitaji yaliyopo hapo juu, CAO inawasilisha matokeo yafuatayo:

1. **IFC ilishindwa kutekeleza majukumu yake ya utafiti wa kabla ya mradi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii ("Sera ya Uendelevu").** Utafiti wa IFC wa kabla ya mradi haukukidhi mahitaji ya Sera ya Uendelevu, haswa ibara ya 20 hadi 28, ikizingatiwa hali na kiwango kikubwa cha shughuli za Bridge na hatari kubwa za CSA zinazohusiana na mradi unaohusisha kujumuika kwa mara kwa mara kati ya watu wazima na wanafunzi, wanafunzi wa K–12 katika jamii za kipato cha chini. Nchini Kenya, kama ilivyo katika nchi nyingi, unyanyasaji wa watoto kingono na aina zinazolingana za GBV dhidi ya watoto zimeenea na huwa haziripotiwi. Kwa pamoja, ripoti ya mwaka wa 2010 ya shirika lisilo la kiserikali (NGO) linalosimamia kwa pamoja nambari kuu ya kitaifa ya kupiga simu kuhusiana na CSA bila malipo,[27]

---

[25] WBG, Julai 31, 2017, *Kufanya kazi pamoja ili kuzuia dhuluma na unyanyasaji wa kingono: mapendekezo kwa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.* Inapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/482251502095751999/pdf/117972-WP-PUBLIC-recommendations.pdf. **Unyanyasaji na Dhuluma za Kingono** ni tendo halisi au jaribio la kutumia vibaya mamlaka, nafasi yako au kuaminiwa na mtu ambaye yuko hatarini kuathiriwa kwa madhumuni ya ngono, ikijumuisha, na wala sio tu, na lengo la kunufaika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na kumnyanyasa mtu mwingine kingono. Unyanyasaji wa kingono unafanuliwa zaidi kama "uingiliaji halisi au kutishiwa kingono, iwe kwa nguvu au kupitia hali zisizo sawa au kwa kulazimisha." Wanawake, wasichana, wavulana na wanaume wanaweza kupitia SEA. Katika muktadha wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, wanaonufaika kutokana na mradi au wanajamii ambako mradi unatekelezwa wanaweza kupitia SEA. (Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi Inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia, yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf). **Makala kwa msomaji:** Ripoti hii haitumii neno SEA **isipokuwa** tu wakati wa kutaja stakabadhi fulani za IFC ambazo zimetumia neno hilo wazi.

[26] WBG, Septemba 28, 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia; IFC, CDC, EBRD, Julai 2020, Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia katika Sekta Binafsi; na WBG, Septemba 2022, Kushughulikia Dhuluma na Ukatili wa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono (SEA/SH) katika Operesheni za Maendeleo ya Binadamu. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf; hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/gpn-addressinggbvh-july2020.pdf; na hapa: https://thedocs.worldbank.org/en/doc/0e0825d39c28f61080380c6be9c40811-0290032022/original/SEA-SH-GPN-for-HD-Operations-CESSO-Issue-Version-September-26-2022.pdf

[27] Childline Kenya, 2010, Unyanyasaji Wa Watoto Kingono nchini Kenya: Kutokea Kwake, Muktadha, Vihatarishi na Matokeo, uk. 8. Inapatikana hapa: https://childlinekenya.co.ke/assets/files/Child%20Sexual%20Abuse%20Research%20Report-CLK-2011.pdf. "Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya nchini Kenya uligundua kuwa asilimia 12 ya wanawake nchini Kenya wenye umri wa miaka kati ya 15 na 49 walisema kwamba walilazimishwa kufanya ngono mara ya kwanza. Idadi hii iliongezeka hadi asilimia 23 kwa wanawake ambao walisema walifanya ngono mara ya kwanza kabla ya umri wa miaka 15. Utafiti wa hivi karibuni wa Girl Childline Network katika mwaka wa 2011 uliohusisha watoto wa shule kutoka eneo la Tana River nchini Kenya uligundua kuwa asilimia 25 ya wasichana walipitia hali ya kudhulumiwa kingono kupitia kuguswa na asilimia 10 walikuwa wamelazimishwa kufanya ngono au walifanya bila kutaka. Ushahidi wa kina pia unaonesha kwamba dhuluma za kingono ni tatizo la kawaida nchini Kenya."

utafiti wa kitaifa wa mwaka wa 2010 kuhusu dhuluma dhidi ya watoto nchini Kenya,[28] na ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN) ya mwaka wa 2011 juu ya ubaguzi wa kijinsia nchini[29] zote zinaonesha kuenea kwa CSA na dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya elimu nchini Kenya.

IFC haikuzingatia hatari za CSA zinazoweza kutokea wakati wa mradi, licha ya hatari zinazojulikana za muktadha, wala kuzingatia uwezo wa mteja wake mtarajiwa kukidhi mahitaji ya Kimazingira na Kijamii (E&S) kuhusiana na hatari na athari za CSA. Kutokana na hali hii, IFC haikupendekeza hatua zozote za kukabiliana na hali ili kuhakikisha kwamba Bridge inashughulikia hatari na athari hizo. Aidha, kwa kutotathmini hatari za CSA na athari zinazoweza kutokea za mradi wala uwezo wa mteja kuzishughulikia, IFC haikuwa na msingi wa kudai kwamba mradi unaweza kukidhi mahitaji ya Kimazingira na Kijamii (E&S) ya IFC yanayohusiana na CSA ndani ya muda unaofaa -hali inayohitajika kwa IFC kufanya uwekezaji.[30]

Mambo mahsusi yanayoonyesha kuwa IFC haikuridhia wajibu wake wa kufanya utafiti kabla ya uwekezaji ni pamoja na kushindwa kwake:

- Kutoa wito kwa Bridge iandae au iagize tathmini ya hatari katika jamii kwa kuzingatia ukubwa wa mradi na idadi ya walengwa walio hatarini kuathiriwa na ni pamoja na hatari za CSA na GBV katika jamii (kama inavyotakiwa katika PS1).
- Kutathmini sera na taratibu zilizopo za Bridge za kuzuia na kukabiliana na CSA na GBV na kukabiliana na GIIP na kufuata sheria za Kenya zilizoundwa ili kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono (kama inavyotakiwa na PS1, aya za 6 ns 7 na PS4 aya ya 5).
- Kushughulikia utegemeaji wa Bridge kwa walimu ambao hawakuwa wamesajiliwa na kwa hivyo iliongeza hatari kwa kiwango kikubwa kwa kuwa ulinzi uliopo wa serikali kwa watoto hauwezi kutumika.[31]
- Kutafakari kuhusu mambo yanayoingiliana yanayowafanya wanafunzi kuwa hatarini zaidi, kama vile utambulisho wa jinsia, jinsia, umri, na mambo mengine, na kutathmini ikiwa Bridge iliweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa athari mbaya zinazohusiana na CSA hazikumbi kwa kiasi kikubwa wanafunzi (tayari) waliokuwa hatarini kuathiriwa (kama inavyotakiwa na PS1, aya ya 12).

2. **Wakati wote wa uwekezaji, IFC haikuridhia kikamilifu mahitaji ya Sera ya Uendelevu yanayohusiana na usimamizi (aya ya 45).** Wajibu wa IFC wa kusimamia E&S uliihitaji kufuatilia mara kwa mara kuridhia kwa Bridge kwa mahitaji ya PS yanayohusiana na hatari na athari za CSA zinazohusiana na mradi (aya ya 45, kitone cha 1 na 2) na kufanya kazi na mteja kushughulikia athari mbaya za E&S ambazo zilitokana na

[28] UNICEF, CDC, Jamhuri ya Kenya, na Pamoja kwa Manufaa ya Wasichana, 2010, Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Kenya (VAC). Utafiti huu - ambao unafuatilia maisha kwa jumla na hali ya sasa ya watoto wa kike 1,227 na wakiume 1,456 kati ya umri wa miaka 13 hadi 24 waliodhulumiwa kabla ya umri wa miaka 18 - unawakilisha utafiti wa kisasa zaidi na wa kina kuwahi kufanywa kuhusu kuenea kwa dhuluma za kingono, kimwili na kisaikolojia kwa watoto chini ya miaka 18 nchini Kenya. Unapatikana hapa: https://evaw-global-database.unwomen.org/-/media/files/un%20women/vaw/full%20text/africa/kenya%20violence%20against%20children%20survey%20%202010.pdf?vs=1219.

[29] Uchunguzi wa mwisho wa Kamati ya Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake, 2011, CEDAW/C/KEN/CO/7. Unapatikana hapa: https://www2.ohchr.org/english/bodies/cedaw/docs/co/CEDAW-C-KEN-CO-7.pdf.

[30] IFC, Januari 1, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, ibara za 20-28). Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-policy-on-environmental-and-social-sustainability-2012-en.pdf.

[31] Hitaji la kuwa na walimu waliosajiliwa kwa idadi ya kutosha huchangia kupunguza hatari kwa watoto kwa kuwa walimu waliosajiliwa mbali na kuwa na shahada ya taaluma ya elimu ambayo iliwapa mafunzo kuhusu jinsi ya kufanya kazi kwa usalama na watoto pia lazima watoe cheti cha mwenendo mzuri na fomu ya matibabu, na wahalifu wa ngono wanaopatikana na hatia huwa hawasajiliwi. Mahitaji ya Usajili na Uajiri wa Walimu. Yanapatikana hapa: https://www.tsc.go.ke/index.php/services/teacher-registration/registration. Tazama, pia, Kanuni za Kufuatwa za Tume ya Kuajiri Walimu za mwaka wa 2015, kifungu cha 20. Zinapatikana hapa: http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/LegalNotices/196-Teachers_Service_Commission_Regulations__2015.pdf, na TSC Circular, 3/2010. Zinapatikana hapa: https://www.tsc.go.ke/index.php/downloads-b/file/22-circular-on-protection-of-pupils-students-from-sexual-abuse-2010.

mabadiliko ya hali ya shughuli za biashara (aya ya 45, kitone cha 3). Sera ya Uendelevu pia iliitaka IFC kumtaka mteja wake kufanyia marekebisho Mfumo wake wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESMS) ili kushushughulikia mabadiliko ya nyenzo katika vigezo vya hatari ya E&S vya mradi (aya ya 25) kwa namna inayorandana na Mfumo wa Uendelevu wa IFC. Usimamizi wa IFC haukufuata kikamilifu majukumu haya, kama ilivyoelezewa hapo chini.

a. **Kabla ya uchunguzi wa nyanjani wa CAO wa Februari mwaka wa 2020 wa Bridge-01, IFC ilishindwa kufuatilia mara kwa mara au kushughulikia kwa kiasi kikubwa hatari na athari za CSA na GBV zinazohusiana na mradi na mteja wake.** Mapungufu haya yaliendelea licha ya IFC kuarifiwa kuhusu matukio ya CSA mwaka 2013, 2016, na 2017, na licha ya utafiti wa 2019 unaoonesha kuenea kwa CSA na GBV dhidi ya watoto nchini Kenya.[32] Hasa, IFC ilitepetea kwenye majukumu yake chini ya aya ya 25 na 45 ya Sera ya Uendelevu kwa: (1) kutotathmini kubadilika kwa hali ya hatari katika jamii kwa kuzingatia matukio yaliyoripotiwa ya CSA wala kumtaka mteja wake kurekebisha ESMS yake ili kushughulikia hatari na athari za CSA; na (2) kutotathmini utoshelevu wa sera na mfumo wa mikakati ya Bridge ya kushughulikia CSA na GBV zinazoweza kutokea. Baada ya kufahamu kuhusu matukio mahususi, IFC ilipaswa kumtaka mteja wake kurekebisha ESMS zake ili kujumuisha uzuiaji na ushughulikiaji wa athari na hatari za CSA, na kuanzisha na kutekeleza mpango wa kawaida wa kusimamia ushughulikiaji wa hatari za CSA. Kwa kuongezea, IFC ilipaswa kufanya kazi na Bridge ili kuhakikisha utekelezaji wa hatua zifuatazo zinazorandana na Viwango vya Utendakazi vya 1 na 4:

- Mfumo wa kutathmini na kusimamia CSA na hatari zinazoingiliana za GBV dhidi ya watoto (PS1, aya ya 5) na kufidia au kushughulikia athari zozote mbaya kwa wanafunzi (PS1, aya ya 14.)
- Mchakato wa kutambua hatari za mradi zinazohusiana na CSA na GBV dhidi ya watoto kurandana na GIIP (PS1, aya ya 7).
- Hatua mahsusi za kuzuia na kudhibiti CSA na GBV zinazorandana na GIIP na kuzingatia hali na ukubwa wa hatari na athari zinazohusiana na mradi katika maeneo haya (PS4 aya ya 5).

b. **Kuanzia Machi mwaka wa 2020, usimamizi wa IFC uliboreshwa, lakini mapungufu yaliendelea kushuhudiwa.** Mwezi mmoja baada ya uchunguzi wa CAO wa Bridge-01 nyanjani mwezi wa Februari mwaka wa 2020 kuripoti matukio kadhaa ya madai ya CSA kwa IFC, IFC ilifanya ziara ya usimamizi nyanjani kwa shule ya Bridge nchini Kenya iliyolenga hatari za kudhulumiwa kwa watoto na usalama wa watoto katika mazingira ya shuleni. Kwa mara ya kwanza, IFC ilichunguza kwa makini na kuzingatia mbinu na uwezo wa Bridge kushughulikia CSA. IFC ilitambua na kuwasilisha maeneo muhimu ya kuboreshwa kwa Bridge na kupendekeza mipango ya kushughulikia pamoja maswala yanayohusu afya ya mtoto, usalama, na ushughulikiaji wa matukio ya CSA. Hata hivyo, juhudi za usimamizi za IFC ziliendelea kuwa na mapungufu ya mahitaji ya Sera ya Uendelevu kwa njia kadhaa:

- **Ufikiaji wa IFC kwa taarifa za mteja kuhusu ulinzi na usalama wa watoto ulikuwa muhimu kwa kazi yake ya usimamizi, lakini IFC ilishindwa kuhakikisha kwamba ilipokea na kukagua taarifa zote zinazohitajika.** Taarifa ambayo CAO ilipata inaonesha kwamba IFC ilikumbana na changamoto za kufikia stakabadhi za mteja, na wakati mwingine haikupokea stakabadhi zilizoitishwa, na kwa hivyo kutoweza kukagua stakabadhi muhimu katika kutekeleza wajibu wake wa usimamizi. Hii iliathiri uwezo wa IFC wa kusimamia mradi kwa ufanisi na kuamua kwa usahihi ikiwa mradi uliridhia Viwango vya Utendakazi vya IFC. Kwa kuongezea, IFC haikutilia maanani mbinu za kurekebisha hali hii, kama

[32] UNICEF, 2019, Utafiti Nchini Kenya wa Ukatili Dhidi ya Watoto (VACS). Unapatikana hapa: https://www.unicef.org/kenya/media/1516/file/2019%20Violence%20Against%20Children%20Survey%20(VACS)%20.pdf.

vile kuzingatia haki zake za kuomba rufaa (ikiwa zipo) chini ya Sera ya Uendelevu ya IFC (aya ya 45) au stakabadhi zake za shughuli na Bridge.

- **IFC haikusimamia ushughulikiaji wa mteja wa hatari na athari zinazohusiana na CSA kwa kuzingatia Viwango vya Utendaji vya IFC vya 1 na 4.** Mwezi wa Septemba mwaka wa 2021, IFC ilibainisha kuwa Bridge iliridhia Viwango vya Utendakazi vinavyohusiana na GBV na dhuluma na ukatili wa unyanyasaji wa kingono (SEAH). CAO inabainisha kuwa IFC ilifanya uamuzi huu ingawa inaonekana mteja alishindwa kutekeleza mapendekezo yote ya kushughulikia hatari za CSA/GBV ambazo IFC ilipendekeza kati ya mwaka wa 2020 na mwaka wa 2021. CAO inaonelea kwamba maamuzi ya IFC hayakutegemea taarifa za kutosha kwa kuwa haikuwa imekagua stakabadhi muhimu ili kufanya uamuzi kuhusu kuridhia, hasa kuhusiana na utekelezaji wa mfumo wa mteja wa ushughulikiaji wa hatari za CSA.[33] [34] Baada ya Septemba mwaka wa 2021, IFC haikutoa mapendekezo zaidi ya kuboresha hali kwa Bridge.
- IFC ilishindwa kumsimamia mteja vya kutosha kushughulikia athari za CSA zilizojitokeza. Mapungufu ya usimamizi wa IFC pia yalionekana kupitia kushindwa kufanya kazi na mteja ili kushughulikia kikamilifu athari zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi. Kwa mfano, Kiwango cha Utendakazi cha 1 kinahitaji mteja kulipa fidia kutokana na athari zilizobaki kwa jamii zilizoathiriwa - katika hali hii waathirika wa CSA na GBV.[35] CAO haikupata ushahidi kwamba IFC ilimtaka mteja wake kufanya hivvyo au kuchukua hatua nyingine madhubuti kushughulikia athari za CSA ambazo zilizojitokeza.

Kwa kuongezea, uchunguzi wa CAO unabainisha kuwa mwanzoni mwa mwaka wa 2020, IFC ilipokea habari ambayo ilionyesha kuwepo kwa visa 70 vya CSA. CAO haijaona taarifa hizi. Kilicho wazi, hata hivyo, ni kwamba taarifa iliyoko kwenye stakabadhi hii ilikuwa "hali ya hatari" ambayo ilimfanya mfanyakazi wa IFC kutambua kuwa kunaweza kuwa na uwezekano wa matukio zaidi ya CSA na taarifa hiyo haikushughulikiwa na IFC.

## Madhara

IFC ilifahamu kuhusu visa kadhaa vya unyanyasaji wa watoto kingono, vilivyohusisha waathirika 23, wakati ilipositisha uwekezaji wake mwezi wa Machi mwaka wa 2022. CAO inabainisha kuwa, katika visa vyote isipokuwa kimoja, unyanyasaji huo ulitokea baada ya IFC kuwekeza kwa Bridge na wakati wa kipindi cha usimamizi ambapo IFC ilipaswa kufanya kazi na mteja ili kuendeleza na kutekeleza mikakati ya kutathmini na kudhibiti hatari na athari zinazohusiana na usalama na ulinzi wa watoto, ikiwa ni pamoja na CSA. Mbali na waathirika 23 wanaojulikana, kuanzia mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2021, IFC ilifahamu kuhusu visa zaidi vya CSA. Madhara kwa mwili na ya kisaikolojia ya CSA yanafahamika vizuri. Waathiriwa wa CSA huteseka milele na kuna uwezekano wa kuathiriwa kizazi baada ya kizazi, ikiwa ni pamoja na madhara makubwa ya kudumu kwa ukuaji wao wa mwili, hisi, kijamii na kihisia, pamoja na shida za kiuchumi kutokana na kupoteza tija, ulemavu, na kupungua kwa ubora wa maisha.

---

[33] IFC ilizingatia GIIP inayohusiana na CSA na GBV na inayotumika kwa sekta binafsi ya elimu ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini kama "kiwango muhimu" ambacho hakikuhitajika kwa "ridhaa msingi" na mahitaji ya mradi ya E&S. Hiki ni kinyume cha PS1, ambayo inahitaji kwamba utambuzi na tathmini ya hatari na athari na "…itaanzisha hatua za kuzuia na kudhibiti zinazorandana na mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (GIIP)." Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

[34] PS1, aya ya 5, 2012, inahitaji kwamba "wateja sharti wafuate sheria za kitaifa zinazotumika." PS4, 2012, inahitaji kwamba mteja atathmini hatari na athari na kubainisha mikakati ya kuzuia na kudhibiti "inayorandana na mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (GIIP)." Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

[35] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, Malengo na ibara ya 14. Vinapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

**Sababu Kuu za Kutoridhia**

CAO inaona kuwa sababu kuu zifuatazo zilisababisha uchukuaji au kutochukua hatua na IFC na kupelekea kutoridhia kama ilivyobainishwa hapo juu:

- **Kutofanya utafiti wa kutosha kabla ya mradi:** Mchakato wa ESDD wa IFC haukutambua wala kutathmini hatari na athari za CSA na GBV, licha ya hatari za CSA zinazojulikana kutokana na hali na muktadha. Kwa hivyo, hakukuwa na uchambuzi wa uwezo wa mteja kushughulikia hatari hizi na hakuna ujumuishaji wa hatua zozote za kukabiliana nazo au za kuzipunguza katika Mpango wa Utekelezaji wa Mazingira na Jamii uliokubalika.[36] Hii kwa upande wake ilidhoofisha uwezo wa IFC wa kumsimamia mteja wake vyema na pia inaweza kuwa ilichangia mteja kusisitiza kwamba CSA na GBV hazikushughulikiwa na Mfumo wa Uendelevu wa IFC alipotakiwa kushughulikia maswala haya.
- **Ukosefu wa wataalamu:** Kikosi cha mradi wa IFC kilikosa wataalamu wa kushughulikia hatari katika jamii zinazohusiana na CSA na GBV wakati mwingi wa uwekezaji, na kuwa kizingiti kwa uwezo wake wa kutambua na kufuatilia vyema hatari na athari zinazohusiana na mradi katika maeneo haya. Wataalamu wawili wenye maarifa ya GBV (mmoja wao pia alikuwa na maarifa ya CSA) walifanya kazi kama sehemu ya kikosi cha uwekezaji katika kazi za kipekee mapema mwaka wa 2020 na Juni mwaka wa 2021, mtawaliwa. Kushiriki kwao kulitokea miezi 16 baada ya ziara ya CAO nyanjani kufanya uchunguzi wa Bridge-01 ulipobaini visa viwili vya CSA vilivyohusisha waathirika 15.
- **Ukosefu wa taarifa:** Ugumu kwa IFC kupata taarifa iliyoomba mteja wake kuhusu visa vya CSA katika masuala yanayohusiana na CSA ilifanya kuwa vigumu kwa juhudi za kusimamia na kushirikiana na kampuni vizuri kushughulikia masuala yanayohusiana na CSA. Stakabadhi nyingi za E&S zilitolewa tu kupitia mtindo salama wa data za kielektroniki unaozuia watumiaji kupakua au kuchapisha stakabadhi, ambapo wakati mwingine zilipatikana kwa muda tu kwa watumiaji mahususi na kufuatilia majina ya watumiaji na tarehe na muda ambao hati zilipitiwa. CAO iliarifiwa kuwa hii iliathiri uwezo wa IFC wa kupata habari muhimu kwa ufanisi na kufanya kukagua na kuchambua stakabadhi za mteja kuwa kazi ngumu.
- **Mwelekeo wa kitaasisi**: IFC inaonekana kutoelewa mfumo wa kitaasisi kuhusu mambo kama haya katika Kundi pana la Benki ya Dunia. Katika mwaka wa 2016, Rais wa WBG Jim Yong Kim alizindua kikosi kazi cha GBV/SEAH ili kukagua hatari na athari za GBV zinazoweza kutokea katika Benki ya Dunia kama sehemu ya kukabiliana na visa vya GBV vilivyoshughulikiwa na uchunguzi wa Jopo la Kufanya Uchunguzi katika Mradi wa Sekta ya Uchukuzi nchini Uganda.[37]
- **Kujiondoa kwa mradi:** Kulikuwa na ukosefu wa uwazi katika kikosi cha IFC kuhusu jinsi kuridhia kwa Viwango vya Utendakazi unavyopaswa kushughulikiwa katika muktadha wa kujiondoa. Hii ilichangia kutokuwa na uhakika kuhusu jinsi ya kuwasiliana na mteja kuhusu kuridhia PS wakati ambapo kujiondoa kulikuwa kunajadiliwa[38].

[36] ESAP inawakilisha hatua zilizokubaliwa kati ya IFC na mteja wake.

[37] WGB, Julai 31, 2017, Ripoti ya Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Unyanyasaji wa Kijinsia. Inapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/482251502095751999/pdf/117972-WP-PUBLIC-recommendations.pdf. Tazama pia taarifa katika Toleo la Habari la Benki ya Dunia, Oktoba 2016, Benki ya Dunia Yazindua Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia. Zinapatikana hapa: https://www.worldbank.org/en/news/press-release/2016/10/13/world-bank-launches-global-task-force-to-tackle-gender-based-violence.

[38] Kujiondoa kwa IFC kutoka kwa shule za Bridge lilikuwa jaribio la kwanza kwa IFC kujaribu kutumia kanuni bora kujiondoa kama zoezi la majaribio.

## Mapendekezo ya CAO kwa IFC

Kwa kuzingatia Sera ya CAO, Menejimenti ya IFC itaandaa Mpango Kazi wa Menejimenti (MAP) kushughulikia matokeo ya kutoridhia na madhara yanayohusiana katika ripoti hii. Kwa kufanya hivyo, CAO inapendekeza kwamba IFC izingatie hatua zifuatazo kwa kuzingatia mradi na taasisi.

**Mapendekezo Kutegemea Mradi Mahususi**

Kwa kuzingatia mradi, mapendekezo ya CAO yanalenga kuwezesha kutoa suluhisho kwa waathirika wa CSA na familia zao na kusaidia kushughulikia hatari zozote zinazoweza kuendelea kutokea.

1. **Kushughulikia waathirika wa CSA.** IFC inapaswa kushirikiana na Bridge kuanzisha kituo cha Dharura cha Kulinda Watoto (ECPR) ili kusaidia mchakato wa kuwezesha waathirika na familia zao kuweza kushughulikia hali. CAO inabainisha kuwa Benki ya Dunia ilisaidia kukuza ECPR chini ya Mpango Kazi wa Menejimenti (MAP) uliotokana na Jopo la Kufanya Uchunguzi katika Sekta ya Uchukuzi nchini Uganda.[39] ECPR inapaswa, angalau, kutoa yafuatayo kwa waathirika wa mradi uliofadhiliwa na IFC:

   - Ushauri kwa waathirika na familia zao
   - Msaada wa huduma za afya, ikiwa ni pamoja na huduma za afya ya sehemu nyeti na afya ya uzazi na matibabu ya magonjwa ya zinaa
   - Msaada wa ujumuishaji wa jamii ili kuwezesha waathirika kuendelea na elimu au juhudi za waathirika kutafuta ajira nzuri pale ambapo CSA imetinga shughuli kama hizo
   - Ufadhili na kuelekezwa kwa huduma za kisheria kwa familia zinazotafuta sheria kuchukuliwa dhidi ya wahalifu
   - Mfumo unaowezesha waathirika kujitokeza, kujitambulisha ikiwa wanataka, na kukubali hatua yoyote ya kurekebisha mambo ambayo itatolewa kwao
   - Kufidiwa kifedha, kama inavyofaa.

   Hatua za kukabiliana na hali zinapaswa kulinda usiri wa walalamishi na kuwalinda walalamishi na familia zao dhidi ya hatari yoyote ya vitisho au kulipiza kisasi. Katika kuendeleza ECPR yake, CAO inahimiza sana IFC kuzingatia kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yana maarifa mwafaka kuhusu eneo, uwezo na yanayoaminiwa na jamii husika ili kufanikisha utekelezaji wa mchakato wa kufidiwa.

2. **Kuimarisha ushughulikiaji wa jamii wa CSA na GBV dhidi ya watoto katika jamii ambazo mradi unatekelezwa.** IFC inapaswa kushirikiana na Bridge ili kusaidia kuzuia madhara ya baadaye yanayohusiana na mradi kwa kuwezesha utoaji wa mafunzo kupitia hatua za mabadiliko ya tabia za jamii ili kupunguza kukubalika kwa CSA na GBV dhidi ya watoto katika jamii. Mafunzo yanapaswa kutafuta kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa Bridge na watoto wa eneo hilo kujikinga dhidi ya hatari za CSA na GBV na kutafuta msaada wa kutosha ikiwa watapitia hali hii. Kwa kuongezea, mafunzo ya kukabiliana na CSA na GBV dhidi ya watoto yanapaswa kujumuisha wazazi; vikosi vya afya vya eneo husika; watoa huduma za afya ya akili; machifu wa eneo husika na viongozi wengine wa jamii; polisi, majaji, na maafisa wengine wa utekelezaji wa sheria; na

[39] Jopo la Ukaguzi la Benki ya Dunia, Agosti 4, 2016, Ripoti ya Uchunguzi wa Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi nchini Uganda. Inapatikana hapa: https://www.inspectionpanel.org/sites/default/files/ip/PanelCases/98-Inspection%20Panel%20Investigation%20Report.pdf.

viongozi wa kidini na kitamaduni. Mafunzo ya aina hii yanapaswa kutolewa katika jamii zote zilizo na shule za Bridge.

**Mapendekezo ya Ngazi ya Taasisi**

Uchunguzi huu ulionyesha sababu kadhaa za msingi za kutoridhia ambazo zinaweza kunufaika na hatua za kushughulikia hali za IFC, kama ifuatavyo.

3. **Kupitia miradi yake yote ili kutambua miradi yote ambapo watoto wako hatarini zaidi na wanaweza kuathiriwa katika jamii zinazoathirika ili kutambua na kutathmini ikiwa hatua mwafaka za ushughulikiaji wa hatari katika jamii zipo na zinatekelezwa.** Mahali ambapo hazipo, IFC inapaswa kufanya kila juhudi ili kuwezesha mradi uliofadhiliwa kuridhia, ikiwa ni pamoja na:

   - Kushirikiana na mteja husika kutambua hatua za kushughulikia CSA na GBV ambazo hazijatekelezwa au ambazo hazikutambuliwa wakati wa utafiti wa kabla ya mradi, na kumsaidia mteja kubuni na/au kutekeleza hatua hizo

   - Kupitia upya mikataba ya uwekezaji ili kubaini: (1) kwamba hatua za usalama wa watoto na ulinzi wa watoto ni sharti zizingatiwe ndani ya wigo wa majukumu yote ya E&S ya wateja; na (2) kwamba sababu zozote za kuaminika za kuamini kuwa unyanyasaji wa watoto kingono umetokea lazima ziripotiwe mara moja kwa wataalamu wa E&S wa IFC

   - Kufanyia Marekebisho Vielelezo vya Ukaguzi wa Ufuatiliaji wa Kila Mwaka ili kujumuisha taarifa na kushughulikia maswala yanayohusiana na dhuluma dhidi ya watoto-ikiwa ni pamoja na CSA na GBV.

4. **Kuimarisha na kufafanua vifungu vya E&S kuhusu watoto, pamoja na madhara tofauti ya kijinsia na kingono, ndani ya Mfumo wa Uendelevu. IFC inapaswa kufanyia marekebisho Mfumo wake wa Uendelevu ili kujumuisha yafuatayo:**

   - Vifungu vipya katika Viwango vya Utendakazi ambavyo vinalenga na kuelezea zaidi majukumu ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa mteja na kuwataka wateja kushughulikia na kurekebisha madhara yoyote yanayohusiana na mradi kwa watoto.

   - Vifungu vipya katika Sera ya Uendelevu vinavyohusu watoto tu na madhara yanayotofautishwa ya kijinsia na kingono ambavyo vinaelezea majukumu ya IFC katika suala la kutambua, kuepuka, kupunguza, na kukabiliana na hatari za mradi na athari mbaya kwa watoto na watu wengine walio hatarini zaidi kuathiriwa, ikiwa ni pamoja na wanawake na wasichana, watu wa LGBT+, watu maskini, wazee, watu wenye ulemavu, makabila madogo, watu wa kiasili, na watu wengine walio hatarini zaidi kudhulumiwa, kubaguliwa kijinsia, au aina nyingine za madhara yanayotokana na miradi inayofadhiliwa na IFC.

5. **Kufanya juhudi za kujengea uwezo taasisi nzima ili kuzuia CSA na aina zinazoingiliana za GBV kutokea katika miradi yake ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na:**

   - Mafunzo na uhamasishaji kuhusu uzuiaji wa GBV na CSA kwa wafanyikazi wote wa IFC wanaoshughulikia mradi. Mafunzo ya aina hii yanapaswa kufanywa mara kwa mara; kusasishwa kama GIIP inayohusiana na ulinzi wa watoto, usalama wa watoto, na mabadiliko ya kuzuia GBV; na yaundwe ili kushughulikia kwa haraka na na kwa njia mwafaka masuala yoyote yanayoibuliwa kuhusiana na GBV na CSA wakati wa uwekezaji.

- Ukuzaji wa nyenzo za mwongozo kuhusu dhuluma dhidi ya watoto unaorandana na mbinu zilizosawazishwa za WBG. IFC inapaswa kuandaa mwongozo mahususi wa kudhibiti hatari za dhuluma dhidi ya watoto katika miradi yake yote, kwa kuzingatia sana CSA, kwa kutumia uzoefu wa Benki ya Dunia wa kushughulikia CSA na GBV zinazohusiana.

6. **Kuanzisha kikosi kazi cha kimataifa cha GBV ili kushauri IFC** kuhusu kuimarisha mbinu yake ya kutambua na kushughulikia GBV katika uwekezaji wake wote, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono utekelezaji wa mapendekezo yaliyofafanuliwa hapo juu. Kikosi kazi kinapaswa kuwa na wataalamu madhubuti kuhusiana na uzuiaji wa unyanyasaji wa watoto kingono na kinapaswa kujumuisha wataalamu anuwai wa ndani na nje ya taasisi.

7. **Kufafanua matarajio ya mradi kuridhia Viwango vya Utendakazi wakati IFC inapopanga kujiondoa.** Vigezo vya kujiondoa kwenye mradi wakati PS haijaridhia Viwango vya Utendakazi vinapaswa kujumuishwa katika Rasimu ya Kanuni za Kujiondoa za IFC.

Katika kuwasilisha mapendekezo yaliopo hapo juu, CAO inasisitiza kwamba mapendekezo ya ngazi ya taasisi na mafunzo kutokana na matokeo ya ripoti hii ni muhimu kwa utendakazi wa jumla wa E&S za IFC hata nje ya sekta ya elimu. Kwa hivyo, yanabaki kuwa muhimu licha ya tangazo la IFC la Mei mwaka wa 2022 kwamba itaepuka kufanya uwekezaji wowote katika sekta binafsi ya K–12 katika siku zijazo.[40]

## Hatua zinazofuata

Baada ya kukamilisha uchunguzi wake, IFC imetuma ripoti hii kwa Menejimenti ya IFC. Kwa kuzingatia Sera ya CAO, Menejimenti ya IFC itaandaa Ripoti ya Usimamizi ambayo itajumuisha, kwa idhini ya Bodi, Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Menejimenti (MAP) kutokana na matokeo ya CAO ya kutoridhia na Madhara yanayohusiana. MAP itajumuisha hatua za kushughulikia hali kwa kipindi maalum zilizopendekezwa na Menejimenti. Ripoti ya uchunguzi wa ridhaa, Ripoti ya Menegimenti, na MAP zitatolewa kwa umma, na CAO itafuatilia utekelezaji kikamilifu wa mambo yaliojumuishwa kwenye MAP.

[40] IEG, Juni 2022, Tathmini ya Uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa katika Shule Binafsi za K–12; na IFC, 2022, Ushugulikiaji wa Menejimenti wa Ripoti ya IEG. Inapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/sites/default/files/Data/Evaluation/files/IFCSupport_K12PrivateEducation_GS_and_MC.pdf.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/evaluations/evaluation-international-finance-corporation-investments-K–12-private-schools-7.

# 1. USULI

Sehemu hii inatoa muktadha wa elimu na uwekezaji nchini ambamo IFC ilichukulia Bridge International Academy ("Bridge," "mteja," au "kampuni") kama mteja na kutoa muhtasari wa historia ya uwekezaji. Kisha inaeleza usuli uliopelekea uchunguzi wa CAO wa mbinu ya IFC kuhusu hatari na athari zinazoweza kutokea kuhusiana na unyanyasaji wa watoto kingono kutokana na shughuli za Bridge nchini Kenya na kutoa ratiba ya matukio muhimu. Hatimaye, inaelezea mbinu ya CAO na uendeshaji wa uchunguzi, ikijumuisha ufafanuzi wa istilahi muhimu na vikwazo kwa ukusanyaji wa taarifa.

## 1.1. Muktadha Nchini na katika Sekta ya Elimu

Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN) ni pamoja na kuhakikisha kwamba watoto wote wanamaliza elimu ya msingi na sekondari bila malipo, kwa usawa na ya kiwango cha juu kufikia mwaka wa 2030 (Lengo la 4). Hata hivyo, serikali katika nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati zimetatizika kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la watu, na kupelekea msongamano wa watoto shuleni au ukosefu wa kutimiza mahitaji ya kutosha. Ili kusaidia kukidhi mahitaji, wahusika wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na taasisi, wafadhili, wawekezaji wa sekta binafsi, na taasisi za fedha za maendeleo, wameshirikiana na makampuni ya biashara ili kutoa elimu ya gharama nafuu kwa watoto wasiojimudu.[41] Kenya, ambapo zaidi ya watoto milioni 1.13 wenye umri wa miaka kati ya 6 na 13 hawakuwa shuleni mwaka wa 2020,[42] ni miongoni mwa nchi ambazo Bridge iliona fursa kubwa ya kutoa huduma za elimu ya gharama nafuu kwa kupata faida.

Sababu nyingine muhimu ya kimuktadha ya uwekezaji wa IFC katika sekta hii ni kwamba mazingira mbalimbali ya shule huwa na hatari zinazojulikana na kuenea za unyanyasaji wa kijinsia—kote ulimwenguni[43] na hasa nchini Kenya. Kati ya nchi 153 zilizoangaziwa katika Ripoti ya Pengo la Jinsia Duniani ya mwaka wa 2020, Kenya iliorodheshwa nambari 109, ikiwa na alama 0.671, hali inayowakilisha ukosefu mkubwa wa usawa katika upataji wa elimu matokeo ya afya, na ushiriki katika soko la ajira.[44] Licha ya marekebisho ya hivi majuzi ya sheria na sera kuhusiana na usawa wa kijinsia katika sekta zote, wanawake na wasichana waliobalehe wanasalia kuwa kundi lililo hatarini zaidi nchini Kenya,[45] na watoto wanasalia katika mazingira magumu zaidi shuleni. Katika utafiti wa serikali wa mwaka 2019 ulioungwa mkono na UNICEF, asilimia 49 ya wasichana na asilimia 48 ya wavulana wenye umri wa miaka kati ya 13 na 17 waliripoti kudhulumiwa mwili, na asilimia 11 ya wasichana na asilimia 4 ya wavulana waliripoti kupitia unyanyasaji wa kijinsia.[46] Serikali ya Kenya ilishughulikia hali hii kupitia Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia na Kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Watoto unaoendelea, ambao unajumuisha kukuza na kuimarisha "mazingira salama, yalio na usalama na mazuri shuleni."[47]

IFC ilipowekeza kwa Bridge mwaka wa 2014, taasisi za Benki ya Dunia hazikuwa na ufafanuzi wa wazi kuhusu unyanyasaji wa watoto kingono (CSA) katika stakabadhi zinazotoa mwongozo kuhusu ushughulikiaji wa hatari

[41] Ibid.
[42] Taasisi ya Takwimu ya UNESCO, 2021, *Mpango wa Wasio Shuleni Ulimwenguni (OOSCI): Utafiti Nchini Kenya.*
[43] UN, 2006, Ripoti ya Mtaalam wa Kujitegemea wa Umoja wa Mataifa: Utafiti kuhusu Ukatili Dhidi ya Watoto Iliyowasilishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, A/61/299. Inapatikana hapa: https://documents-dds-ny.un.org/doc/UNDOC/GEN/N06/491/05/PDF/N0649105.pdf?OpenElement.
[44] USAID, Aprili 2020, Makala ya Ukweli kuhusu Usawa wa Jinsia na Kujengea Wanawake Uwezo. Yanapatikana hapa: https://www.usaid.gov/kenya/document/gender-equality-female-empowerment-kenya.
[45] Ibid.
[46] UNICEF, 2019, Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Nchini Kenya (VACS). Unapatikana hapa: https://www.unicef.org/kenya/reports/The-2019-Violence-Against-Children-Survey.
[47] UNICEF, Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia na Kushughulikia VAC 2019-2023, p38. Unapatikana hapa: https://www.unicef.org/kenya/media/1526/file/National%20Prevention%20&%20Response%20Plan%20on%20VAC.pdf

kwa mazingira na jamii. Hata hivyo, hali hii ilibadilika wakati wa usimamizi wa IFC wa uwekezaji huu. Kufuatia unyanyasaji wa watoto kingono unaohusiana na mradi wa sekta ya uchukuzi nchini Uganda, aliyekuwa wakati huo Rais wa Benki ya Dunia Jim Yong Kim alizindua Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Unyanyasaji wa Kijinsia cha Benki ya Dunia, ambacho matokeo yake yalionyesha wazi kuwa shule ni miongoni mwa maeneo ambayo watoto wako hatarini kunyanyaswa kingono.[48] Mapendekezo ya Kikosi Kazi hiki ni pamoja na kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa hatari zinazohusiana na mradi za unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia (GBV). Baadaye, Benki ya Dunia iliunda Makala ya Mwenendo Mzuri wa kushughulikia hatari za ukatili na unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia (SEA/SH) kwa kazi za miradi ya umma (2018) na sekta za elimu na afya (Septemba 2022). [49]

Huu ndio muktadha wa kitaasisi nchini na wa Kundi la Benki ya Dunia (WBG) ambapo IFC ilifanya utafiti wake wa kabla ya uwekezaji na usimamizi wake katika shule za Bridge International Academies.

## 1.2. Uwekezaji wa IFC

Wakati wa kipindi cha uwekezaji, Bridge International Academies ilimiliki na kuendesha msururu mkubwa zaidi wa shule za kibinafsi za gharama nafuu barani Afrika. Mteja wetu ni kampuni tanzu nchini Kenya inayomilikiwa kikamilifu na NewGlobe Schools, Inc (NGS), iliyoanzishwa mwaka wa 2009 na yenye makao yake katika jimbo la Delaware, nchini Marekani.[50] Katika mwaka wa 2021, shughuli za Bridge zilijumuisha kuendesha shule binafsi takribani 161 za msingi na sekondari, "shule za jamii" kote nchini Kenya, Nigeria, na Uganda, pamoja na idadi ndogo ya shule za ubia na mashirika yasiyo ya serikali (NGO) nchini India na Kenya. NGS pia hutoa huduma za elimu kupitia ubia na shule zinazoendeshwa na serikali nchini China, Liberia, Nigeria na Rwanda.[51]

Katika mwaka wa 2013, IFC ilitambua Bridge ilikuwa na uwezo wa kuwa mteja, kwa kuzingatia mbinu ya IFC ya wakati huo ya kuwekeza katika shule zinazopata faida zinazohudumia jamii za kipato cha chini. Wakati huo, Bridge iliendesha shule 211 zinazohudumia wanafunzi 57,000 nchini Kenya, na lengo la kutoa elimu kwa watoto kutoka kwa familia zinazopata chini ya dola 2 za Marekani kwa kila mtu kwa siku.[52]

Uchunguzi wa IFC wa kabla ya uwekezaji ulielezea mfumo wa Bridge kama kujenga shule za kibinafsi katika jamii zilizo na idadi kubwa ya watu, wenye kipato cha chini na kutumia "maandalizi ya mitaala katika eneo moja, kutoa mafunzo kwa walimu na jukwaa la teknolojia ya kina ili kutoa elimu bora kwa gharama nafuu."[53] IFC ilitarajia mradi huu kuwezesha upatikanaji wa elimu msingi, kupelekea uwezo wa kumudu karo, kuimarisha ubora

---

[48] WGB, Julai 31, 2017, Ripoti ya Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Unyanyasaji wa Kijinsia. Inapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/482251502095751999/pdf/117972-WP-PUBLIC-recommendations.pdf. Tazama pia taarifa katika Toleo la Habari la Benki ya Dunia, Oktoba 2016, Benki ya Dunia Yazindua Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia. Zinapatikana hapa: https://www.worldbank.org/en/news/press-release/2016/10/13/world-bank-launches-global-task-force-to-tackle-gender-based-violence.

[49] WBG, Septemba 28, 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia; na WBG, Septemba 2022, Kushughulikia Dhuluma na Ukatili wa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono (SEA/SH) katika Operesheni za Maendeleo ya Binadamu. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na hapa: https://thedocs.worldbank.org/en/doc/0e0825d39c28f61080380c6be9c40811-0290032022/original/SEA-SH-GPN-for-HD-Operations-CESSO-Issue-Version-September-26-2022.pdf.

[50] IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Taarifa za Uwekezaji (SII). Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies; na IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Tathmini ya Mazingira na Jamii (ESRS). Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.

[51] NGS, Historia ya NewGlobe. Inapatikana hapa: https://newglobe.education/history/.

[52] IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Taarifa za Uwekezaji (SII). Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies.

[53] IFC, Oktoba 30, 2013, Muhtasari wa Tathmini ya Mazingira na Jamii (ESRS). Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.

wa elimu na uwajibikaji, kubuni nafasi za kazi, na kuboresha lishe ya wanafunzi.[54] Ungefaulu, IFC ilitarajia kuwa mradi huo ungetoa "athari ya kuigwa," na kuvutia makampuni mengine katika sekta hii kutumia mikakati sawia.[55]

Desemba mwaka wa 2013, Bodi ya Wakurugenzi wa IFC iliidhinisha uwekezaji wa hisa zilizopendelewa wa dola za Marekani milioni 10 ili kukuza msururu wa shule za Bridge nchini Kenya na kusaidia upanuzi wa kampuni hii hadi katika nchi tatu mpya.[56] Uwekezaji huu wa kwanza katika NGS ulifanywa Januari mwaka wa 2014 (mradi #32171), ukifuatiwa na uwekezaji wa jumla ya dola milioni 3.5 za ziada mwezi wa Julai na wa Novemba mwaka wa 2016 (miradi #38733, #39170, na #39224). Wawekezaji wengine ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola, Gates Frontier LLC, Muungano wa Kitaifa wa Elimu, Mtandao wa Omidyar, na Mpango wa Chan Zuckerberg. [57]

IFC iliorodhesha uwekezaji kwa Kundi B la Hatari za Kimazingira na Kijamii, kuonesha kuwa uwezekano wa hatari zake kuwa mbaya zaidi kwa Mazingira na Jamii (E&S) ulikuwa "mdogo", kwa kiasi kikubwa zingeweza kushughulikiwa, na zinaweza kupunguzwa kwa urahisi.[58] Kufuatia kuondoka kwa IFC mwezi wa Machi mwaka wa 2022, IFC ilikuwa na uhusiano usio wa moja kwa moja na shule za Bridge kupitia taasisi ya kifedha iliowaunganisha, Learn Capital Venture Partners Fund III (mradi #32429),[59] ambapo IFC ilijitolea kutoa mtaji ya Dola za Marekani milioni 21.94. Mahusiano yasio ya moja kwa moja kati IFC na Bridge kupitia Learn Capital yalikuwa yanaendelea wakati wa kuandika ripoti hii.

Mwanzoni mwa uwekezaji wa IFC, lengo kuu la Bridge lilikuwa kuboresha "shule za jamii," zinazojulikana kama “academies,” ambazo ilimiliki na kuendesha. Wakati huo, IFC ilikadiria kuwa, kupitia kuongeza mtaji na ukuaji utakaofuata, Bridge ingeanzisha shule zipatazo 2,100 ambazo zingehudumia takriban watoto milioni 1 kufikia mwaka wa fedha wa 2020—ongezeko la asilimia 1,500 la wanafunzi.

Kuanzia mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2016, Bridge ilishuhudia ukuaji mkubwa wa shule, kutoka shule 211 za jamii zilizohudumia watoto 57,000 wenye umri wa miaka kati ya 3 na 14 hadi shule 520 za jamii zilizohudumia takriban wanafunzi 87,600. Bridge pia ilipanuka na kuendesha shule za jamii kwa ubia na mashirika yasiyo ya serikali nchini India, Nigeria, na Uganda, pamoja na ubia wa NGO nchini Kenya.[60]

### 1.2.1. Kujiondoa kwa IFC na uamuzi wa kusitisha uwekezaji katika shule za kibinafsi za K–12 zinazolipisha karo

Tarehe 22 mwezi Machi mwaka wa 2020, Rais wa Benki ya Dunia (WBG) alimwandikia Katibu wa Hazina wa Marekani akisema kwamba IFC itasitisha uwekezaji wa moja kwa moja katika shule za kibinafsi za K–12. Pia alijitolea kuanzisha mchakato wa mashauriano na Kikundi cha Tathmini Kinachojitegemea kutathmini uwekezaji wa IFC katika sekta hii ndogo ili kubaini kama kunaweza kuwa na hali zozote za kipekee ambazo uwekezaji wa

[54] IFC, 2013, SII. Inapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32171/bridge-international-academies.
[55] Ibid.
[56] Ibid.
[57] IEG 2022, Tathmini ya Uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa katika Shule Binafsi za K–12. Inapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/sites/default/files/Data/Evaluation/files/IFCSupport_K12PrivateEducation_GS_and_MC.pdf.
[58] IFC, 2013, ESRS. Inapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.
[59] IFC, April 2014, Muhtasari wa Taarifa za Uwekezaji (SII) za Mradi #32429. Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32429/education-innovation-fund.
[60] IFC, Mei 31, 2018, Ripoti za Kila Mwaka za Ufuatiliaji wa Mazingira na Jamii (AMR) (2016.3.1-2017.12.31). Ukurasa wa Wavuti wa Bridge, Programu. Unapatikana hapa: https://www.bridgeinternationalacademies.com/.

aina hii unaweza kutokea katika siku zijazo.[61] Miaka miwili baadaye, Machi mwaka wa 2022, IFC ilikomesha uwekezaji wake katika kampuni mama ya Bridge, NewGlobe Schools.[62]

Mwezi Juni mwaka wa 2022, Kikundi Kinachojitegemea cha Kutathmini Benki ya Dunia (IEG), kilichapisha tathmini yake ya Uwekezaji wa IFC katika Shule Binafsi za K–12, na kushauri kutoanza tena kwa uwekezaji wa aina hii. Tathmini iliona vipengele kadhaa vya mfumo wa biashara uliopo wa IFC kuwa haufai kwa uwekezaji katika elimu ya binafsi ya K–12 (ikijumuisha wanafunzi wa kipato cha chini). Ilifikia uamuzi kwamba "IFC italazimika kubadilisha mfumo wake wa biashara ili kuwa na ufikiaji sawa [wa elimu], kulenga kufikia wanafunzi wa kipato cha chini na maskini, kuboresha elimu, na kupelekea manufaa ya kutosha kutokana na uwekezaji.[63] Ili kuanza tena uwekezaji kama huo, tathmini ilipendekeza mabadiliko kadhaa kwa mfumo wa biashara wa IFC.[64] Wasimamizi wa IFC kwa kuzingatia tathmini walikubaliana na maoni na mapendekezo ya IEG na wakasema kuwa IFC haitarajii kurejesha uwekezaji wa aina hii "katika siku za usoni."[65]

## 1.3. Chanzo cha Uchunguzi wa CAO wa Bridge-04

### 1.3.1. Malalamishi, tathmini na uchunguzi wa Bridge-01

Katika mwezi wa Aprili mwaka wa 2018, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa East Africa Centre for Human Rights (EachRights), NGO nchini Kenya, kwa niaba ya wazazi na walimu wa sasa na wa zamani ("walalamishi wa Bridge-01") kuhusu uwekezaji wa IFC kwa Bridge nchini Kenya (kesi ya Bridge-01). Malalamishi hayo yaliibua masuala kuhusu kuridhia kwa Bridge kwa sheria za kimataifa na za Kenya, matakwa ya mtaala wa kitaifa wa Kenya, na madai ya matumizi ya walimu wasiohitimu. Yalidai kuwa Bridge ilikuwa inakiuka Viwango vya Utendakazi vya IFC (PS) kuhusiana na hatari kwa mazingira na jamii (PS1); ajira na mazingira ya kazi (PS2); na masuala ya afya, usalama na usalama wa jamii (PS4), ikijumuisha ujenzi na usalama wa majengo, usafi wa shule na masuala ya usalama wa watoto. Walalamishi wa Bridge-01 wameomba utambulisho wao usitolewe kwa umma. Tathmini ya CAO iliofuata ilifikia uamuzi kuwa kulikuwa na masuala ya kutisha kuhusu matokeo ya E&S ya uwekezaji wa IFC kwa Bridge na uwezekano wa kutoridhia Viwango vya Utendaji 1, 2, na 4.[66] Kwa hivyo, CAO ilianzishaa uchunguzi wa ridhaa Oktoba mwaka wa 2019.[67]

### Makamu wa Rais wa CAO aanzisha tathmini ya ridhaa ya Bridge-04

Kama sehemu ya uchunguzi wa Bridge-01, wafanyakazi wa CAO walisafiri hadi nchini Kenya Februari mwaka wa 2020. Kikosi cha uchunguzi kilizungumza na walalamishi, wanajamii, wawakilishi wa wateja, na mamlaka za

---

[61]WBG, Machi 20, 2020, Barua kutoka kwa Rais wa Benki ya Dunia (WBG) kwa Katibu wa Hazina ya Marekani. Makala yaliyohaririwa yanapatikana hapa: https://democrats-financialservices.house.gov/uploadedfiles/malpass_ltr_mnuchin_3202020.pdf.

[62] IFC, April 2014, Muhtasari wa Taarifa za Uwekezaji (SII) za Mradi #32429. Unapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/SII/32429/education-innovation-fund.

[63] IEG, Juni 2022, Tathmini ya Uwekezaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa katika Shule Binafsi za K–12. Inapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/sites/default/files/Data/Evaluation/files/IFCSupport_K12PrivateEducation_GS_and_MC.pdf.

[64] Ibid. Mapendekezo yanajumuisha:

- Kushirikisha washikadau wengi wanaoweza kuathiriwa na uwekezaji wa IFC katika mfumo wa elimu
- Kushughulikia kwa uwazi upatikanaji na ushirikishwaji wa elimu pasipo na upendeleo pamoja na ubora wa elimu
- Kuboresha ufuatiliaji na usimamizi wa mradi ili kutathmini vipengele zaidi mbali na utendakazi wa biashara, ikiwa ni pamoja na vile vinavyohusiana na upatikanaji na ubora wa elimu, na athari chanya na hasi zinazoweza kutokea katika shule zingine na mifumo ya elimu ya eneo husika.
- Kwa kuzingatia mwafaka kati ya mafanikio ya matokeo ya elimu (ikijumisha ufikiaji, usawa, na ubora) na uendelevu wa kifedha wa uwekezaji wa IFC katika sekta binafsi ya elimu ya K-12.

[65] Ibid.; na IFC, 2022, Ushughulikiaji wa Wasimamizi wa Ripoti ya IEG. Unapatikana hapa: https://ieg.worldbankgroup.org/evaluations/evaluation-international-finance-corporation-investments-K–12-private-schools-7.

[66] CAO, Octoba 21, 2019, Ripoti ya Tathmini ya Ridhaa ya Bridge 01, uk. 2. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/CAOAppraisalReport_BridgeInternationalAcademies_English.pdf.

[67] Ibid.

maeneo husika. Katika mazungumzo hayo, wanajamii waliifahamisha CAO kuhusu madai yanayohusu matukio mengi ya unyanyasaji wa watoto kingono (CSA) katika shule za Bridge uliofanywa na walimu wawili wa Bridge yanayohusisha angalau waathirika 15. Ili kukabiliana na hali mbaya ya matukio haya, CAO ilitafuta taarifa kutoka kwa uongozi wa Bridge kuhusu mifumo ya kampuni ya kulinda na kutunza watoto na jinsi ilivyoshughulikia matukio ya aina hii hapo zamani. CAO pia iliwafahamisha wafanyakazi na wasimamizi wa IFC kuhusu hali hiyo. Mwezi wa Septemba mwaka wa 2020, Makamu wa Rais wa CAO (VP) alitoa ombi kwa CAO kufanya tathmini tofauti ya ridhaa kuhsu jinsi IFC ilivyokagua na kusimamia hatari za E&S na athari zinazoweza kutokea kutokana na shughuli za Bridge zinazohusiana na CSA.

**Muhtasari wa tathmini ya ridhaa ya Bridge-04**

CAO ilikamilisha tathmini yake ya ridhaa ya Bridge-04 mwezi wa Desemba mwaka wa 2020 na kuchapisha Ripoti ya Tathmini Januari mwaka wa 2021.[68] Kama ilivyoelezwa katika ripoti iliyo wazi kwa umma, upitiaji wa awali wa CAO wa stakabadhi za mradi wa IFC uliibua maswali kuhusu utoshelevu wa utafiti wa IFC wa kabla ya uwekezaji na usimamizi wa mteja kwa kuzingatia mahitaji yake ya E&S. Hasa, maswali haya yalihusiana na kama iwapo utafiti wa IFC wa kabla ya mradi na usimamizi wa IFC wa mradi ulizingatia ipasavyo matakwa ya Viwango vya Utendakazi vya IFC vya 1 na 4, sheria ya kitaifa ya Kenya, na mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (GIIP) kama mambo muhimu kwa hatari za kulinda na kutunza watoto.

CAO ilikubali kuwa "kuna kiwango kikubwa cha mambo ya kusikitisha kuhusiana na matokeo ya Kimazingira na Kijamii (E&S) ya uwekezaji wa IFC kwa Bridge kwa kuzingatia: (a) madai maalum ya unyanyasaji wa watoto kingono yaliyotolewa wakati wa uchunguzi wa Bridge-01; na (b) uwezo mkubwa wa hatari za Kimazingira na Kijamii (E&S) kutokea shuleni kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi na uwezekano kwao kuwa hatarini zaidi." Kwa hivyo, CAO iliamua kwamba uchunguzi wa ridhaa kwa masuala yaliyoibuliwa kupitia ombi la Makamu wa Rais wa CAO ulikuwa na mashiko.

Ili kufanya uamuzi huu, CAO ilizingatia "ukubwa wa hatari na athari zilizojitokeza, kiwango [kikubwa] cha biashara ya mteja kote duniani, umri [wachanga] wa watoto wanaosomea shule za Bridge, na uwezo wa kuwa hatarini zaidi kwa watoto na familia ambazo ndizo soko linalolengwa na shule za Bridge."[69]

**Uzinduzi wa uchunguzi wa ridhaa wa Bridge-04**

Kwa hivyo, CAO ilizindua uchunguzi huu wa ridhaa mwezi wa Januari mwaka wa 2021 unaohusu usimamizi wa IFC wa masuala ya kulinda na kutunza watoto, kwa kuzingatia hasa hatari na athari za CSA katika shule za Bridge nchini Kenya. Hatari na athari hizi za CSA ziko katika mawanda ya unyanyasaji wa kijinsia (GBV)[70] dhidi ya watoto.[71] [72]

---

[68] CAO, Desemba 23, 2020, Tathmini ya Ridhaa ya Bridge International Academies-04. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/CAOAppraisalReport-BIA-04-Dec23.pdf.


[69] Ibid, uk. 16.


[70] **Unyanyasaji wa kijinsia** ni unyanyasaji ambao husababisha, au unaoweza kusababisha, madhara au mateso kwa mwili, kingono, au kisaikolojia, dhidi ya mtu kutokana na ubaguzi wa kijinsia, matarajio ya wajibu wa jinsia, na/au dhana potofu za kijinsia, au kutokana na hali inayotofautiana ya mamlaka inayohusiana na jinsia.

[71] Angalia, kwa mfano, UNICEF, "Unyanyasaji wa Kijinsia dhidi ya Watoto," (inaelezea unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto kama aina ya "unyanyasaji wa kijinsia" na kubaini kuwa wavulana na wasichana hukabiliwa na unyanyasaji wa kingono). Inapatikana hapa: https://www.unicef.org/protection/sexual-violence-against-children.

[72] CAO inatambua kwamba madai ya unyanyasaji wa watoto kingono yaliyotajwa katika ripoti hii yanaweza kuchukuliwa kama uhalifu chini ya sheria ya Kenya, *lakini inasisitiza kwamba ripoti hii haijampata mtuhumiwa kuwa mhalifu wala kumtaka kulipia.* Mchakato wa kuridhia wa CAO hauhusiki na ushahidi, sio wa kimahakama, na "haujaundwa wala kukusudiwa kutumiwa katika kesi mahakamani au kutoa hukumu au kwa makusudi ya kuhusisha uhalifu kisheria au kuwajibikia hali." Sera ya CAO katika aya ya 9 na 117. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf. Kwa kuongezea, CAO inabainisha kuwa kwa sababu uchunguzi wa kitengo cha ridhaa sio michakato ya kimahakama, viwango vya ushahidi vinavyohitajika ili kuwa ushahidi wa kutosha kuunga mkono matokeo ya uchunguzi wa CAO havihusiani na mahitaji ya kumuhukumu mhalifu wala mahitaji ya kotoa ushahidi mahakamani.

## 1.4. Ratiba ya Matukio Muhimu[73]






[73] Vyanzo hivi vinahusiana na ratiba ya matukio hapo juu. Benki ya Dunia, April 2015, Muhtasari wa Sekta ya Elimu kuhusu Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana. Unapatikana hapa: https://openknowledge.worldbank.org/server/api/core/bitstreams/7a81b7cb-8ba5-5c96-9a80-9f32821f170e/content.WBG, Julai 31, 2017, Kushirikiana Kuzuia Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono Unapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/482251502095751999/pdf/117972-WP-PUBLIC-recommendations.pdf. Toleo la Habari la Benki ya Dunia, Oktoba 2016, Benki ya Dunia Yazindua Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia. Linapatikana hapa: https://www.worldbank.org/en/news/press-release/2016/10/13/world-bank-launches-global-task-force-to-tackle-gender-based-violence. Tazama pia, Benki ya Dunia, Septemba 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi Inaayohusisha Kazi Kuu za Kiraia. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf.

## 1.5. Ufafanuzi wa dhana

Ripoti hii inatumia istilahi ya/za *tukio (matukio)* kama tukio kuhusiana na CSA, na *muathirika/waathirika* kurejelea watoto walliodhulumiwa kupitia CSA. Kwa kuongezea, CAO inatumia istilahi zifuatazo katika ripoti hii. Ufafanuzi huu umechukuliwa kutoka kwa Maelezo ya Matendo Mazuri ya Benki ya Dunia ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji wa Miradi inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia (2018), *Zana za UNICEF za Ulinzi wa watoto za Mashirika ya Biashara* (2018), UNESCO, *Mwongozo wa Kimataifa wa Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Unyanyasaji wa Kijinsia Shuleni* (2016), na Kikundi Kazi cha Mashirika Mbalimbali kuhusu Kudhulumiwa Kingono kwa Watoto, Miongozo ya *Istilahi za Ulinzi wa Watoto dhidi ya Kudhulumiwa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono.*[74]

**Mtoto.**[75] Mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 18, bila kujali iwapo umri wa watu wengi katika taifa ni wa chini.

**Unyanyasaji wa mtoto.**[76] Aina zote za dhuluma kwa mwili na/au hisia, unyanyasaji wa kingono, kutelekezwa, hatua za kutelekezwa, dhulima za biashiara au zinginezo zinazofanyiwa mtoto zinazopelekea kudhuriwa au uwezekano wa kudhuriwa kwa afya ya mtoto, maisha yake, kukua kwake au utu wake.

**Unyanyasaji wa watoto kingono (CSA).**[77] Kushiriki kwa mtoto katika shughuli za kingono-ikiwa ni pamoja na "unyanyasaji bila kuguswa" kama vile unyanyasaji wa kingono kwa mtoto - ambao mtoto hauelewi kikamilifu, hawezi kutoa idhini kwa kuelewa, au mtoto hajakua vya kutosha na kwa hivyo hawezi kutoa idhini, au kitu kinachokiuka sheria au miiko katika jamii. Unyanyasaji wa watoto kingono unathibitishwa na shughuli ya aina hii kati ya mtoto na mtu mzima au mtoto mwingine ambaye kwa kuzingatia umri au ukuaji ana uwezo wa kuwajibika, kuaminiwa au mamlaka, shughuli hiyo ikikusudiwa kutimiza au kukidhi mahitaji ya mtu mwingine.

**Ulinzi wa watoto.**[78] Ulinzi wa watoto unarejelea hatua zote ambazo kampuni huchukua ili kuwaweka watoto wote wanajumuika nayo salama, ikijumuisha hatua zinazochukuliwa ili kuhakikisha watoto hawadhuruwi kwa kujumuika moja kwa moja au kwa njia isio moja kwa moja na kampuni. Ulinzi wa watoto unajumuisha uzuiaji wa unyanyasaji wa mwili, wa kingono na kihisia, pamoja na kutelekezwa na kudhulumiwa kwa watoto na wafanyakazi na watu wengine ambao kampuni inawajibikia, ikiwa ni pamoja na wakandarasi, washirika wa biashara, wageni wa kampuni na watu wanaofanya kazi bila malipo.

**Utunzaji wa watoto**[79] Utunzaji wa watoto ni sehemu muhimu ya ulinzi, na unarejelea hatua ambazo kampuni huchukua kushughulikia wasiwasi wa kipekee kwamba mtoto fulani ana uwezekano mkubwa wa kudhuriwa

[74] UNICEF, Mei 2018, *Zana za Ulinzi wa watoto za Mashirika ya Biashara,* 2018. Zinapatikana hapa: https://www.unicef.ch/de/media/1049/download; na Susanna Greijer na Jaap Doek, 2016 *Miongozo ya Istilahi za Ulinzi wa Watoto dhidi ya Kudhulumiwa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono (Uliopishwa na* Kikundi Kazi cha Mashirika Mbalimbali kuhusu Kudhulumiwa kwa Watoto Kingono *katika Luxembourg, Januari 28, 2016).* Zinapatikana hapa: https://ecpat.org/wp-content/uploads/2021/05/Terminology-guidelines-396922-EN-1.pdf.
[75] UNICEF, Mei 2018, *Zana za Ulinzi wa watoto za Mashirika ya Biashara*. Zinapatikana hapa: https://www.unicef.org/thailand/media/2601/file/Child%20Safeguarding%20Toolkit%20for%20Business.pdf.
[76] Ibid.
[77] Susanna Greijer na Jaap Doek, 2016 Miongozo ya Istilahi za Ulinzi wa Watoto dhidi ya Kudhulumiwa Kingono na Unyanyasaji wa Kingono, uk. 19. Ufafanuzi wa Mwongozo huu wa "unyanyasaji wa watoto kingono" ulitolewa kwa mara ya kwanza na WHO katika *Ripoti yake ya Ushauriano kuhusu Uzuiaji wa Unyanyasaji Wa Watoto* (WHO, Geneva, Machi 29-31, 1999). Unapatikana hapa: https://ecpat.org/wp-content/uploads/2021/05/Terminology-guidelines-396922-EN-1.pdf, and here: https://apps.who.int/iris/handle/10665/65900.
[78] UNICEF, Mei 2018, *Zana za Ulinzi wa watoto za Mashirika ya Biashara.* Zinapatikana hapa: https://www.unicef.org/thailand/media/2601/file/Child%20Safeguarding%20Toolkit%20for%20Business.pdf.
[79] UNICEF, Mei 2018, *Zana za Ulinzi wa watoto za Mashirika ya Biashara.* Zinapatikana hapa: https://www.unicef.org/thailand/media/2601/file/Child%20Safeguarding%20Toolkit%20for%20Business.pdf.

kutokana na yeye kujumuika na wahusika katika kampuni, washirika wa biashara, bidhaa au huduma. Utunzaji wa watoto ni muhimu ikiwa kuna wasiwasi kwamba mtoto anapitia unyanyasaji au usalama wake uko hatarini.

**Unyanyasaji wa kijinsia (GBV).**[80] Unyanyasaji wa kijinsia ni istilahi kuu kwa shughuli yoyote ya kudhuru inayotekelezwa bila hiari na inayozingatia tofauti zinazotolewa katika jamii (yaani, jinsia) kati ya wanawake na wanaume. Inajumuisha vitendo kama vile kudhulumu mtu mwili, kingono, akili au mateso; vitisho vya aina hii; kulazimisha; na kunyimwa uhuru kwa njia nyingine yeyote. Matendo haya yanaweza kutokea hadharani au kisiri. Wanawake na wasichana huathiriwa zaidi na GBV kote duniani.

**Ukatili na unyanyasaji wa kingono (SEA).**[81] Ni tendo halisi au jaribio la kutumia vibaya mamlaka, nafasi yako au kuaminiwa na mtu ambaye yuko hatarini kuathiriwa kwa madhumuni ya ngono, ikijumuisha, na wala sio tu, lengo la kunufaika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na kumnyanyasa mtu mwingine kingono. Unyanyasaji wa kingono unafanuliwa zaidi kama "uingiaji halisi au kutishiwa kingono, iwe kwa nguvu au kupitia hali zisizo sawa au kwa kulazimisha." Wanawake, wasichana, wavulana na wanaume wanaweza kupitia SEA. Katika muktadha wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, wanaonufaika na mradi au wanajamii ambako mradi unatekelezwa wanaweza kupitia SEA. **Taarifa kwa msomaji:** Ripoti hii haitumii neno SEA *isipokuwa* tu wakati wa kutaja stakabadhi fulani za IFC ambazo zimetumia neno hilo wazi.

Kwa kuongezea, CAO inabaini kuwa unyanyasaji wa watoto kingono uko chini ya unyanyasaji wa kijinsia (GBV) dhidi ya watoto. Huku unyanyasaji wa kijinsia hujadiliwa mara nyingi kuhusiana na athari zake kwa wanawake na wasichana, unaweza na huwa unaathiri wanawake na wanaume, wasichana, wavulana, pamoja na watu wa jinsia mbalimbali. Kama inavyoelezwa na UNICEF:

> "Utamaduni katika jamii ulio na masharti kuhusu jinsia na utambulisho wa jinsia pia huchangia katika ukatili na ubaguzi dhidi ya wavulana, wanaume na watu binafsi walio na utambulisho mbalimbali wa kijinsia, wanavyoelezea jinsia zao, na sifa kuhusu jinsia, ikiwa ni pamoja na wasagaji, mashoga, wanaovutiwa na jinsia zaidi ya moja, waliobadili jinsia, jinsia isiyokuwa ya kawaida au jinsia isiyoeleweka, na watoto na vijana walio na jinsia isiyojulikana (LGBTQI+). Kutokana na hayo, watafiti na mikataba ya kimataifa wametoa wito wa juhudi za kuzuia na kushughulikia ukatili kwa kutumia mbinu inayoleta mabadiliko ya kijinsia, kumaanisha mbinu inayoshughulikia sababu za kukosekana kwa usawa wa kijinsia na kufanya kazi kubadilisha majukumu hatari ya kijinsia, mazoea, na ukosefu wa usawa."[82]

## 1.6. Mbinu Iliyotumiwa na CAO Kufanya uchunguzi wa ridhaa wa Bridge-04

Madhumuni ya kitengo cha ridhaa cha CAO ni kutathmini kuridhia kwa IFC/MIGA kwa Sera za Kimazingira na Kijamii (E&S), kutathmini madhara yoyote yanayohusiana,[83] na kupendekeza hatua za kukabiliana na hali hii inapowezekana. Kwa mujibu wa Sera ya Mfumo Huru wa Uwajibikaji wa IFC/MIGA (Sera ya CAO), kuanzia tarehe 1 Julai mwaka wa 2021, ripoti hii inawasilisha matokeo ya uchunguzi kwa kuzingatia kuridhia, kutoridhia

[80] WBG, Septemba 28, 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi Inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf.

[81] WBG, Septemba 28, 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi Inaayohusisha Kazi Kuu za Kiraia. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf.

[82] UNICEF, Aprili 2020, Vipengele vya Kijinsia vya Ukatili Dhidi ya Watoto na Vijana (Karatasi ya Mikakati), uk.2. Vinapatikana hapa: https://www.unicef.org/media/92376/file/Child-Protection-Gender-Dimensions-of-VACAG-2021.pdf.

[83] Madhara yanafafanuliwa katika Sera ya CAO kama "athari yoyote mbaya ya kimazingira na kijamii kwa watu au mazingira inayotokana moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na Mradi au Mradi Ndogo. Madhara yanaweza kuwa halisi au yanayoweza kutokea katika siku zijazo" (uk. iv). Yanapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf.

kwa IFC, na madhara yanayohusiana ya unyanyasaji wa watoto kingono. Pia inajumuisha maamuzi ya CAO kuhusu sababu msingi za kutoridhia zilizobainishwa wakati wa uchunguzi na mapendekezo kwa IFC kuzingatia wakati wa kuandaa Mpango Kazi wa Utekelezaji ili kushughulikia madhara ya mradi kutoridhia na madhara yanayohusiana nao. Zaidi ya hayo, ripoti hii inajumuisha hatua zinazohitajika ili kuzuia kutoridhia katika siku zijazo, katika hali inayohusiana na hii.[84]

Kama ilivyobainishwa kulingana na marejeleo yaliyochapishwa Oktoba 21, 2021,[85] uchunguzi wa Bridge-04 wa uwekezaji wa IFC kwa Bridge International Academies unahusu masuala ya kulinda na kutunza watoto, ukizangatia hasa hatari za CSA katika shule za Bridge nchini Kenya. Hata hivyo, sera na taratibu nyingi za ulinzi wa watoto za Bridge zilizopitiwa ni za kimataifa, na mapendekezo kadhaa ya CAO ni mwafaka katika uwekezaji mbalimbali wa IFC unaoathiri watoto kote duniani.

Uchunguzi unatathmini kama utafiti wa IFC wa kabla ya kuwekeza na usimamizi wa mifumo ya Bridge na hatua za kuzuia na kushughulikia CSA ziliendana na mahitaji yafuatayo:

- Kiwango cha kwanza cha Utendakazi: Tathmini na Ushughulikiaji wa Hatari na Athari kwa Mazingira na Jamii
- Kiwango cha nne cha Utendakazi: Afya na Usalama wa Jamii,
- Sheria za kitaifa za Kenya zinazohusiana na utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto
- Mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa[86] katika nyanja ya elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini.

Kama ilivyothibitishwa na sera ya CAO, uchunguzi huu unaonyesha kuridhia au kutoridhia kwa kuzingatia taarifa zilizokuwepo wakati maamuzi yalipofanywa; haipelekei matokeo na uamuzi kwa nia ingine yoyote.[87] Ingawa madhumuni ya uchunguzi huu ni kutathmini ridhaa ya IFC kwa E&S, CAO inazingatia utendakazi wa Bridge wa E&S kama inavyohitajika ili kutathmini umakini na usimamizi wa IFC wa mradi na kupata matokeo kuhusu madhara na iwapo madhara yoyote yanahusiana na kutoridhia kwa IFC kwa sera za E&S.[88]

Katika kufanya uchunguzi huu, wafanyakazi wa CAO walifanya kazi na wataalam wa utunzaji na ulinzi wa watoto na walifanya shughuli zifuatazo:

- Walifanya mahojiano na washikadau walijitolea na watu binafsi wanaohusishwa moja kwa moja na uwekezaji huu na pia mashirika ya uraia nchini Kenya yenye ujuzi wa utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto.
- Walifanya uhakiki wa stakabadhi za mradi huu zilizotolewa na IFC na Bridge

[84] Sera ya CAO, Juni 2021, aya ya 120c. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf.
[85] CAO, Oktoba 21, 2021, Masharti ya Uchunguzi wa Ridhaa wa Bridge-04. Yanapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/downloads/Bridge-04%20ToR%20for%20Compliance%20Investigation%20FINAL.pdf.
[86] Viwango vya Utendakazi vya IFC vinafafanua mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa "kama zoezi la maarifa ya kitaalamu, bidii, busara, na uwezo wa kuelewa unaoweza kutarajiwa kutoka kwa wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wanaojishughulisha na aina moja ya shughuli chini ya hali sawa au mazingira sawa duniani au kikanda." PS1, aya ya 7, tanbihi 10. Vinapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.
[87] Sera ya CAO, Juni 2021, aya ya 116. Inapatikana hapa: https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf.
[88] Ibid, aya ya 114.

- Walipitia ripoti zinazopatikana kwa umma kuhusu kuenea kwa CSA nchini Kenya na hasa katika shule za Bridge
- Walipitia sheria na sera za Kenya pamoja na mikataba ya kimataifa inayoonekana ingeweza kutekelezeka chini ya sheria za Kenya na malengo na athari za utunzaji na ulinzi wa watoto.
- Stakabadhi zilizokaguliwa zinazounda GIIP zilizochapishwa kati ya mwaka wa 2013 na mwaka wa 2022 kuhusu utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto katika elimu binafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini.

CAO haikufanya uchunguzi huu nyanjani, kutokana kwa kiasi fulani kuwa ulikuwa mwaka wa pili wa janga la korona (COVID-19). Hata hivyo, wafanyakazi wa CAO walioshughulikia kesi hii walipata taarifa muhimu zilizokusanywa na wafanyakazi wenzao nyanjani wakati walipokuwa nyanjani kwa Bridge-01 mwezi Februari mwaka wa 2020. Taarifa hii ilijumuisha madai ya kina yaliyosababisha ombi la Makamu wa Rais wa CAO kuitisha tathmini ya ridhaa ya CSA katika shule ya Bridge nchini Kenya. Aidha, CAO ilimshirikisha mshauri kufanya uchunguzi zaidi wa kupata ukweli nchini Kenya kama sehemu ya uchunguzi.

### 1.6.1. Upatikanaji na Ufichuzi wa Taarifa

Kwa mujibu wa Sera ya CAO, na kwa kuzingatia wajibu wa taasisi za IFC na WBG, katika kutekeleza kazi yake, CAO itatumia dhana inayopendelea ufichuzi wa taarifa za mazingira na jamii, na wakati uo huo, kudumisha, inavyofaa, usiri wa habari nyeti za kibiashara (aya ya 27).

CAO inahitajika kuridhia Sera za Upatikanaji wa Taarifa (AIPs) za IFC na MIGA. Kwa kuzingatia haya, CAO inaweza kufichua habari iliyokusanywa wakati wa shughuli zake, kulingana na AIPs na masharti mengine yanayotumika. Pale ambapo IFC/MIGA imeibua maswala ya usiri ambayo hayajatatuliwa baada ya CAO kupitia na kushughulikia maoni ya IFC/MIGA yanayotokana na mchakato wa uhakiki na maoni halisi, haya yanaweza kutegemea utaratibu wa kuongoza kesi chini ya aya ya 28 ya Sera ya CAO. Hii inabainisha kuwa suala lolote la upatikanaji au ufichuzi wa taarifa linapaswa kujadiliwa kati ya Mkurugenzi Mkuu (DG) wa CAO na Menejimenti kwa lengo la kupata suluhu.

Iwapo suala hilo halitatatuliwa, ikiwa ni pamoja na kama taarifa yoyote ni ya siri na kama na jinsi gani inaweza kufichuliwa au kulindwa, Sera ya CAO inaeleza kwamba "itapelekwa kwa majadiliano kati ya Mshauri Mkuu wa IFC/MIGA (katika nafasi yake ya kitaasisi), Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa CODE, DG wa CAO, na Menejimenti” (aya ya 29).

Kuhusiana na kesi hii, mahitaji ya usiri kati ya IFC na Bridge yalianishwa katika Makubaliano ya Haki za Wawekezaji (IRA) mwaka wa 2013. Katika mwaka wa 2020, IFC na Bridge ziliingia katika makubaliano ya ziada ya kudumisha usiri. Makubaliano haya ya Barua ya mwaka wa 2020 yanarejelea AIP na makubaliano ya awali kati ya wahusika. Hata hivyo, mbali na IRA inabainisha aina nne maalum za stakabadhi na taarifa ambazo zinafaa kushughulikiwa kama siri na kwa kuzingatia wajibu wa usiri wa IRA. Ingawa yalijadiliwa na kutiwa saini bila ushirikishwaji au idhini ya CAO, na kabla ya DG wa sasa kuteuliwa, Makubaliano haya ya Barua yanaeleza wazi kwamba kila mojawapo ya masharti haya yanatumika kwa CAO.

Muda wa Makubaliano haya ya Barua ya mwaka wa 2020 ulizua mwonekano wa kutaka kusitisha uchunguzi wa CAO na kuibua maswali kuhusu jinsi CAO inavyoweza kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia vifungu vya makubaliano ya usiri kuhusiana na ufichuzi wa uchunguzi wa ridhaa ya Bridge-01 na Bridge-04. CAO ilishirikisha wakili wa kujitegemea kisheria ili kutoa ushauri wa kuelewa: i) athari za makubaliano ya usiri, pamoja na AIP, kuhusu CAO kufichua ripoti; na ii) uwezo wa ufichuzi ili kutimiza wajibu wa CAO wa uwazi na ufichuzi huku ikiheshimu masilahi halali ya kudumisha usiri. Wakili aliripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mkuu wa CAO na

pia alisaidia CAO kuandaa mbinu iliyopendekezwa na nyenzo zinazoiunga mkono kwa majadiliano yaliyofanywa chini ya aya ya 28 na 29 ya Sera ya CAO. Ingawa Makubaliano haya ya Barua ya mwaka wa 2020 hatimaye hayakuzuia uwezo wa CAO kupata taarifa wala kufanya uchunguzi wake jinsi ilivyokusudiwa, yalisababishia CAO ucheleweshaji wa muda na gharama za ziada za kifedha. Kwa mtazamo wa CAO, hali hii ya Makubaliano ya Barua ya mwaka wa 2020 inaibua masuala muhimu ambayo yanahitaji kuzingatiwa iwapo makubaliano yoyote kama haya yatawahi kujadiliwa katika siku zijazo. Yanajumuisha jinsi ya kuzingatia wajibu na viwango vilivyowekwa katika Sera ya CAO, hasa kwa kuwa vinahusiana na uhuru wa CAO, na viwango vyake vya uwazi na ufichuzi, na umuhimu wa kushauriana na CAO kabla ya kuingia makubaliano.

# 2. Viwango, Sera, na Vigezo Vinavyotumiwa kuhusiana na Unyanyasaji wa Watoto Kingono

Sehemu hii inawasilisha sera za IFC za kimazingira na kijamii (E&S), taratibu, na Viwango vya Utendakazi (PSs) kuhusiana na hatari zinazohusiana na unyanyasaji wa watoto kingono (CSA) zinazohusiana na mradi. Kisha inatoa muhtasari wa sheria za kitaifa za Kenya zinazotumika na mazoea mazuri yaliowekwa ya tasnia ya kimataifa (GIIP) zinazohusiana na elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini, ambazo IFC pia ilihitajika kutathmini na kusimamia chini ya Mfumo wa Endelevu. Kwa uchunguzi huu, CAO ilitathmini hatua za IFC dhidi ya mahitaji haya ili kubainisha iwapo IFC iliridhia wajibu wake wa E&S wakati wa utafiti wa kabla ya mradi na usimamizi wake wa Bridge International Academy.

## 2.1. Viwango vya IFC vinavyotumika

Ushirikiano wa IFC na mteja huyu ulianzishwa katika muktadha wa Sera ya IFC ya mwaka wa 2012 kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii ("Sera ya Uendelevu") na Viwango vya Utendakazi vya IFC vya mwaka wa 2012, kwa pamoja vinavyojulikana kama "Mfumo wa Uendelevu.″ Sera na viwango hivi vimeundwa ili kulinda watu na mazingira dhidi ya madhara yanayohusiana na uwekezaji wa IFC.

Mfumo wa Uendelevu haushughulikii tu hatari na athari zinazohusiana na watoto mbali na ajira kwa watoto na watoto kuwa hatarini zaidi kukumbwa na usafirishaji haramu wa binadamu (PS2, aya ya 21 na tanbihi ya 13). Hata hivyo, mahitaji ya jumla ya kutathmini, kupunguza, kukabiliana, na kurekebisha hatari za kijamii na athari za shughuli za biashara chini ya Mfumo wa Uendelevu yanatumika kwa wazi kwa hatari na athari za CSA zinazohusiana na mradi, ikizingatiwa kwamba:

- CSA ni tishio kubwa kwa afya, ulinzi na usalama wa watoto, ikiwa na athari mbaya zaidi kwa maendeleo ya kijamii ya watoto na jamii, familia zao na jamii.[89]
- Haki za binadamu zilizopo za watoto zinawapa haki ya uhuru dhidi ya aina zote za unyanyasaji na ubaguzi, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) na aina nyingine za ubaguzi wa kijinsia.[90]

Chini ya PS1, watoto ni kikundi kidogo cha vikundi vinavyopitia ugumu na vilivyo hatarini ambavyo wateja wa IFC ni sharti wavitambue na kisha kudhibiti hatari ambazo zinaweza kuwaathiri zaidi (aya ya 12, tazama pia sehemu ya 2.1.1. hapo chini). Zaidi ya hayo, Benki ya Dunia ilishughulikia kwa uwazi hatari za CSA zinazohusiana na mradi wakati wote wa uwekezaji wa IFC kwa Bridge, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.1. na 1.2. hapo juu. Mfumo wa Uendelevu wa IFC pia unaeleza dhamira yake ya "kuhakikisha kwamba gharama za maendeleo ya kiuchumi hazidhuru zaidi wale ambao ni maskini au walio hatarini zaidi" (Sera ya Uendelevu, aya ya 9). Sera ya Uendelevu na Viwango vya Utendakazi, ambavyo wateja wa IFC wanapaswa kuzingatia, vina

[89] Tazama, UNICEF, 2014 Wazi ila Fiche: Uchambuzi wa Takwimu za Ukatili Dhidi ya Watoto, uk. 62. ("Matukio ya unyanyasaji wa kingono utotoni hudhuru vipengele vyote vya ukuaji: kimwili, kisaikolojia na kijamii."). Unapatikana hapa: https://data.unicef.org/resources/hidden-in-plain-sight-a-statistical-analysis-of-violence-against-children/; na IFC, EBRD, CDC, na Maendeleo ya Jamii Moja kwa Moja, 2020, Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu, katika uk. 1 (inaonyesha kwamba "GBVH ni suala nyeti na la kimfumo katika sekta ya elimu" ambalo hutokea katika mazingira yote ya elimu na lina "athari za kudumu katika ujifunzaji, afya, ustawi na njia ya kupata ajira kwa wanafunzi," pamoja na uwezekano wa athari zinazotofautiana kijinsia kwa wavulana na wasichana). Unapatikana hapa: https://www.ifc.org/en/insights-reports/2020/publications-gpn-addressinggbvh.

[90] Tazama, kwa mfano, Kifungu cha 19 na 34 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (1989), na CEDAW (1981). Vinapatikana hapa: https://www.ohchr.org/sites/default/files/crc.pdf na hapa: https://www.ohchr.org/sites/default/files/cedaw.pdf.

ulinzi mahususi kwa makundi yaliyo hatarini, wakiwemo watoto, wanawake na wasichana.[91] PS1, kwa mfano, inasema kwamba hali ya watu walio katika mazingira magumu au walio hatarini zaidi “huenda ikatokana na rangi ya mtu au kikundi, rangi, jinsia, lugha, dini, maoni ya kisiasa au mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mali, apozaliwa, au hali nyingine. Mteja pia anapaswa kuzingatia mambo kama vile jinsia, umri, kabila, utamaduni, kusoma na kuandika, ugonjwa, ulemavu wa kimwili au kiakili, umaskini au hali mbaya ya kiuchumi, na utegemezi wa malighafi za kipekee.[92]

Sera ya Uendelevu inatambua "wajibu wa shirika la biashara kuheshimu haki za binadamu" na inatambua kwamba wajibu huu "unamaanisha kuepuka kukiuka haki za binadamu za wengine na kushughulikia athari mbaya kwa haki za binadamu ambazo shirika la biashara linaweza kusababisha au kuchangia" (aya ya 12).

Chini ya masharti ya Sera ya Uendelevu, IFC itawekeza katika mradi tu iwapo shughuli inazofadhili "zinatarajiwa kukidhi mahitaji ya Viwango vya Utendakazi ndani ya muda unaofaa" (aya ya 22). IFC hufanya utafiti wa E&S (ESDD) kabla ya uwekezaji  ili kutathmini kama mradi unaonuiwa unaweza kutarajiwa kukidhi mahitaji haya (Sera ya Uendelevu, aya ya 20–28). Utafiti wa kabla ya mradi ni sharti "ulingane na hali, ukubwa, na hatua ya shughuli ya biashara, na kiwango cha hatari kwa mazingira na kwa jamii na/au athari" (aya ya 26). Zaidi ya hayo, ikiwa baada ya idhini ya Bodi kuna mabadiliko makuu katika hali ya hatari ya Kimazingira na Kijamii za mradi, IFC inahitaji kutathmini hali hii na, kwa kuzingatia hatari na mahitaji ya Viwango vya Utendakazi na, kumtaka mteja kurekebisha Mfumo wake wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESMS) ili kuyashughulikia (Sera ya Uendelevu, aya ya 25).

Wakati wote wa uwekezaji, IFC inahitajika kufuatilia mradi mara kwa mara ili kuhakikisha unaridhia masharti katika makubaliano ya uwekezaji na sera na viwango vya IFC vinavyotumika (aya ya 7, 25, na 45). Iwapo mteja atashindwa kuridhia makubaliano katika masharti ya E&S yanayoongoza uwekezaji wa IFC, “IFC itafanya kazi na mteja kumfanya kuridhia kwa kiwango kinachowezekana, na ikiwa mteja atashindwa kuridhia, IFC itatumia masuluhisho mwafaka” (aya ya 45).

Zaidi ya hayo, vipengele mbalimbali vya Viwango vya Utendakazi vya 1 na 4 vinaingiana na hatari na athari za CSA zinazohusiana na mradi na vina umuhimu mahususi kwa uwekezaji wa IFC kwa Bridge. Vimefupishwa hapo chini.

### 2.1.1. Kiwango cha kwanza cha Utendakazi cha IFC:  Tathmini na Ushughulikiaji wa Hatari na Athari kwa Mazingira na Jamii

PS1 inawahitaji wateja kutambua na kutathmini "hatari zote kuu kwa mazingira na kwa jamii na athari zinazoweza kutokea" zinazohusiana na mradi na kuweka "mfumo wa kukabiliana na hali" kutazamia na kuzizuia au ambapo haiwezi kuepukika, kupunguza hatari na athari kwa wafanyikazi, jamii zilizoathiriwa, na kwa mazingira. Pale ambapo athari za mradi zitasalia, wateja wanatakiwa kufidia au kukabiliana na hatari na athari (Malengo na aya ya 14). PS1 inabainisha kuwa kila Kiwango cha Utendakazi cha IFC kina vipengele vya haki za binadamu na kwamba utafiti wa kabla ya mradi kwa kuzingatia viwango huwezesha wateja kushughulikia masuala ya haki za binadamu yanayohusiana na mradi wao.

Kuhusu hatari na athari za CSA, bila kubainisha CSA kwa jina, PS1:

---

[91] Tazama, kwa mfano, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Kijamii, 2012, katika aya ya 9; na IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, aya za 12, 27, 30); PS2 (aya za  2, 21, 22, 27); PS4 (aya za 1 na 9); PS5 (aya za 8 na 19); na PS7. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/sp-english-2012.pdf na hapa; https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

[92] PS1, 2012, aya ya 12, tanbihi 18. Unapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

- Huhitaji mteja wa IFC kutambua, kutathmini na kushughulikia hatari na athari za E&S za mradi. Mipango ya ushughulikiaji wa hatari na athari inapaswa kutoa kipaumbele kwa uepukaji wa hatari na athari. Pale ambapo haiwezekani kuepukika, inanuia kuzipunguza, na, pale ambapo athari zitabakia, wateja lazima walipe/kuzifidia popote inapowezekana kiufundi na kifedha (Malengo, aya ya 5 na 14).
- Huhitaji michakato ya mteja kutambua hatari za Kimazingira na Kijamii (E&S) kurandana na mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (PS1, aya ya 7).
- Huhitaji wateja wa miradi iliyo na vipengele, mambo, nyenzo mahususi, zilizoainishwa zinazoweza kupelekea athari za E&S: (1) kutambua watu binafsi na vikundi ambavyo vinaweza kuathiriwa moja kwa moja na kwa njia tofauti au kwa kiasi kikubwa na mradi kutokana na hali ya mazingira magumu au kuwa hatarini zaidi, na (2) kupendekeza na kutekeleza mikakati mbalimbali ili athari mbaya zisikumbe watu hawa zaidi (aya ya 12). Watoto wamejumuishwa miongoni mwa makundi haya kutokana na umri wao (aya ya 12).[93]
- Kumtaka mteja azingatie sheria na kanuni za kitaifa zinazohusiana na mradi husika, ikiwa ni pamoja na zile zinazotekeleza ahadi za kimataifa (aya ya 6 na 16).

PS1 pia huweka mahitaji muhimu ya mchakato ili kuwasaidia wateja wa IFC kutekeleza hatua zinazohitajika hapo juu. Ni pamoja na:

- Kuanzisha sera ya E&S inayolingana na PS na kuwasilisha sera hiyo kwa wafanyikazi wote (aya ya 6).
- Kutengeneza programu za usimamizi wa E&S zilizo na hatua za kupunguza na kuboresha utendakazi zinazoshughulikia hatari na athari za E&S zilizotambuliwa (aya ya 13).
- Pale ambapo hatari na athari haziwezi kuepukika, kutambua hatua za kupunguza na utendakazi na kuanzisha hatua kama hizi ili kuhakikisha mradi utaendeshwa kwa kufuata sheria na kanuni zinazotumika na kukidhi mahitaji ya PS (aya ya 15).
- Kukuza Mipango ya Utekelezaji ya E&S, ambayo kwa kawaida hukubaliwa na IFC, ambayo inajumuisha matokeo yanayotarajiwa, hatua zilizotengewa muda, makadirio ya rasilimali, na majukumu ya utekelezaji (aya ya 16).
- Kuanzisha, kudumisha, na kuimarisha muundo wa shirika ili kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa E&S (aya ya 17) na kufuatilia na kupima ufanisi wake, kwa kuhusisha wawakilishi wa jamii zilizoathiriwa katika shughuli za ufuatiliaji inapohitajika (aya ya 22).

Zaidi ya hayo, PS1 inawahitaji wateja kuendesha ushirikishwaji wa washikadau kulingana na hatari na athari mbaya za mradi (aya ya 25), ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa muhimu kuhusu hatari na athari zozote zinazoweza kutokea kwa jamii zilizoathiriwa na hatua mwafaka za kuzipunguza (aya ya 29). Wateja ni sharti waanzishe mfumo wa kushughulikia malalamishi kuzingatia hatari na athari za mradi kwa kulenga jamii zilizoathiriwa kama watumiaji msingi (aya ya 35).

[93] Ibid, aya ya 12. Hali ya watu walio katika mazingira magumu au walio hatarini zaidi “huenda ikatokana na rangi ya mtu au kikundi, rangi, jinsia, lugha, dini, maoni ya kisiasa au mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mali, alikozaliwa, au hali nyingine. Mteja pia anapaswa kuzingatia mambo kama vile jinsia, umri, kabila, utamaduni, kusoma na kuandika, ugonjwa, mwili."

**2.1.2. Kiwango cha Nne cha Utendakazi cha IFC: Afya, Usalama na Ulinzi wa Jamii**

PS4 pia inahusiana na uwekezaji wa IFC kwa Bridge na hatari na athari zinazohusiana na CSA kutokana na mpangilio wa mradi katika shule za msingi na sekondari. Kiwango hiki kinahitaji mteja:

- Kuepuka na kupunguza hatari za kawaida na zisizo za kawaida za afya na usalama wa jamii (aya ya 1).
- Kutathmini hatari na athari hizo katika mradi mzima (aya ya 5).
- Kuanzisha hatua zinazohusiana za kuzuia na kudhibiti hali zinazorandana na GIIP na hatua za kukabiliana na hali zinazolingana na hali na ukubwa wa hatari na athari (aya ya 5).

Hatua zitakazochukuliwa na mteja kuridhia PS4 ni sharti zipendelee kuepuka hatari na athari badala ya kuzipunguza (aya ya 5).

## 2.2. Sheria za Kenya zinazotumika katika nyanja ya elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini

Kiwango cha kwanza cha Utendakazi wa IFC kinawahitaji wateja kuanzisha sera ya E&S inayoridhia PS ambayo inawajibisha mradi wao kuridhia sheria zinazotumika, ikiwa ni pamoja na sheria zinazotekeleza ahadi za kimataifa (aya ya 6). Katika hali hii, wakati wa hatua za utafiti wa kabla ya mradi wa IFC (2013) na awamu ya usimamizi wake (2014-2022), sheria husika za Kenya zilijumuisha ulinzi wa kina zaidi dhidi ya unyanyasaji wa watoto kingono na athari kwa wanaokiuka CSA. Sheria hizi zinatumika kwa taasisi za elimu za kibinafsi—kama vile shule za Bridge—na wafanyakazi wake, washauri na watu wanaojitolea.

Masharti muhimu ya sheria na kanuni zilizokuwepo wakati wa uchunguzi wa utafiti wa IFC wa kabla ya kuwekeza katika shughuli za Bridge yamefupishwa hapo chini.[94]

**Sheria iliyokuwa inatumika wakati wa utafiti wa IFC wa kabla ya mradi:**

- Inapinga aina zote za ukatili dhidi ya watoto, inaharamisha unyanyasaji wa watoto kingono, na kutambua haki za watoto za kulindwa dhidi ya ukatili na unyanyasaji.
- Iliweka taratibu ambazo mamlaka za serikali zinapaswa kupokea na kushughulikia ripoti za watoto wanaohitaji kutunzwa au kulindwa
- Inahitaji elimu ya msingi ya kibinafsi na ya umma itolewe bila aina yoyote ya unyanyasaji wa watoto au ubaguzi wa kijinsia
- Inawataka walimu kuripoti ndani ya masaa 24 sababu zozote za msingi za kuamini kwamba mtoto amenyanyaswa kingono kwa mwalimu mkuu, maafisa wa elimu, kamati za usimamizi wa shule, bodi ya magavana, polisi, au shirika lolote linalofanya kazi na masuala ya utunzaji wa watoto, na kwa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC)
- Kuanzisha utaratibu wa walimu wote kusajiliwa ili kufundisha kihalali nchini Kenya, na kuondoa wahalifu wa ngono waliopatikana na hatia kwenye mchakato huu.

[94] Ona sheria zifuatazo za Kenya: Sheria ya Watoto ya mwaka wa 2001, Sheria ya Makosa ya Ngono ya mwaka wa 2006, Katiba ya mwaka wa 2010, Kanuni za Adhabu za mwaka wa 2010, Waraka wa Tume ya Huduma ya Walimu wa 3/2010, Sheria ya Tume ya Huduma ya Walimu ya mwaka wa 2012, na Sheria ya Elimu ya Msingi ya mwaka wa 2013.

- Chini ya Katiba ya Kenya Kifungu cha 2(6)), kinaonyesha kuwa mikataba yote ya kimataifa inaweza kutekelezwa chini ya sheria za nchi, ikijumuisha ifuatayo iliyoidhinishwa na Kenya kabla ya mwaka wa 2010: Mkataba wa Afrika wa Haki na Maslahi ya Watoto (1990); Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto (1989); na Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979). [95]

**Sheria iliyokuwa inatumika wakati wa usimamizi wa IFC:**

Sheria ya Kenya inayotumika kwa elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini ilibadilika zaidi kati ya mwaka wa 2014 na 2021 na:[96]

- Kuzuia walimu ambao hawajasajiliwa na TSC kuajiriwa katika ngazi yoyote ya programu ya shule
- Kuweka masharti ya kina kuhusu mienendo ya walimu ili kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono
- Kuanzisha haki za waathirika wa uhalifu, ikiwa ni pamoja na waathirika wa unyanyasaji wa kingono
- Kuwataka watoa huduma mbadala za elimu ya msingi kusajiliwa na Wizara ya Elimu na kuajiriwa tu kwa walimu waliofuzu pekee.

Sheria hizi zilitoa mfumo thabiti wa kitaifa wa kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na shuleni.

## 2.3. Mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa yanayotumika kwa Masuala Yanayohusiana na CSA katika elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini

GIIP katika eneo hili imekuzwa vizuri na ni ya kina. Mazoea kama haya ni muhimu kwa uchunguzi huu kwa sababu Viwango vya Utendakazi vya IFC vinahitaji mchakato wa utambuzi wa mteja wa hatari na athari (PS1, aya ya 7) na hatua zake za lazima za kuzuia na kudhibiti hali zinazohusiana na afya na usalama wa jamii (PS4 aya ya 5) kwa kurandana na GIIP. Viwango vya Utendakazi vya IFC vinafafanua mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa "kama zoezi la maarifa ya kitaalamu, bidii, busara, na uwezo wa kuelewa unaoweza kutarajiwa kutoka kwa wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wanaojishughulisha na aina moja ya shughuli chini ya hali au mazingira sawa duniani au kikanda."[97]

[95] Mbali na mahitaji haya yanayowabana kisheria, serikali ya Kenya imetoa: Mwongozo wa Viwango vya Usalama kwa Shule nchini Kenya wa mwaka wa 2008 (ulio na maelekezi kuhusu utekelezaji wa usalama shuleni na kutambua na kukabiliana na hatari husika na, ikiwa ni pamoja na atakachofanya mwalimu akifahamu kuhusu dhuluma za kingono na ukatili mwingine). Unapatikana hapa: http://cwsglobal.org/wp-content/uploads/2017/01/CWS-SSZ-Schools-Manual_Kenya.pdf; Sera ya Sekta ya Elimu na Mafunzo kuhusu Jinsia ya mwaka 2015 (inayosema kwamba shule zinapaswa kuweka mazingira salama ya kujifunzia na kuzuia GBV). Inapatikana hapa: https://www.education.go.ke/sites/default/files/2022-05/EDUCATION-and-TRAINING-Sector-Gender-Policy-2015-FINAL-PRINTED-VERSION1.pdf; na Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia na Kushughulikia Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Kenya (2019-2023) (unatoa maelekezi ya kina zaidi ya kuondoa ukatili na unyanyasaji kwa elimu kabisa, na kushauri shule: a) kuimarisha mifumo ya kuripoti, vijisanduku vya kutoa maoni, saraka za rufaa na fomu za rufaa za viwango; b) kuimarisha uwezo wa walimu kuzuia, kutambua na kukabiliana na unyanyasaji wa watoto; na c) kukuzaTaratibu za Utendekazi za Kawaida kuhusu unyanyasaji wa kijinsia Unaohusiana na Shule). Unapatikana hapa: https://www.unicef.org/kenya/media/1526/file/National%20Prevention%20&%20Response%20Plan%20on%20VAC.pdf.

[96] Tazama sheria zifuatazo za Kenya: Sheria ya Kulinda Waathiriwa ya mwaka wa 2014, Kanuni za Maadili ya Kazi za Tume ya Kuwaajiri Walimu za mwaka wa 2015; Miongozo ya Usajili wa Utoaji Mbadala wa Elimu na Mafunzo ya Msingi ya Mwaka wa 2015, kuweka taratibu za utekelezaji wa Sera ya Utoaji Mbadala wa Elimu na Mafunzo ya Msingi; na Waraka wa TSC wa 14/2018, Mwongozo wa Ziada wa Kuimarisha Usalama na Maslahi ya Wanafunzi wote. Unapatikana hapa: 2018_TSC_Circular on Protection of Pupils - Students copy.pdf.

[97] PS1, 2012, aya ya 7, maelezo ya 10. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

Kwa uwekezaji kwa Bridge, GIIP kuhusu utambuzi, uzuiaji na udhibiti wa hatari za CSA katika elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini inatumika. Mazoea mwafaka mazuri wakati wa utafiti wa IFC wa kabla ya mradi na usimamizi wa mradi yamefupishwa hapo chini.

### 2.3.1. GIIP iliyokuwa inatumika wakati wa utafiti wa IFC wa kabla ya mradi

GIIP iliyokuwepo wakati wa utafiti wa IFC wa kabla ya uwekezaji wa IFC kwa Bridge mwaka wa 2013 ingehitaji shule za kibinafsi katika mazingira ya kipato cha chini, kama vile Bridge:[98]

- Kuheshimu haki zote za binadamu zinazotambulika katika ngazi ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na haki za watoto kupata elimu na kuepuka aina zote za unyanyasaji, ukatili na ubaguzi na ukatili wa kijinsia.[99]
- Kutathmini (kwa ushirikiano na watoto na familia zao) sheria zilizopo za kulinda na kutunza watoto ili kutathmini utendakazi wake, kutambua hatari, na kuunda fahirisi ya hatari inayojumuisha unyanyasaji wa kimwili na kingono.
- Kutekeleza utafiti wa kabla ya mradi wa haki za binadamu unaoendelea unaojumuisha unyanyasaji wa watoto kimwili na kingono, kufuatilia na kuwasiliana kuhusu jinsi athari hizi zinavyoshughulikiwa, na kujumuisha mchakato unaozingatia watoto kushughulikia athari yoyote mbaya kwa haki za watoto ambayo shirika la biashara husababisha au kuchangia.
- Kukuza, kuwasiliana na wafanyakazi, na kutekeleza sera ya ulinzi na utunzaji wa watoto isiyoruhusu aina yoyote ya ukatili; kanuni zinazohusiana za maadili na mafunzo kwa wafanyakazi; taratibu za kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono, kudhulumiwa, ukatili na unyanyasaji; na mifumo ya malalamishi, ya rufaa, na ya kuripoti inayotii sheria.
- Kuweka ulinzi na mifumo ya kuwalinda wasichana na wanawake dhidi ya GBV, ikiwa ni pamoja na hatua mahususi za ulinzi kwa wasichana, watoto katika makazi duni mijini, na watoto wa maeneo ya vijijini, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya kuwahamasisha wafanyakazi kuhusu jinsi tofauti za kijinsia zinavyowaweka watoto katika hatari ya kudhuriwa.
- Kumwachisha kazi na kufungua mashitaka dhidi ya mwalimu yeyote aliye na hatia ya unyanyasaji au ukatili dhidi ya mtoto, na kwa hali yoyote walimu wa aina hii wasihamishwe kwenda shule nyingine.
- Kushughulikia matukio ya CSA shuleni kwa kuhakikisha kwamba waathiriwa walioumizwa mwili wanashughulikiwa na kwa kutoa ushauri nasaha na aina nyingine za usaidizi huku usiri wa waathiriwa ukulindwa.
- Kutengeneza mwongozo kuhusu usiri na kutoa habari kuhusu utunzaji wa watoto.

### 2.3.2. GIIP iliyokuwa inatumika wakati wa usimamizi wa IFC wa mradi

GIIP inayotumika kwa elimu ya kibinafsi ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini ilibadilika zaidi kati ya mwaka wa 2014 na 2019—kipindi cha usimamizi kabla ya CAO kwenda nyanjani Februari mwaka wa 2020, hali

---

[98] Tazama ), A/61/299; Mwongozo wa UNICEF kuhusu Mazingira Bora Shuleni kwa Watoto (2009); Kanuni za Umoja wa Mataifa Zinazoongoza Mashirika ya Biashara na Haki za Kibinadamu (2011); Viwango vya Kuweka Watoto Salama vya Ulinzi wa Watoto (2011); na UNICEF, Global Compact, Save the Children - Haki za Watoto na Kanuni za Kufanya Biashara (2012).

[99] Haki hizi zilikuwa zimeanzishwa na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto (ACRWC), Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto (UNCRC), na Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW).

iliyopelekea uchunguzi huu. Vyanzo vya GIIP vilivyotolewa katika kipindi hiki vilihitaji shule za kibinafsi katika mazingira ya kipato cha chini:[100]

- Kuandaa, kutekeleza, na kuwasiliana na umma kuhusu sera ya kulinda na kutunza watoto na taratibu zinazohusiana zinazoshughulikia GBV inayohusiana na shule.
- Kuhakikisha kwamba michakato inayoendelea ya shirika la biashara ya haki za binadamu kutokana na utafiti wa kabla ya mradi inajumuisha tathmini kuhusu jinsia, hatua za kuleta mabadiliko kuhusu jinsia na masuluhisho ya mabadiliko yanayozingatia jinsia.[101]
- Kuajiri walimu waiohitimu, wakiwemo walimu wa kike
- Kutoa ripoti ya uchunguzi kuhusu ukiukaji wa maadili kuhusiana na GBV inayohusiana na shule
- Kuhakikisha kwamba matukio yote ya ukatili dhidi ya wasichana yanaripotiwa na kurekodiwa
- Kuangalia rekodi za uhalifu za wanaomba kazi shuleni kabla ya kuajiriwa.

Wakati uo huo, mwongozo mpya wa GIIP mahususi kwa miradi inayofadhiliwa na taasisi za kimataifa za fedha ya maendeleo ulitolewa, ukijumuisha Kundi la Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Marekani.[102] Mwongozo huu ulihitaji wafanyakazi:

- Kuhakikisha kwamba hatua zinazohusiana na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana zinazuia unyanyasaji tena, na kuzingatia uwezekano wa kutokea tena kwa matukio ya ukatili na unyanyasaji wa watoto.
- Kuzingatia mahali na jinsi shule zinavyojengwa ili kuwezesha usalama wa wanafunzi, ikiwa ni pamoja na kujumuisha usalama wa mwili wa wasichana katika muundo wa miundomsingi wa shule na kuhakikisha kuna mwanga wa kutosha, kuonekana sana ndani na nje ya vyumba shuleni, na vifaa mbalimbali vya usafi wa mazingira.
- Kutoa mafunzo kwa walimu na wafanyakazi wote wa shule ili kuwajengea uwezo wa kukuza kanuni za usawa wa kijinsia na kutambua na kuzuia unyanyasaji wa kingono, ikijumuisha kuwashirikisha wazazi na jamii kwa ujumla.

[100] Tazama: Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu kuhusu Ukatili dhidi ya Watoto, Ripoti kutoka kwa mashauriano ya kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto shuleni (2014); Viwango vya Kuweka Watoto Salama vya Ulinzi Wa Watoto (2014); Mwongozo wa Kimataifa wa UN Women na UNESCO wa Kushughulikia GBV inayohusiana na Shule (2016); Pendekezo la Jumla la 35 la Kamati ya CEDAW kuhusu Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake (2017); Pendekezo la Jumla la 36 la Kamati ya CEDAW kuhusu Haki ya Wasichana na Wanawake Kupata Elimu (2017); Zana za UNICEF za Ulinzi wa watoto kwa Mashirika ya Biashara (2018); na Viwango vya Kuweka Watoto Salama vya Ulinzi Wa Watoto (2019).

[101] Kikundi kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu mashirika ya biashara na haki za binadamu kimefafanua "mabadiliko na hatua zinazozingatia jinsia" kama zile "zinazoweza kuleta mabadiliko kwa kanuni za mfumo dume na mahusiano yasiyo na usawa ya madaraka ambayo yanapelekea ubaguzi, unyanyasaji wa kijinsia na maoni potovu kuhusu jinsia." Tazama Vipengele vya Jinsia vya Kanuni Elekezi kwa Mashirika ya Biashara na Haki za Binadamu (2019), na A/HRC/41/43, katika aya ya 39.

[102] Vyanzo vya GIIP vilivyotolewa katika kipindi hiki na kulenga miradi ya maendeleo ya kimataifa ni pamoja na: Kundi la Benki ya Dunia, Taasisi ya Kimataifa ya Wanawake, na Benki ya Maendeleo ya Kimataifa ya Marekani, Mwongozo wa Taarifa kuhusu Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana (2014); Kundi la Benki ya Dunia, Mwongozo wa Nyenzo za Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana: Muhtasari wa Sekta ya Elimu (Aprili 2015); Viwango vya USAID vya Ulinzi wa watoto (Agosti 2016); na Sera ya Kulinda Watoto ya Idara ya Mambo ya Nje na Biashara ya Australia (DFTA) (2017). Ikumbukwe, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kundi la Benki ya Dunia kuhusu Kushughulikia GBV katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia (2018) *hayajajumuishwa katika muhtasari wa GIIP uliowasilishwa katika sehemu hii kwa sababu hayajumuishi ukatili dhidi ya watoto.* Hata hivyo, Maelezo hayo hayabainishi kuwa shughuli yoyote ya kingono na watu walio chini ya umri wa miaka 18 inachukuliwa kuwa "unyanyasaji wa watoto kingono" kwa sababu watoto hawawezi kutoa idhini kwa kuelewa kwa shughuli za aina hii. WBG, Septemba 28, 2018, Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia katika Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi Inaayohusisha Kazi Kuu za Kiraia, uk. 6. Yanapatikana hapa: https://documents1.worldbank.org/curated/en/399881538336159607/Environment-and-Social-Framework-ESF-Good-Practice-Note-on-Gender-based-Violence-English.pdf.

- Kusambaza sera za serikali na taratibu za kuripoti kuhusu dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia shuleni kwa wazazi, vyama vya wazazi na walimu (PTAs), kamati za shule na makundi ya jamii.
- Kuimarisha uwezo wa wazazi/walimu na mashirika ya jamii kufuatilia hali shuleni kuhusu ulinzi wa watoto na kusaidia kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.
- Kuzingatia kulinda na kutunza watoto katika upangaji wa miradi, na kuhitaji miradi kutekeleza uajiri kwa njia salama kwa watoto na taratibu za kukagua wafanyakazi na wanakandarasi.
- Kuhakikisha mteja anafuata masharti thabiti zaidi ya utunzaji na ulinzi wa watoto yaliyoundwa chini ya sheria za eneo, kitaifa na kimataifa.

Kuanzia mwaka wa 2020 hadi mwaka wa 2022, wakati wa miaka ya mwisho ya usimamizi wa mradi wa IFC, mwongozo wa ziada kuhusu unyanyasaji wa watoto kingono na GBV ulitolewa ili kutumiwa na taasisi za fedha za maendeleo ya kimataifa, ikijumuisha IFC.[103] Katika mwezi wa Desemba mwaka wa 2020, IFC, Benki ya Ulaya ya Ujenzi na Maendeleo (EBRD), Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (CDC), na Maendeleo ya Jamii ya Moja kwa Moja walitoa Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu. Hii iliwakilisha mwongozo wa kwanza wa IFC ambao unalenga wazi unyanyasaji wa watoto kingono katika sekta ya elimu, na kuonyesha kwamba "GBVH ni suala nyeti na la kimfumo katika sekta ya elimu" lililo na "athari za kudumu kwa masomo, afya, ustawi na ya safari ya kuajiriwa kwa wanafunzi," pamoja na athari zinazoweza kutofautishwa kijinsia kwa wavulana na wasichana (uk. 1). Chapisho linashughulikia GBVH kati ya wanafunzi, kati ya walimu na wanafunzi, kati ya walimu na wafanyakazi, na nyumbani na katika jamii-maswala yote yalio muhimu kwa uwekezaji huu.

IFC pia ilijiunga na EBRD na CDC katika kuzindua mwongozo kwa wawekezaji na makampuni kuhusu ushughulikiaji wa hatari za GBVH na sekta ya kibinafsi katika masoko yanayoibuka.[104] Kwa kuongezea, Ofisi ya Mambo ya Nje ya Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza (iliyokuwa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa) ilitoa Mwongozo wa Utafiti wa Kabla ya mradi wa Ulinzi wa watoto kwa Washirika wa Nje mwaka wa 2020.

[103]Ikumbukwe Maelezo ya Matendo Mazuri ya Kushughulikia ukatili na unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia (SEA/SH) kwa Ufadhili wa Uwekezaji kwa Miradi inayohusisha Kazi Kuu za Kiraia (2020), au Maelezo ya Matendo Mazuri ya kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (2020) yanahusu ukatili dhidi ya watoto, lakini haihusiani na vitendo vya WBG kuhusiana na GBV katika miktadha mingine. Vinapatikana hapa: https://thedocs.worldbank.org/en/doc/632511583165318586-0290022020/original/ESFGPNSEASHinmajorcivilworks.pdf na hapa: https://www.ifc.org/en/insights-reports/2020/publications-gpn-addressinggbvh.

[104] IFC, Julai 2020, ***Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia: Mazoea Mazuri Yanayoibuka kwa Sekta Binafsi.*** Yanapatikana hapa: https://www.ifc.org/en/insights-reports/2020/publications-gpn-addressinggbvh.

# 3. Uchambuzi wa Matokeo ya CAO na Kutoridhia: E&S ya IFC Utafiti wa Kabla ya Mradi

## 3.1. Maelezo ya jumla ya E&S ya IFC ya Utafiti Wa Kabla Ya Mradi

Tathmini ya athari kwa mazingira na jamii (ESDD) ya IFC kwa Bridge kama mteja mtarajiwa ilipuuza hatari na athari zinazoweza kutokea zinazohusiana na utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto, ikiwa ni pamoja na hatari ya unyanyasaji wa watoto kingono (CSA).

Katika kufanya tathmini yake kuanzia Juni hadi Oktoba mwaka wa 2013, IFC ilizingatia Viwango vya Utendakazi (PSs) vifuatavyo kuwa vinatumika kwa mradi:

- PS1: Tathmini na Ushughulikiaji wa Hatari na Athari kwa Mazingira na Jamii
- PS2: Ajira na Mazingira ya Kazi
- PS3: Kutumia Rasilimali Vizuri na Kuzuia Uchafuzi
- PS4: Afya na Usalama wa Jamii [105]

IFC ilisema kuwa PS5 kuhusu Upataji wa Ardhi na Makazi Mapya bila Hiari haikutumika kwa sababu shule mpya za Bridge kwa ujumla zilijengwa ndani ya makazi yasiyo rasmi au maeneo ya watu wa kipato cha chini ambapo ardhi ilikuwa imeharibiwa sana na kubadilishwa matumizi.[106] Pia ilisema kuwa PS6 kuhusu Kuhifadhi kwa Bayoanuai na Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Hai na PS7 kuhusu Watu wa Kiasili hazikutumika kwa sababu shule za Bridge zilijengwa ndani ya mazingira ya mijini nchini Kenya.[107] Taarifa iliyotolewa na IFC inataja kukosekana kwa hatari na athari zinazohusiana na PS5 na PS6 kuwa sababu kuu kwa nini IFC iliainisha shughuli hiyo kuwa kitengo cha Hatari Kwa Mazingira na kwa Jamii B—inayochukuliwa kuwa inawasilisha hatari na athari finyu za E&S, zinazoweza kuondolewa na kupunguzwa kwa urahisi.[108]

Wakati wa utafiti wa kabla ya mradi wa IFC, Bridge ilikuwa imendesha shughuli zake kwa kipindi cha miaka minne na ilikuwa imejenga shule 211 nchini Kenya, zilizohudumia takribani wanafunzi 57,000. Licha ya kuwa na shule nyingi na hatari nyingi za E&S zinazohusiana na ujenzi na uendeshaji wa shule, IFC haikufanya ukaguzi wa nyanjani wakati wa mchakato wa ESDD. Wala haikukagua utoshelevu wa mteja mtarajiwa kutambua hatari na athari kwa jamii kutoka kwa mradi huu. Badala yake, IFC ilizingatia uchanganuzi wake wa utafiti wa kabla ya mradi kwa kutumia stakabadhi zilizochaguliwa na mteja ambazo ziliangazia mbinu ya Bridge ya kujenga shule zake na matumizi yake, afya na utoaji wa usalama pamoja na tathmini ya athari kwa mazingira kwa shule moja ilyopendekezwa.[109] Kwa kuongezea, IFC ilifanya "mahojiano kwa njia ya simu" na afisa mkuu mtendaji wa Bridge na mshirika mkuu wa kifedha wa shirika ambaye aliwasilisha kuhusu utendakazi wa shule za Brigde kimazingira

[105] IFC, 2013, ESRS. Inapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.
[106] Ibid.
[107] Ibid.
[108] Ibid.
[109] ESRS inataja jinsi stakabadhi zifuatazo zilivyokaguliwa na IFC wakati wa tathmini: “Mipango ya Maisha, Moto na Usalama; Mpango wa Kazi, Usalama na Afya; Muhtasari wa Mifumo ya Mahusiano na Jamii; Mwongozo wa Vifaa na jinsi Vinavyotunza; Muundo wa Vyoo, Stakabadhi kuhusu Idadi ya Wanafunzi na Wanavyoketi; Masharti ya Ujenzi wa Vyoo vya Bridge International Academy (BIA); Taratibu za Usimamizi wa Mtoa huduma za Chakula cha mchana; Utafiti wa Soko na Uwasilishaji wa Muhtasari kuhusu Uchaguzi wa Eneo; Uwasilishaji wa Mchakato wa Upataji wa Eneo la Kujenga; Mipango mbalimbali ya ujenzi; picha za Shule halisi za Bridge na; Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa shule iliyopendekezwa ya Bridge International Academy (L13454) eneo la Kimilili, nchini Kenya." Inaonekana kwamba IFC pia ilipitia Kitabu cha Mwongozo wa Wafanyakazi, ambacho kimetajwa kwa ufupi katika sehemu ya Kiwango cha 2 cha Utendakazi cha ESRS. IFC, 2013, ESRS. Kinapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.

na kijamii.[110] Kwa kawaida, ESDD huhusisha kuwasiliana moja kwa moja na mtaalamu wa E&S ili kukagua na kuthibitisha taarifa muhimu.

Kuhusiana na mahitaji chini ya PS1, IFC ilibainisha katika Muhtasari wake wa Ukakuzi wa Mazingira na Jamii (ESRS) kabla ya kuwekeza kwa mradi kwamba Bridge ilikuwa katika mchakato wa kutengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMS) wa kikundi ambao ungetambua na kushughulikia hatari na athari. Mpango wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESAP) wa awali, uliokubaliwa kati ya IFC na mteja wake Oktoba mwaka wa 2013, uliwajibisha Bridge kubuni na kutekeleza ESMS kwa shule zake zote kufikia tarehe 31 Januari mwaka wa 2014.

Kuhusiana na PS4, IFC ilibainisha katika mradi wa ESRS kwamba shule za Bridge wakati huo hazikuwa na wafanyakazi wa kudumisha usalama lakini ziliajiri "mfanyikazi wa jumla" ambaye aliishi kwenye eneo hilo na kuelekezwa jinsi ya kukabiliana na masuala ya usalama.[111] Kwa kuongezea, IFC ilisema kuwa "Bridge ina mifumo na taratibu thabiti za ushirikishwaji wa jamii."[112]

### 3.1.1. Utafiti wa kabla ya mradi na ulinzi wa watoto

IFC pia iliidhinisha ripoti ya mtaalamu wa sekta ya ndani (wa elimu) kama sehemu ya ESDD yake ya Bridge. Huku ikizingatiwa utamaduni wa uwajibikaji wa hali ya juu wa Bridge, ripoti hii iliipa IFC maaelezo kuhusu mambo hatari yanayohusiana na ulinzi wa watoto katika shule zinazoendeshwa na mteja wake mtarajiwa. Hasa, IFC iligundua kuwa wanafunzi wa Bridge kwa ujumla waliishi maisha ya chini ya dola 1 kwa siku na huenda wakakabiliwa na changamoto za masomo na/au changamoto nyumbani ambazo zinaweza kutatiza masomo yao. Isitoshe, IFC ilifahamishwa kuwa Bridge ilikuwa ikifanya kazi kwa karibu na TSC wakati huo ili kusajili walimu wote kwa wakati ufaao. Hii ilikuwa muhimu kwa sababu ilionyesha kuwa Bridge ilitegemea walimu ambao hawakuwa wamesajiliwa, jambo liliongeza hatari kwa kiwango kikubwa kwa kuwa ulinzi uliopo wa serikali kwa watoto (angalia sehemu ya 2.2.) hauwezi kutumika.

Katika kukagua stakabadhi za jumla za utafiti wa IFC wa kabla ya mradi, CAO ilipata rejeleo moja la unyanyasaji wa watoto kingono. Stakabadhi hiyo ilirejelea kesi ya *R v. Abdallah Changoma* (Kesi ya Uhalifu nchini Kenya Namba 491, 2013), ambapo mwalimu wa Bridge alishtakiwa kwa kumdhulumu mwanafunzi. Rekodi za umma zinaonyesha kuwa awali mwalimu huyo alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha katika jela mwezi wa Novemba mwaka wa 2014, lakini mwezi wa Oktoba mwaka wa 2015 mahakama ya rufaa ilibatilisha hukumu hiyo na kumwachilia huru mwalimu huyo.

## 3.2. Matokeo ya Uchunguzi wa CAO

### 3.2.1. Maelezo ya Jumla

Baada ya kukagua stakabadhi za mradi wa IFC na kufanya mahojiano na kikosi cha mradi wa IFC cha uwekezaji kwa Bridge, CAO inatoa kauli kuwa ESDD ya IFC ya kabla ya uwekezaji haikuzingatia upeo kamili wa uwezekano wa kutokea kwa hatari na athari kwa jamii kama inavyotakiwa na Sera ya Uendelevu ya IFC (aya 12, 27, na 28). Kimsingi, IFC haikuzingatia hatari zinazoweza kutokea zinazohusiana na utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto kwa ujumla, au vitisho vinavyohusiana na CSA kwa wanafunzi.[113] Kwa hivyo, kabla ya uwekezaji, hakuna

[110] Ibid.
[111] IFC, 2013, ESRS. Inapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.
[112] Ibid.
[113] CAO inaona kwamba hakuna stakabadhi za tathmini zilizopitiwa wakati wa uchunguzi huu zinaangazia: "ulinzi wa watoto," "utunzaji wa watoto," "unyanyasaji wa watoto kingono," "unyanyasaji wa watoto," "ukatili dhidi ya watoto" au "unyanyasaji wa kijinsia."

kipengele chochote cha sera zilizopo za Bridge za kulinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa watoto kingono (CSA) au aina zinazoingiliana za unyanyasaji wa kijinsia (GBV) kilitambuliwa, kutathminiwa, au kutathminiwa dhidi ya GIIP au kutumia vipengele vya kisheria vya Kenya viliyoundwa kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono. Hii ilimaanisha, wakati wa ESDD, IFC haikuzingatia wala kujitayarisha kufanya kazi na Bridge ili kuhakikisha, kwamba mteja alikuwa na mikakati ya kuzuia, kupunguza, na kudhibiti hatari hizo. Matokeo ya utendakazi yalikuwa kwamba hatari zinazohusiana na CSA na hatua za kuzipunguza hazikujumuishwa katika Mkakati kazi wa E&S (ESAP)—stakabadhi muhimu ambayo hutumiwa na IFC na wateja wake kuongoza kazi ya ushughulikiaji wa hatari za E&S wakati wa utekelezaji wa mradi.

Utafiti wa IFC wa kabla ya mradi ulishindwa kushughulikia athari kwa jamii ambazo hujitokeza katika sekta ya elimu, licha ya kufahamu kuhusu kisa cha unyanyasaji wa watoto kingono kupitia stakabadhi zake za tathmini mwezi wa Desemba mwaka wa 2013. Matokeo yake, uwekezaji huo uliidhinishwa bila IFC kutambua hatari na athari za CSA na kutathmini uwezo wa mteja kuzishughulikia. IFC haikuthibitisha kuwa Bridge ilikuwa na mfumo unaohitajika wa E&S, sera, na taratibu, na huenda ikakosa uwezo kupitia vitendo wa kushughulikia hatari za CSA au kukidhi mahitaji ya GIIP na sheria ya Kenya kama inavyotakiwa na PS1 (aya 3, 6, na 7). Ingawa IFC ilizingatia hatari fulani kwa usalama wa wanafunzi kuhusiana na ujenzi wa majengo, usafi wa mazingira, na moto wakati wa ESDD,[114] haikuzingatia hatari zinazohusiana na CSA kwa njia yoyote ile.

Kwa kuongezea, wakati stakabadhi za utafiti wa kabla ya mradi zinaonyesha kwamba wanafunzi wa Bridge walikuwa hatarini zaidi kutokana na umaskini, IFC haikuzingatia uhusiano wa kuwa hatarini zaidi na ngono, jinsia, umri, na mambo mengine (kama ilivyoorodheshwa katika Viwango vya Utendakazi),[115] yanayoweza kuchangia kuongezeka kwa hatari ya CSA kutokana na umaskini. IFC pia haikutathmini au kuuliza Bridge kuhusu ulinzi wake wa watoto na utunzaji wake wa watoto. Kutotekeleza haya kulitokea licha ya sheria za Kenya za utunzaji wa watoto kwa mazingira ya elimu na uwepo wa mwongozo wa GIIP kuhusu viwango vya utunzaji wa watoto.

Iwapo IFC ingechanganua kiwango na ubora wa tathmini ya athari kwa jamii za mteja wake na ushughulikiaji wa E&S zinazoweza kutokea na mapungufu ya mradi unaotarajiwa kwa kuzingatia mahitaji husika ya PS, ingeweza kutambua hatari zaidi kwa jamii, ikiwa ni pamoja na CSA. PS1 inahitaji kuwa kama sehemu ya mchakato wa kutambua hatari na athari, mteja atambue watu binafsi na vikundi ambavyo vinaweza kuathiriwa moja kwa moja na kwa njia tofauti au vibaya na mradi kutokana na hali zao duni au kuwa hatarini zaidi.[116] Kama matokeo yake, tathmini kama hiyo pia ingetathmini mradi na muktadha wake kwa kuzingatia GIIP zinazohusiana na utunzaji na ulinzi wa watoto katika sekta ya elimu ya kibinafsi ya K-12 katika mazingira ya mapato ya chini, pamoja na sheria za Kenya za kuwalinda na kuwatunza watoto.[117]

### 3.2.2. Uwezo wa mradi kuwa na hatari za CSA

Katika kuchunguza mapungufu ya ESDD ya IFC, ni muhimu kutambua muktadha wa kitaasisi, kitaifa na kimataifa kwa wakati huo, ambapo hatari za CSA-ikiwa ni pamoja na mazingira ya shule-zilijulikana vyema, ikiwa ni pamoja na:

- **Katika ngazi ya Kimataifa**, hatari za CSA zinazohisiana na mazingira yote ya shule za msingi na sekondari kutokana na mazoea na kujumuika moja kwa moja kati ya wanafunzi na wafanyikazi

[114] Tazama, kwa mfano, ESRS, Octoba 30, 2013. Inapatikana hapa: https://disclosures.ifc.org/project-detail/ESRS/32171/bridge-international-academies.
[115] PS1, 2012, aya ya 12, tanbihi ya 18. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.
[116]PS1, aya ya 12. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.
[117] Ibid, aya ya 7.

wanaowahudumia moja kwa moja. Mwingiliano huu wa muda mrefu unahusishwa na hatari kuu zinazotambulika za unyanyasaji wa watoto kingono katika mazingira yote ya elimu katika nchi zote.[118]

- **Nchini Kenya**, unyanyasaji wa watoto kingono na aina zinazoingiliana za GBV dhidi ya watoto zimeenea, huwa haziripotiwi, umechukuliwa kama jambo la kawaida na hutegemea na jinsia ya muathiriwa. Kwa pamoja, ripoti ya mwaka wa 2010 ya shirika lisilo la kiserikali (NGO) linalosimamia nambari kuu zaidi ya kupiga simu bila malipo kuhusiana na CSA nchini,[119] utafiti wa kitaifa wa mwaka wa 2010 kuhusu ukatili dhidi ya watoto nchini Kenya,[120] na ripoti ya mwaka 2011 ya Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu ubaguzi wa kijinsia nchini[121] zote zinaonyesha kuenea kwa CSA na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya elimu nchini Kenya.

Iwapo IFC ingefanya tathmini ya kina ya kijamii kuhusiana na hatari za utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto, ingeelewa vyema zaidi ukubwa wa hatari ambayo CSA inayohusiana na mradi na GBV dhidi ya watoto kwa mapana inayotolewa kwa watu binafsi na kwa malengo mapana ya maendeleo katika jamii. Waathiriwa wa CSA huteseka milele na kuna uwezekano wa kuathiriwa kizazi baada ya kizazi, ikiwa ni pamoja na madhara makubwa ya kudumu kwa kwa ukuaji wao wa mwili, hisi, kijamii na kihisia, pamoja na shida za kiuchumi kutokana na kupoteza tija, ulemavu, na kupungua kwa ubora wa maisha.[122]

### 3.2.3. Kutoridhia kwa IFC

**IFC ilishindwa kutekeleza majukumu yake ya utafiti wa kabla ya mradi kama ilivyoainishwa katika Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii ("Sera ya Uendelevu") aya ya 20 hadi 28.**

Wakati wa kukagua hatua za IFC dhidi ya mahitaji ya Mfumo wa Uendelevu yaliyoainishwa katika sehemu ya 2, CAO inapata kuwa IFC haikuridhia katika utekelezaji wake wa utafiti wa kabla ya mradi unaostahili kabla ya uwekezaji. Utafiti wa IFC wa kabla ya mradi haukukidhi mahitaji ya Sera ya Uendelevu, haswa aya 12 na ya 20 hadi 28, ikizingatiwa hali na kiwango kikubwa cha shughuli za Bridge na hatari kubwa za CSA zinazohusiana na mradi unaohusisha kujumuika kwa mara kwa mara kati ya watu wazima na wanafunzi, wanafunzi wa K–12 katika jamii za kipato cha chini. IFC haikuzingatia hatari za CSA za mradi zinazoweza kutokea, wala kuzingatia uwezo wa mteja wake mtarajiwa kukidhi mahitaji ya Kimazingira na Kijamii (E&S) kuhusiana na hatari na athari za CSA.

[118] Tazama, Mwongozo wa UNICEF Mazingira Bora Shuleni kwa Watoto (2009); IFC, Desemba 2020, Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu; na UNESCO-UN Women, 2016, Mwongozo wa Kimataifa wa Kushughulikia GBV Shuleni. Unapatikana hapa:https://www.unicef.org/media/66486/file/Child-Friendly-Schools-Manual.pdf; hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/gpn-addressinggbvh-july2020.pdf; na hapa: https://www.unwomen.org/en/digital-library/publications/2016/12/global-guidance-on-addressing-school-related-gender-based-violence.

[119] Childline Kenya, 2010, Unyanyasaji Wa Watoto Kingono nchini Kenya: Kutokea Kwake, Muktadha, Vihatarishi na Matokeo, uk. 8. Unapatikana hapa: https://childlinekenya.co.ke/assets/files/Child%20Sexual%20Abuse%20Research%20Report-CLK-2011.pdf. "Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya nchini Kenya uligundua kuwa asilimia 12 ya wanawake nchini Kenya wenye umri wa miaka kati ya 15 na 49 walisema kwamba walilazimishwa kufanya ngono mara ya kwanza. Idadi hii iliongezeka hadi asilimia 23 kwa wanawake ambao walisema walifanya ngono mara ya kwanza kabla ya umri wa miaka 15. Utafiti wa hivi karibuni wa Girl Childline Network katika mwaka wa 2011 uliohusisha watoto wa shule kutoka eneo la Tana River nchini Kenya uligundua kuwa asilimia 25 ya wasichana walipitia hali ya kudhulumiwa kingono kupitia kuguswa na asilimia 10 walikuwa wamelazimishwa kufanya ngono au walifanya bila kutaka. Ushahidi wa kina pia unaonesha kwamba dhuluma za kingono ni tatizo la kawaida nchini Kenya."

[120] UNICEF, CDC, Jamhuri ya Kenya, na Pamoja kwa Manufaa ya Wasichana, 2010, Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Kenya (VAC). Utafiti huu - ambao unafuatilia maisha kwa jumla na hali ya sasa ya watoto wa kike 1,227 na wa kiume 1,456 kati ya umri wa miaka 13 na 24 waliodhulumiwa kabla ya umri wa miaka 18 - uliwakilisha utafiti wa kisasa zaidi na wa kina kuwahi kufanywa kuhusu kuenea kwa dhuluma za kingono, kimwili na kisaikolojia kwa watoto chini ya miaka 18 nchini Kenya. Unapatikana hapa: https://evaw-global-database.unwomen.org/-/media/files/un%20women/vaw/full%20text/africa/kenya%20violence%20against%20children%20survey%20%202010.pdf?vs=1219.

[121] Maoni yaliofikiwa na Kamati ya Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake, 2011, CEDAW/C/KEN/CO/7. Yanapatikana hapa: https://www2.ohchr.org/english/bodies/cedaw/docs/co/CEDAW-C-KEN-CO-7.pdf.

[122]Tazama, kwa mfano: UNICEF, 2014 Wazi ila Fiche: Uchambuzi wa Takwimu za Ukatili Dhidi ya Watoto, uk. 62. ("Matukio ya unyanyasaji wa kingono utotoni hudhuru vipengele vyote vya ukuaji: kimwili, kisaikolojia na kijamii."); na IFC, EBRD, CDC, na Maendeleo ya Jamii Moja kwa Moja (2020), Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu uk.1. Inaonyesha kwamba "GBVH ni suala nyeti na la kimfumo katika sekta ya elimu" ambalo hutokea katika mazingira yote ya elimu na lina "athari za kudumu katika ujifunzaji, afya, ustawi na njia ya kupata ajira kwa wanafunzi," pamoja na uwezekano wa kutokea kwa athari zinazotofautiana kijinsia kwa wavulana na wasichana). Inapatikana hapa: https://data.unicef.org/resources/hidden-in-plain-sight-a-statistical-analysis-of-violence-against-children/ na hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/gpn-addressinggbvh-july2020.pdf

Kutokana na hali hii, IFC haikupendekeza hatua zozote za kipekee au za kukabiliana na hali ili kuhakikisha kwamba Bridge inashughulikia hatari na athari hizo. Aidha, kwa kutotathmini hatari za CSA na athari zinazoweza kutokea za mradi wala uwezo wa mteja kuzishughulikia, IFC haikuwa na msingi wa kufikia uamuzi kwamba mradi unaweza kukidhi mahitaji ya Kimazingira na Kijamii (E&S) ya IFC yanayohusiana na CSA ndani ya muda unaofaa -hali inayohitajika kwa IFC kufanya uwekezaji.[123]

**Mifano ya kutoridhia majukumu yake ya ESDD ni pamoja na kushindwa kwa IFC:**

- Kutoa wito kwa Bridge iandae au iagize tathmini ya hatari za E&S katika jamii kwa kuzingatia ukubwa wa mradi na idadi ya walengwa walio hatarini kuathiriwa na ingejumuisha hatari za CSA na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) kwa jamii (kama inavyotakiwa katika PS1).
- Kutathmini sera na taratibu zilizopo za Bridge za kuzuia na kukabiliana na CSA na GBV kwa kuzingatia GIIP na kufuata sheria za nchi ya Kenya zilizoundwa ili kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono (kama inavyotakiwa katika PS1, aya ya 6 na 7, na PS4, aya ya 5).
- Kushughulikia utegemejii wa Bridge kwa walimu ambao hawakuwa wamesajiliwa. Hii ilikuwa inahusiana hasa na hatari za CSA kwa sababu viwango vya usajili vya serikali vilijumuisha vipengele ambavyo vingechangia kwa upunguzaji wa hatari za kiafya, na kwa usalama wa watoto. Utafiti wa IFC wa kabla ya mradi ulionyesha kwamba usajili ulihitajika chini ya sheria ya Kenya na IFC ina wajibu wa kuwataka wateja wake kuridhia sheria za kitaifa zinazohusika (PS1, aya ya 6).[124]
- Kufikiria kuhusu mambo yanayoingiliana yanayowafanya wanafunzi kuwa hatarini zaidi, kama vile utambulisho wa jinsia, jinsia, umri, na mambo mengine, na kutathmini ikiwa Bridge iliweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa athari mbaya zinazohusiana na CSA hazikumbi kwa kiasi kikubwa wanafunzi (tayari) waliokuwa hatarini kuathiriwa (kama inavyotakiwa na PS1, aya ya 12).

### 3.2.4. Athari za mapungufu ya IFC kwa ESDD

Matokeo ya utafiti wa IFC wa E&S kabla ya mradi kuhusu shughuli inayopendekezwa ya biashara ni hatua muhimu katika mchakato wake wa kuidhinisha na huamua upeo wa masharti ya E&S yanayohusishwa na ufadhili wa IFC. Kwa kutozingatia utafiti wa kabla ya mradi unaostahili, IFC ilijiibulia changamoto nyingi kuhusiana na kufanya kazi na mteja wakati wa usimamizi ili kufanya mradi kuridhia Viwango vya Utendakazi 1 na 4. Hasa, IFC ilianza kusimamia mradi bila kufikia makubaliano na mteja kuhusu:

- Kutambua watu binafsi na vikundi ambavyo vinaweza kuathiriwa moja kwa moja na kwa njia tofauti au kwa kiasi kikubwa na mradi kutokana na hali yao ngumu au kuwa hatarini zaidi.[125]

---

[123] IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya ya 22. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/sp-english-2012.pdf.

[124] Hitaji la kuwa na walimu waliosajiliwa kwa idadi ya kutosha huchangia kupunguza hatari kwa watoto kwa kuwa walimu waliosajiliwa mbali na kuwa na shahada ya taaluma ya elimu ambayo iliwapa mafunzo kuhusu jinsi ya kufanya kazi kwa njia salama na watoto pia lazima watoe cheti cha mwenendo mzuri na fomu ya matibabu, na wahalifu wa ngono wanaopatikana na hatia huwa hawasajiliwi. Mahitaji ya Usajili na Uajiri wa Walimu. Yanapatikana hapa: https://www.tsc.go.ke/index.php/services/teacher-registration/registration. Tazama, pia, Kanuni za Kufuatwa za Tume ya Kuajiri Walimu za mwaka wa 2015, kifungu cha 20. Zinapatikana hapa: http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/LegalNotices/196-Teachers_Service_Commission_Regulations__2015.pdf, na TSC Circular, 3/2010. Zinapatikana hapa: https://www.tsc.go.ke/index.php/downloads-b/file/22-circular-on-protection-of-pupils-students-from-sexual-abuse-2010.

[125] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, aya ya 12. Vinapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

- Hatua za kukabiliana na hali na za utendakazi na hatua zinazolingana na hizi katika ESAP na masharti mengine ya uwekezaji wa IFC ya kushughulikia hatari za CSA na kuhakikisha mradi utaendeshwa kwa kuzingatia sheria husika za kitaifa, kukidhi mahitaji ya PS zinazohusika, na kuzingatia GIIP.[126]

- Mahitaji ya ufuatiliaji na kuripoti kuhusiana na visa vya CSA na utendakazi wa mteja.

Hasa, ukosefu wa kurejelea masuala ya CSA katika Mkakati Kazi wa E&S ulisababisha athari kubwa kwa usimamizi wa IFC wa hatari na athari za CSA zilpoendelea kujitokeza wakati wa usimamizi.[127]

[126] Mpango wa Utekelezaji wa Kimazingira na Kijamii (ESAP) unabainisha masuala muhimu ya kushughulikiwa wakati wa usimamizi wa mradi na hatua zinazopaswa kutekelezwa na mteja.
[127] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, Kiwango cha kwanza cha Utendakazi kinahitaji kwamba ESAPs, mikakati na hatua zilizobainishwa "…ziwiane na hatari na athari za mradi" (aya ya 15), na kufafanua "…matokeo na hatua zinazotarajiwa kushughulikia masuala yaliyoibuliwa katika mchakato wa utambuzi wa hatari na athari, kama matukio yanayoweza kupimika kadiri inavyowezekana, na vipengele kama vile viashirio vya utendakazi, shabaha, au vigezo vya kukubalika ambavyo vinaweza kufuatiliwa kwa muda uliobainishwa na pamoja na makadirio ya rasilimali na majukumu ya utekelezaji" na pamoja na makadirio ya rasilimali na majukumu ya utekelezaji (aya ya 16). Vinapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf.

# 4. Uchambuzi wa CAO na Matokeo ya Kutoridhia wakati wa Usimamizi

Sehemu hii inaeleza na kuchanganua shughuli za usimamizi wa mradi kati ya Januari mwaka wa 2014 na kujiondoka kwa IFC kwenye mradi Machi mwaka wa 2022. Inaangazia nyakati mbili kuu: i) kipindi cha usimamizi kabla ya CAO kwenda nyanjani nchini Kenya Februari 7–14, 2020, kwa ajili ya uchunguzi wa Bridge-01; na ii) kipindi kinachofuatia hadi IFC ilipojiondoa tarehe 3 Machi mwaka wa 2022.

## 4.1. Maelezo ya jumla kuhusu usimamizi wa IFC

Sehemu hii inatoa maelezo ya kile kilichotokea katika kipindi cha miaka minane ya usimamizi wa IFC wa uwekezaji wake katika Bridge International Academies, ikifuatiwa na matokeo ya CAO kuhusu IFC kutoridhia mahitaji ya Mfumo wa Uendelevu katika kipindi hiki.

IFC inahitajika chini ya Sera yake ya Uendelevu kutekeleza programu ya kawaida ya kumsimamia mteja kwa mujibu wa Taratibu za Ukaguzi wa Mazingira na Jamii za IFC (ESRP). Kama sehemu ya mchakato huu, IFC ilikuwa na wajibu wa kutambua na kukagua fursa za kuboresha zaidi utendakazi wa E&S wa mteja wake, kufanya kazi na mteja kushughulikia mabadiliko katika hali ambazo zinaweza kusababisha athari mbaya kwa mazingira au kwa jamii, na ikibidi kumfanya mteja kuridhia.[128] Hasa, kwa kuzingatia hatari na athari za CSA, mteja wa IFC alitakiwa kuridhia Viwango vya Utendakazi vya 1 na 4 katika kipindi chote cha mradi, sheria za kitaifa za Kenya kuhusu ulinzi wa watoto, ikijumuisha shuleni, na GIIP kuhusu utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto katika shule za K-12.

Katika kutathmini mambo yafuatayo ya kufanya au kutofanya kwa IFC, CAO ilitazama mbinu ya IFC ya usimamizi kwa kuzingatia muktadha huu. Kwa muhtasari, CAO inaona kwamba IFC ilikuwa na uelewa wa vipengele mbalimbali wakati wa usimamizi wa uwezekano wa hatari na athari kutokea na hatari halisi za unyanyasaji wa watoto kingono katika shule za Bridge na, kabla ya Machi mwaka wa 2020, ilishindwa kufuatilia ipasavyo taarifa hizo. Ingawa CAO inatambua kwamba IFC ilifanya uboreshaji mkubwa katika usimamizi wake kuanzia Machi mwaka wa 2020, mapungufu yalisalia. Kwa ujumla, usimamizi wa IFC haukulingana na uzito wa hatari inayoweza kuwapata watoto katika shule za mteja wake.

### 4.1.1. Usimamizi wa IFC kabla ya CAO kupokea taarifa kuhusu CSA inayohusiana na mradi Februari mwaka wa 2020

Mbinu ya IFC kuhusu kulinda na kutunza watoto kuhusiana na uendeshaji wa shule za Bridge ilitofautiana sana kabla na baada ya CAO kufahamu kuhusu visa vya CSA wakati ilipokutana na wanajamii kuchunguza malalamishi ya Bridge-01. Kuanzia kwa utoaji wa fedha za IFC kwa Bridge mwezi wa Januari mwaka wa 2014 hadi Februari mwaka wa 2020, IFC iliibua kwa nadra masuala yanayohusiana na utunzaji na ulinzi wa watoto na mteja wake ilipopata taarifa kuhusu visa vinavyohusiana na CSA. Katika awamu hii, IFC haikufanya jitihada za kujumuisha hatua za kushughulikia hatari na athari za CSA na kuchukua hatua za utunzaji na ulinzi wa watoto katika Mkakati Kazi wa E&S (ESAP) wa mradi ili kuhakikisha kuwa Mfumo wa Usimamizi wa E&S wa Bridge unashughulikia hatari na athari za CSA.

IFC ilitumia mbinu hii licha ya kupokea taarifa kuhusu visa kadhaa vya CSA mwaka wa 2013, 2016, na 2017, inavyofupishwa hapo chini:

---

[128] Sera ya Uendelevu pia inahitaji IFC kuweka mikakati inapohitajika iwapo mteja atakosa kuridhia ahadi zake kuhusu mazingira na jamii. IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya ya 45.

- Kesi moja ya uhalifu nchini Kenya ambapo mwalimu wa Shule ya Kimataifa ya Bridge alishtakiwa kwa kumdhulumu mwanafunzi mwaka wa 2013. IFC ilipokea ripoti hii Desemba mwaka wa 2013, mwezi ambao uwekezaji wa Bridge ulitiwa saini. Rekodi za umma zinaonyesha kuwa mwaka wa 2015 mwalimu huyo aliachiliwa huru.
- Visa vitatu vya unyanyasaji wa watoto kingono (Aprili mwaka wa 2016).
- Malalamishi kadhaa yalitolewa na wazazi na wanafunzi kuhusu CSA na GBV dhidi ya wanafunzi wa kike (Julai mwaka wa 2017).

Uzingatiaji na ushughulikiaji wa IFC wa ripoti hizi unajadiliwa hapo chini chini ya "Uchambuzi na Matokeo ya CAO kuhusu Usimamizi wa IFC."

Licha ya mambo haya, CAO haikupata stakabadhi za usimamizi wa mradi wa IFC zilizotolewa kabla ya Februari mwaka wa 2020 ambazo zinashughulikia visa, hatari, au malalamishi yoyote yanayohusiana na CSA au GBV dhidi ya watoto. Katika mwaka wa 2018, stakabadhi za usimamizi za IFC zilionyesha mafunzo kuhusu utunzaji wa watoto, ulinzi wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia ambao uliripotiwa. Hii ni mara ya pekee istilahi hizi kutajwa na IFC ambako CAO imebainisha katika rekodi za mradi kuhusu suala lolote linalohusiana na utunzaji wa watoto, ulinzi wa watoto, au GBV kuhusiana na shughuli za Bridge kati ya Januari mwaka wa 2014 na Desemba mwaka wa 2018.

Mwezi wa Desemba mwaka wa 2019, miaka mitano ya usimamizi wake wa Bridge, IFC iligundua na kuelezea wasiwasi wake kuhusu taarifa ya ziada kuhusu uwezekano wa CSA inayoingiliana na GBV kutokea. Hasa, IFC ilijadili matokeo ya majaribio ya miaka mitatu ya udhibiti bila mpangilio uliofanywa na Kituo cha Maendeleo Duniani (CGD) ikilinganisha shule ndani ya mpango wa ushirikiano wa serikali ya Liberia "LEAP" na shule nyingine za serikali. Bridge ilikuwa mmoja wa waendeshaji wanane wa kibinafsi waliosimamia mpango wa LEAP.[129] Kulingana na tafiti za wanafunzi, CGD iligundua kuwa shule za LEAP zinazosimamiwa na watoa huduma kadhaa wa kibinafsi, ikiwa ni pamoja na shule 23 zinazoendeshwa na Bridge, zilikuwa zimeshindwa kupunguza unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanafunzi. Ripoti hiyo pia ilisema kwamba kiwango cha juu cha kuacha shule katika shule za Bridge kuliko katika shule nyingine za LEAP na shule za serikali zisizo za LEAP kilionekana kutokana na mimba za wanafunzi.[130] Kulingana na ripoti mpya kuhusu utafiti wa CGD uliopitiwa na IFC, "Takriban asilimia 4 ya wanafunzi [wa LEAP] waliohojiwa ... katika mwaka wa 2019 waliripoti kujamiiana na mwalimu, na asilimia 7.5 walisema walikuwa na aina fulani ya mawasiliano ya ngono na mwalimu."[131] Katika mwezi wa Desemba mwaka 2019 na Januari mwaka wa 2020, IFC ilionyesha wasiwasi kuhusu matokeo ya CGD yanayohusiana na CSA kwa usimamizi wa mradi na pia ilitoa matokeo hayo kwa Bridge. Hata hivyo, CAO haikupata ushahidi wa hatua zilizofuata kutoka kwa IFC kushughulikia mambo yalioibuliwa na utafiti wa CGD.

### 4.1.2. Usimamizi wa IFC kuanzia Februari mwaka wa 2020 hadi ilipojiondoa kwenye mradi Machi mwaka wa 2022

IFC ilianza kufuatilia hatari za CSA zinazohusiana na mradi na kuchukua hatua za kuimarisha utendakazi wa ulinzi na utunzaji wa watoto wa Bridge pindi tu kufuatia ziara za CAO nyanjani za kushughulikia Bridge-01 nchini Kenya zilizofanyika Februari kati ya tarehe 7 na 14, mwaka wa 2020. Wakati wa ziara hii nyanjani, CAO

---

[129] Tazama pia maelezo yanayopatikana katika: Muhtasari wa Zaidi ya Mafanikio ya Muda Mfupi ya Manufaa ya Mafunzo: Athari za Huduma za Shule Kutoka Nje nchini Liberia baada ya Miaka Mitatu (Desemba 2019); Zaidi ya Mafanikio ya Muda Mfupi ya Manufaa ya Mafunzo: Athari za Huduma za Shule Kutoka Nje nchini Liberia baada ya Miaka Mitatu (Desemba 2019); Makala ya Zaidi ya Mafanikio ya Muda Mfupi ya Manufaa ya Mafunzo (Desemba 2019); na Athari za Huduma za Shule Kutoka Nje nchini Liberia kwa Bridge International Academies baada ya Miaka Mitatu (Septemba 2020).

[130] Tazama pia maelezo yanayopatikana katika: Muhtasari wa Zaidi ya Mafanikio ya Muda Mfupi ya Manufaa ya Mafunzo: Athari za Huduma za Shule Kutoka Nje nchini Liberia baada ya Miaka Mitatu (Desemba 2019).

[131] Devex, Desemba 18, 2019, Liberia inaendelea kufanyia majaribio elimu licha ya tathmini isiyopendeza. Inapatikana hapa: https://www.devex.com/news/liberia-forges-ahead-with-education-experiment-despite-lukewarm-evaluation-96238#.Xfo0ecjuZ0o.twitter.

ilifahamishwa kuhusu visa vya CSA, viliripotiwa kuwaathiri waathirika watoto 15, kupitia mazungumzo na wazazi wa Bridge ambao walikuwa wameripoti visa hivyo na wanajamii ambao walitoa msaada kwa waathirika.[132] Kikosi cha wachunguzi wa CAO waliporejea Washington, DC, CAO iliarifu usimamizi wa IFC mara moja kuhusu visa hivi, ambavyo Bridge haikuwa imeelezea IFC. Tarehe 25 mwezi wa Februari mwaka wa 2020, IFC ilifahamishwa kuwa mteja angetoa kwa Halmashauri ya Wakurugenzi rekodi za ripoti zote za unyanyasaji wa watoto kingono tangu mwaka wa 2013.

Mwezi uo huo, IFC ilifahamu kuhusu visa 70 vya CSA. CAO haikuweza kupata dalili yote kwamba IFC ilichukua hatua zozote kushughulikia ripoti hii.

#### *4.1.2.1. Machi 2020:* **Ziara ya IFC ya usimamizi nchini Kenya**

IFC ilifanya ziara ya usimamizi kwa makao makuu ya Bridge mjini Nairobi tarehe 4 na 5 Machi mwaka wa 2020, iliyonuia kujadili tu hatari zinazohusiana na unyanyasaji wa watoto na usalama wa watoto katika shughuli za Bridge. Ukaguzi wa CAO wa stakabadhi za mradi za IFC unaonyesha kuwa ziara hii ilikuwa mara ya kwanza kwa wataalamu wa E&S wa IFC kuzingatia kikamilifu mbinu na uwezo wa ulinzi na utunzaji wa watoto wa Bridge. Wakati wa ziara hiyo, IFC pia ilikagua stakabadhi za mwaka wa 2019 zinazohusu michakato na sera, uwezo, mifumo na mafunzo ya ulinzi wa watoto.

Maelezo ya IFC kutoka kwa ziara hii ya usimamizi yalionyesha wasiwasi kuhusu baadhi ya vipengele vya taratibu na uwezo wa Bridge. Kwa kuongeza, usimamizi wa IFC pia ulibainisha masuala ya kijamii ambayo hayakutambuliwa hapo awali na IFC. Haya yalijumuisha maswali kama Tathmini ya Athari za E&S zilizofanywa kwa shule za Bridge zilijumuisha usalama wa watoto.[133]

Tarehe 12 Machi mwaka wa 2020, IFC ilifahamu kuhusu visa zaidi vya CSA. Kwa kuzingatia uelewa wa IFC wa taratibu ambazo zilikuwa zimeanzishwa hivi majuzi na Bridge, masuala nyeti kama vile CSA yangetambulishwa kama masuala ya "hatari" na ujumbe wa ghafla ungetumwa kwa wasimamizi wakuu. Hata hivyo, hakuna stakabadhi yoyote ya E&S iliyotolewa na Bridge kwa IFC kati ya mwaka wa 2017 na mwaka wa 2022 ilifichua visa vyoyote ya CSA. Mapema katika mwaka wa 2020, IFC iligundua kuwa Bridge ilikuwa imeweka mfumo mkuu wa kuripotia visa vya unyanyasaji wa watoto na kwamba wafanyakazi wa Bridge walikuwa wamepokea mafunzo ya awali na ya ziada kuhusu mada za ESG, ikiwa ni pamoja na CSA na utunzaji wa watoto.

#### *4.1.2.2. Machi hadi Septemba mwaka wa 2020:* **Pendekezo la IFC la mkakati kazi wa kushughulikia CSA pamoja na mteja**

Tarehe 5 Machi mwaka wa 2020, IFC ilipendekeza kwa Bridge uundaji wa mipango ya siku kati ya 90 na 180 ambayo IFC na mteja wake wangeshughulikia kwa ushirikiano masuala yanayohusiana na afya na usalama wa watoto, na ushughulikiaji wa visa vya CSA. Pendekezo la IFC lilijumuisha: Bridge kuteua kituo cha E&S ili kufanya kazi na IFC; uwazi kamili katika kuripoti habari ikijumuisha visa vyovyote vya unyanyasaji wa kingono; kupitia upya kikamilifu hali ya afya na usalama na wataalam wa kujitegemea wanaoshughulikia utunzaji wa watoto; kitengo cha kukabiliana na visa; na hatua za ziada kutokana na ukaguzi unaoendelea.

[132] Kesi moja ilimhusu mwalimu wa Bridge ambaye anadaiwa kuwalawiti wanafunzi 13 (wa kike 11 na wa kiume wawili) katika kipindi cha mwaka wa 2016 na 2017. Kesi ya pili ilimhusu mwalimu wa Bridge ambaye alidaiwa kuwalawiti wanafunzi wawili wa kike mwaka wa 2019 na alikuwa amefutwa na Bridge kutokana na vitendo hivi.

[133] Ukaguzi wa CAO unaonyesha kuwa wakati wa ziara ya usimamizi ya Machi mwaka wa 2020, Bridge ilikuwa imepitia stakabadhi kuhusiana na kuenea kwa CSA katika nchi ambazo iliendesha shughuli zake lakini haikuwa imefanya tathmini ya hatari ya unyanyasaji wa watoto.

Mapendekezo yaliyotajwa hapo juu yalizingatiwa na IFC na Bridge siku sita baada ya Rais wa Kundi la Benki ya Dunia (WBG) kumwandikia Katibu wa Hazina wa Marekani akisema kwamba IFC itasitisha uwekezaji wa moja kwa moja katika shule za kibinafsi za K–12.[134]

Tarehe 1 Aprili mwaka wa 2020, IFC ilifahamu kuwa Bridge ilikuwa imezindua ukaguzi ambao ungeshughulikia vipengele vyote vya ulinzi na utunzaji wa watoto. Mwezi Juni mwaka wa 2020, IFC ilipokea nakala ya ukaguzi wa Bridge, ambayo ilijumuisha orodha ya kina ya shughuli za ulinzi na utunzaji wa watoto. IFC ilitoa mapendekezo zaidi kwa Bridge yaliyotayarishwa na mshauri mtaalamu wa masuala ya GBV ambaye aliyeteuliwa na IFC mapema katika mwaka wa 2020. Katika mwezi wa Septemba mwaka wa 2020, IFC ilimwomba mteja wake taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa kushughulikia mapendekezo ya mshauri. Stakabadhi za usimamizi wa IFC kuanzia Juni mwaka wa 2021 zilionyesha kuwa mapendekezo haya yalikuwa bado hayajashughulikiwa na Bridge, na uchunguzi wa CAO haukupata ushahidi wowote kwamba IFC ilithibitisha kabla ya kujioondoa kwake mwezi Machi mwaka wa 2022 kwamba Bridge illishughulikia mapendekezo hayo.

Kufikia Machi mwaka wa 2020, IFC ilikuwa imetambua haja ya kuziba mapengo yake ya upungufu wa maarifa kuhusiana na madai ya CSA; na kufanya kazi na mteja ili kuboresha kuwashughulikia watoto na kuwalinda. Ili kuendeleza juhudi hizi, IFC ilieleza Bridge mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa kamili zinazohusiana na masuala ya CSA kwa njia ya uwazi.

Kwa mfano, katika mwezi wa Septemba mwaka wa 2020, IFC iliomba taarifa kuhusu stakabadhi kadhaa zinazohusiana na utekelezaji wa Bridge wa hatua za ulinzi wa watoto. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO unaonyesha kwamba wataalamu wa E&S wa IFC walipokea tu mojawapo ya stakabadhi hizi, na kufanya kuwa vigumu kutathmini vizuri utendakazi wa mteja kuhusiana na ushughulikiaji wa hatari za CSA.

CAO iliarifiwa kwamba majaribio ya IFC ya kupata taarifa za kina kuhusu CSA katika kipindi hiki, na kusaidia Bridge kuimarisha sera na taratibu za ulinzi na utunzaji wa watoto, vilitatizwa na maoni ya mteja kuhusu umuhimu wa matumizi ya CSA ya Viwango vya Utendakazi vya IFC. CAO pia iliarifiwa kwamba mteja wa IFC pia aliona kwamba ESAP na stakabadhi zingine za usimamizi zinazohitajika na IFC hazikujumuisha marejeleo ya ulinzi wa watoto na kwa hivyo haikuwa na wajibu wowote kimkataba kuripoti hatari na athari za CSA. IFC iliarifiwa kwamba kwa maoni ya Bridge, Viwango vya Utendakazi havishughulikii kwa uwazi CSA, hatari za utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto.

Kuanzia mwaka wa 2019 kuendelea, wafanyakazi wa IFC walieleza Bridge mara kwa mara kwamba hatari zote zinazohusiana na unyanyasaji wa watoto zilishughulikiwa na Viwango vya Utendakazi vya 1 na 4 na hivyo kupelekea kazi ya kutathmini, kufuatiliwa na kusimamiwa na IFC chini ya Mfumo wa Uendelevu. IFC pia ilisisitiza mara kwa mara kwamba hatari za CSA zilijumuishwa kimkataba katika mahitaji ya mteja ya kuripoti. Hata hivyo hakuna ushahidi kwamba IFC ilichukua hatua kusasisha ESAP na mahitaji ya mteja kuripoti ili kuimarisha maoni yake na kuhakikisha kuwa hatua mwafaka zinachukuliwa. IFC ilionekana kutoweza kumshawishi mteja wake kubadili maoni yake na IFC haikuchukua hatua zaidi kutatua kutokubaliana huku.

CAO iliarifiwa kwamba ugumu wa IFC kupata taarifa kuhusu shughuli za Bridge za utunzaji na ulinzi wa watoto ulipunguza uwezo wa IFC wa kusimamia na kushirikiana na kampuni kwa njia inayoleta manufaa. Mara kadhaa, IFC ilifahamisha CAO kwamba juhudi zake za kusimamia hatari zinazohusiana na CSA zilizuiliwa na msimamo wa mteja wake kuhusiana na masuala haya, hali iliyofanya majaribio ya IFC kushirikiana na Bridge "kutozalisha matunda." Katika jitihada za kuimarisha ufikiaji wa taarifa za Bridge kuhusu E&S (ikijumuisha kuhusu ushughulikiaji wa ulinzi wa watoto na utunzaji wa watoto), IFC iliingia katika makubaliano ya ziada ya usiri na

[134] WBG, Machi 20, 2020, Barua kutoka kwa Rais wa WBG kwa Katibu wa Hazina ya Marekani, barua iliyohaririwa inapatikana hapa: https://democrats-financialservices.house.gov/uploadedfiles/malpass_ltr_mnuchin_3202020.pdf.

mteja tarehe 23 Juni mwaka wa 2020[135] (Ona pia utangulizi katika sehemu ya kwanza). Hata hivyo, stakabadhi zilizopitiwa na CAO zinaonyesha kuwa masharti yanayoongoza kupata taarifa kutoka kwa Bridge kuhusu CSA yalisalia kuwa magumu kufuatia utekelezaji wa makubaliano haya. Bridge mara nyingi ilitoa taarifa kama hizo kwa IFC kupitia mfumo data mtandaoni uliodhibitiwa, hali iliyofanya kuwa vigumu kwa IFC kupata taarifa kikamilifu kwa sababu hawakuruhusiwa kupakua wala kuchapishwa.[136]

#### ***4.1.2.3. Usimamizi wa IFC kuanzia Julai hadi Desemba mwaka wa 2020***

Mwezi Agosti mwaka wa 2020, IFC ilitoa maoni yake kuhusu E&S kwa Bridge kutokana na kumsimamia mteja wao katika mwaka wa 2019. Stakabadhi hizi za usimamizi zilikuwa za kwanza kueleza wasiwasi wa IFC kama msimamizi kuhusu masuala ya kulinda na kutunza watoto, na zinaeleza kwa kina maelezo ambayo hayakurekodiwa awali kuhusu wajibu wa Bridge inavyoshughulikia utunzaji wa watoto katika shughuli zake zote. Kwa mfano, maoni yalibainisha kuwa, tangu mwaka wa 2009, Bridge ilikuwa imeweka sera na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake kuhusiana na ulinzi wa mtoto na kuzuia adhabu ya viboko.

Katika kushughulikia hali, IFC pia ilifahamishwa kwamba Bridge haikuwa imepokea malalamishi au malalamiko yoyote kuhusiana na CSA tangu visa vilivyoripotiwa hapo awali mwaka wa 2016. Hata hivyo, Bridge haikujibu msururu wa maswali kuhusiana na kulinda na kutunza watoto kwa kiwango cha maelezo yaliyohitajika. Bridge ilisema kuwa haikuwa na wajibu wa kutoa majibu kwa sababu mada ilikuwa nje ya upeo wa majukumu yake ya kuripoti.

Vivyo hivyo, IFC na Bridge zilijadili kuhusu kubadilisha kielelezo cha usimamizi ili kujumuisha kwa uwazi maelezo kuhusu hatari za ulinzi wa watoto na utunzaji wa watoto mwishoni mwa mwaka wa 2020. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO unaonyesha kuwa marekebisho haya hayakufanywa. Bridge iliendelea kubishana kuwa masuala ya utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto hayakuwa sehemu ya wajibu wake wa kuripoti hadi IFC ilipojiondoka kwenye mradi huo mwezi Machi mwaka wa 2022.

#### ***4.1.2.4. Usimamizi wa IFC mwaka wa 2021***

*Ukaguzi wa ndani wa IFC wa tathmini ya ulinzi wa watoto wa Bridge nchini Kenya*

Katika mwaka wa 2020, Bridge iliajiri kampuni ya ushauri ya Tunza Child Safeguarding ili kupitia sera na taratibu zake za utunzaji wa watoto na kutathmini utekelezaji wake. Ripoti iliyofuata, *Kuwaweka Wanafunzi Salama Nchini Kenya*: *Mapitio na Tathmini ya Ulinzi wa watoto nchini Kenya* ("Ripoti ya Tunza") ilikamilishwa Agosti mwaka wa 2020, ilitumwa kwa IFC, na kutolewa kwa umma Januari mwaka wa 2021.[137]

Ripoti ya Tunza ilikagua data kutoka vyanzo vya wasomi, vya serikali na mashirika yasiyo ya serikali (NGO) kuhusu unyanyasaji wa watoto kingono katika shule za msingi za serikali nchini Kenya pamoja na sera na taratibu zilizoandikwa za Bridge na unyanyasaji wote wa kingono uliorekodiwa na Bridge kutoka mwaka wa 2013 hadi mwaka wa 2019. Ripoti hiyo pia ilifanya uchunguzi wa kina wa visa 10 vya aina hii pamoja na mahojiano na wafanyakazi 15 wa Bridge na wafanyakazi wa serikali.[138] Ripoti hii ilifikia uwamuzi kuwa:

- Sera za utunzaji wa watoto za Bridge, utekelezaji wa wajibu wa utunzaji wa watoto, taratibu za utunzaji wa watoto na hatua za uwajibikaji za ulinzi wa watoto zilirandana zaidi na viwango vya kimataifa vya Kuwaweka Watoto Salama.

[135] Tazama Sehemu ya 1.6.1 ya ripoti hii.
[136] CAO ilikumbana na changamoto sawia katika juhudi za kupata stakabadhi.
[137] TUNZA Child Safeguarding, Agosti 2020, Kuwaweka Wanafunzi Salama Nchini Kenya. Inapatikana hapa: https://tunzachild.com/wp-content/uploads/2021/01/2020_Keeping-Pupils-Safe-in-Kenya.pdf.
[138] Ibid, uk. 34.

- Juhudi za ulinzi wa watoto za Bridge dhidi ya CSA za walimu zilitimiza au kupita viwango vilivyowekwa na sheria, kanuni na sera husika nchini Kenya.
- Visa vya CSA vilishuhudiwa zaidi katika shule za serikali kuliko za Bridge nchini Kenya.[139]

IFC ilifanya mapitio ya Ripoti ya Tunza, ambayo matokeo ya ripoti hii yalikuwa kwamba Bridge ilikuwa imeweka sera za ulinzi wa watoto na mfumo unaoendeshwa vizuri wa kuripoti mara kwa mara na kusajili visa. Hata hivyo, ndani ya IFC, kulikuwa na taswishi kuhusu ufanisi wa mbinu hiyo. Kulingana na uchunguzi wa CAO, wasiwasi huu haukushirikiwa na Bridge.

*Ukaguzi wa IFC wa utendakazi wa utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto wa Bridge inapoendesha shughuli zake nchini Kenya*

Mwezi wa Juni mwaka wa 2021, kwa mara ya pili, mtaalam wa masuala ya GBV aliitwa kushiriki katika kazi tofauti kama sehemu ya kikosi cha mradi wa IFC. Mtaalamu huyu wa E&S aliye na maarifa ya masuala ya CSA na GBV alifanya ukaguzi wa stakabadhi kwa lengo la kutathmini ikiwa kuna mapungufu yoyote makubwa ya kuridhia E&S yalikuwa yamesalia ambayo yangetinga juhudi za IFC kujiondoa kwa njia bora katika uwekezaji wa Bridge.

Ukaguzi wa stakabadhi za IFC ulijumuisha stakabadhi 15 za Bridge za kulinda na kutunza watoto zinazohusiana na shughuli zake nchini Kenya kuanzia Januari mwaka wa 2016 hadi Juni mwaka wa 2021. Hizi ndizo stakabadhi za pekee zilizotolewa na Bridge kupitia umfumo wake wa kutuma data zinazopatikana tu kwa muda. Yaliyomo, hitimisho na mapendekezo ya ukaguzi huu wa IFC—lakini hakuna uchanganuzi wa kimsingi—umejumuishwa katika ripoti ya ndani ya Juni mwaka wa 2021. Stakabadhi husika zilitolewa tu kwa wafanyakazi wawili wa E&S wa IFC waliohusika katika mchakato wa kujiondoa na kwa siku chache katikati ya mwaka wa 2021. -Uamuzi uliofikiwa na mapendekezo yalitolewa tena katika ripoti ya usimamizi ya IFC kati ya mwaka wa 2020 na 2021 mwezi Septemba 2021.

Ukaguzi huu wa stakabadhi za IFC ulijumuisha Ripoti ya Tunza. Ingawa kulikuwa na uvumi ndani ya IFC kuhusu mbinu ya ripoti hiyo, ukaguzi wa stakabadhi mwezi wa Juni ulionyesha kuwa ripoti ya Tunza ilikuwa ya kina, thabiti, iliyo na ushahidi wa kisayansi, na yenye mafunzo. Aidha, mapitio yalionyesha kuwa maoni ya mbinu ya Ripoti ya Tunza yalionekana kuzingatiwa vyema. Hata hivyo, CAO inabainisha kuwa, wakati wa mahojiano ya uchunguzi huu, wafanyakazi wa IFC walisema mara kwa mara kwamba: (1) waliona nia ya Bridge kufanya tathmini ya ulinzi wa watoto katika shule zake nchini Kenya kama hatua nzuri ya kuimarisha kipengele hiki cha utendakazi wao wa kijamii; na (2) kwa sababu Bridge ilifanya tathmini kwa kujitegemea, IFC haikuwa na mamlaka na uwezo wa kumshirikisha mteja kwa kiasi kikubwa katika masuala yanayohusiana na ripoti hii.

Kwa ujumla, muhtasari wa mapitio ya stakabadhi za Bridge yalionyesha kuendelea kuimarika kwa hatua za ulinzi wa watoto kuanzia mwaka wa 2016 na kufikia uamuzi kuwa Bridge ilikuwa inaridhia PSs zinazohusiana na GBV/SEAH. IFC ilibaini kuwa Bridge ilikuwa imepiga hatua na sasa ilikuwa ikifanya kazi kutekeleza hatua ambazo zilirandana na GIIP, lakini kwamba juhudi za mteja bado zilikuwa bado zinaendelea. Pia ilijumuisha mapendekezo saba, yaliyofupishwa hapo chini:

- Kutekeleza mfumo tofauti wa kutoa malalamishi na taratibu za kuyashughulikia kulingana na hatua za ukuaji wa mtoto
- Kufanya kazi za kisaikolojia katika jamii zinazowalenga wasichana na wavulana

[139] Ibid, uk. 29.

- Kupanua nyenzo za taarifa, elimu na mawasiliano kuhusu ulinzi wa watoto kwa kuzingatia umri wa mtoto
- Kuimarisha maoni na mifumo ya kuripoti inayozingatia umri wa mtoto
- Kupanua mafunzo ya ulinzi wa watoto kwa walimu na wafanyakazi katika mazingira ya shule
- Kuzingatia ukaguzi wa uendeshaji wa shughuli za ulinzi kwa watoto katika nchi zingine ambapo Bridge inaendesha shughuli zake.

Ripoti ya IFC kutokana na mapitio ya stakabadhi pia ilifikia uamuzi kuwa mradi uliridhia Viwango vya Utendakazi vinavyohusiana na GBV na SEAH. Ripoti hii na mapendekezo yalitolewa tena katika stakabadhi za usimamizi wa IFC kati ya mwaka wa 2020 na 2021 mwezi Septemba 2021.

#### ***4.1.2.5.*** **Januari hadi Machi mwaka wa 2022: Bridge inatoa taarifa kuhusu mpango wake wa kuwalinda watoto na IFC inajiondoa kwa mradi**

Mapema mwaka wa 2022, Bridge ilitoa kwa IFC ripoti ya taarifa na hatua zilizopigwa kuhusu shughuli za kuboresha usalama wa watoto, ikionyesha kama kila hatua iliyokuwa inaendelea, imekamilika, imesitishwa au kuondolewa kwenye mpango, na kutoa sababu za uamuzi wa Bridge kuchukua hatua hiyo. Ingawa mengi yalikuwa yamefanywa na kukamilika, mambo 12 yalikuwa yameondolewa.[140] Mambo 10 kwa yaliyoondolewa, maelezo yaliyotolewa ilikuwa matokeo chanya ya ripoti ya Tunza. Uchunguzi wa CAO haukupata ushahidi wowote kwamba IFC ilikagua mpango huo uliosasishwa au kama ilijua kuwa hatua zinazohusiana na kulinda na kutunza watoto zilikuwa zimeondolewa.

IFC iliarifiwa kuwa mteja wake alinuia kuendelea kufuata Viwango vya Utendakazi vinavyotumika baada ya IFC kuondoka. Hasa, Shule za NewGlobe, kampuni mama ya Bridge yenye makao yake makuu nchini Marekani, iliwasilisha dhamira yake ya kudumisha ESMS inayotumika katika Viwango vya Utendakazi vya IFC, pamoja na kamati ndogo ya Ubora, Afya na Usalama inayoongozwa na mkurugenzi anayejitegemea anayesimamia ubora wa kujifunza na afya, usalama, na ulinzi wa wanafunzi.

NGS ilitia saini barua ya kujiondoa kwa mradi huo tahere 3 Machi mwaka wa 2022. Wakati wa kujiondoa, IFC ilikuwa imekagua baadhi ya stakabadhi za Bridge za ulinzi wa watoto na kueleza kuridhishwa kwa jumla na shughuli za Bridge nchini Kenya. Wakati uo huo, idadi ya stakabadhi za utunzaji na ulinzi wa watoto zilizoitishwa na IFC kabla ya kuondoka kwake hazikuwa zimetolewa kwa IFC.

## 4.2. 3. Uchambuzi wa CAO na Matokeo yake

Sehemu hii inatoa uchambuzi wa CAO na matokeo yake kuhusu utendakazi wa IFC kwa kuzingatia wajibu wake wa kusimamia E&S yaliyotolewa kwa ufupi katika sehemu ya 2. Kwa kuzingatia hatua za IFC, CAO pia ilitathmini kuwepo kwa sheria husika ya kitaifa nchini Kenya na matendo mazuri ya tasnia ya kimataifa kuhusu CSA.

Kwa muhtasari, Wajibu wa IFC wa kusimamia E&S chini ya Sera ya Uendelevu uliihitaji: kufuatilia mara kwa mara kuridhia kwa Bridge kwa mahitaji ya PS yanayohusiana na hatari na athari za CSA zinazohusiana na mradi (aya ya 45, vitone vya 1 na 2); kufanya kazi na mteja ili kutambua na kushughulikia mabadiliko ya mradi ya hatari kwa mazingira na jamii (aya ya 25); kufanya kazi na mteja ili kurekebisha maeneo yoyote ambayo hayajaridhia (aya ya 45, kitone cha 3). Pia muhimu katika kesi hii, Sera ya Uendelevu pia iliitaka IFC kumtaka mteja wake

[140] Vitendo 12 vilivyowekwa alama kuwa vimeondolewa ni pamoja na uhakiki wa wafanyakazi wa shule kabla ya kuwaajiri, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa shule na wanafunzi, na kukuza ushirikiano ili kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango. Hasa, vipengee vinne vilivyohitaji hatua kuchukuliwa ni muhimu kwa mchakato wa kuajiri wafanyikazi, na vingine vinane ni mipango vinavyohusiana na mafunzo kwa wafanyikazi wa shule na wanafunzi.

kurekebisha Mfumo wake wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESMS) ili kushughulikia mabadiliko ya nyenzo katika vigezo vya hatari ya E&S vya mradi (aya ya 25) kwa namna inayorandana na Mfumo wa Uendelevu wa IFC. CAO imepata kuwa, wakati mzima wa uwekezaji, usimamizi wa IFC haukufuata kikamilifu majukumu haya.

Kwa kuzingatia sehemu iliyotangulia, uchanganuzi wa usimamizi wa IFC wa mradi uliopo hapo chini umegawanywa katika vipindi viwili—kabla na baada ya ziara ya CAO ya Februari mwaka wa 2020 kubaini visa vya unyanyasaji wa watoto kingono.

### 4.2.1. Uchanganuzi wa usimamizi wa IFC wa mradi: Tangu mwaka wa 2014 hadi Februari mwaka wa 2020

Kabla ya uchunguzi wa nyanjani wa CAO wa Februari mwaka wa 2020 wa Bridge-01, IFC ilishindwa kufuatilia mara kwa mara au kushughulikia kwa kiasi kikubwa hatari na athari za CSA na GBV. Mapungufu haya yaliendelea licha ya IFC kuarifiwa kuhusu matukio ya CSA mwaka wa 2013, 2016, na 2017, na licha ya utafiti wa UNICEF wa mwaka wa 2019 wa Ukatili Dhidi ya Watoto (VAC) unaoonesha kuenea kwa CSA na GBV dhidi ya watoto nchini Kenya.

Hasa, IFC ilitepetea kwa majukumu yake kwa: (1) kukosa kutathmini kubadilika kwa hali ya hatari katika jamii kutokana na visa vilivyoripotiwa vya CSA vilivyomtaka mteja wake kurekebisha ESMS yake ili kushughulikia hatari na athari za CSA (Sera ya Uendelevu); na (2) kutotathmini kikamilifu sera na mfumo wa mikakati ya Bridge ya kushughulikia CSA na hatari zinazoweza kutokea. (Sera ya Uendelevu, aya ya 45). Baada ya IFC kufahamu kuhusu visa mahususi, ilipaswa kumtaka mteja wake kutoa taarifa kuhusu mkakati kazi wa E&S ili kuweka hatua zinahitaji kuchukuliwa na mteja wake, ikijumuisha kusasisha ESMS yake ili kujumuisha uzuiaji na ushughulikiaji wa athari na hatari za CSA. Kwa kuongezea, IFC ilipaswa kubaini na kutekeleza mpango wa kawaida wa usimamizi wa kushughulikia hatari za CSA na kufanya kazi na Bridge ili kuhakikisha utekelezaji wa hatua zifuatazo zinazorandana na Viwango vya Utendakazi vya 1 na 4:

- Mfumo wa kutathmini na kusimamia CSA na hatari zinazoingiliana za GBV dhidi ya watoto (PS1, aya ya 5) na kufidia au kushughulikia athari zozote mbaya kwa wanafunzi (PS1, aya ya 14)
- Mchakato wa kutambua hatari za mradi zinazohusiana na CSA na GBV dhidi ya watoto unarandana na GIIP (PS1, aya ya 7)
- Hatua mbalimbali za kuzuia athari mbaya zinazohusiana na CSA zisiathiri vibaya watoto, wasichana, watoto wakubwa, au kikundi kingine chochote cha watu walio hatarini kuathiriwa na mradi (PS1, aya ya 12)
- Hatua mahususi za kuzuia na kudhibiti CSA na GBV zinazorandana na GIIP na kuzingatia hali na ukubwa wa hatari na athari za CSA zinazoingiliana na GBV katika maeneo haya (PS4, aya ya 5).

#### *4.2.1.1.* Katika mwaka wa 2016, jinsi IFC ilivyoshughulikia visa vya ziada vya CSA kwa shule ya Bridge haikutosha, na tathmini yake ya mfumo wa ulinzi na utunzaji wa watoto wa Bridge haikuwa na mashiko

IFC ilifahamu kuhusu visa vinne vya unyanyasaji wa watoto kingono nchini Kenya katika kipindi cha kati ya Septemba mwaka wa 2014 na Agosti mwaka wa 2016. Kufuatia hali hii, IFC iliomba Bridge itoe maelezo zaidi kuhusu visa vya CSA vilivyoripotiwa pamoja na sera zozote za Bridge kuhusu mada hizi. Stakabadhi za IFC hazionyeshi kuwa ilipokea na kukagua taarifa iliyoitishwa kutoka kwa mteja wake.

Wakati wa shughuli ya usimamizi wa IFC iliyoripotiwa ambayo haikurekodiwa wakati wa msimu wa jua mwaka wa 2016, IFC ilipokea taarifa kuhusu sera na taratibu za mteja wake za kushughulikia madai ya CSA. CAO iliarifiwa kwamba IFC ilipata taratibu hizi zilieleweka wazi na iliridhika kwamba masuala ya CSA yanayohusiana

na mradi yalikuwa yanashughulikiwa. Msingi wa IFC wa kuonyesha kuridhishwa na mfumo wa utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto wa Bridge na hatua za kushughulikia hali katika mwaka wa 2016 haukurekodiwa katika stakabadhi zozote za usimamizi.

CAO imegundua kuwa ushughulikiaji wa IFC kwa ufichuzi wa taarifa za CSA mwaka wa 2016 ulikuwa duni na kinyume na majukumu yake chini ya Sera ya Uendelevu (aya ya 7, 25 na 45) kwa kuzingatia:

- Ripoti zilionyesha kuwa hatari za CSA zilijitokeza na zilihitaji kushughulikiwa. Mapitio ya mfumo wa uzuiaji na kushughulikia CSA ulikuwa duni.
- Hakukuwa na stakabadhi za ukaguzi, ikiwa ni pamoja na uchanganuzi uliofanywa na IFC na kuifanya kufikia uamuzi kuwa masuala ya CSA yalikuwa yanashughulikiwa kwa njia ya kuridhisha na mteja wake na kwamba taratibu za mteja wake zilikubalika na kuridhisha.

**IFC haikufanya juhudi kubwa kutathmini na kubaini ikiwa uboreshaji wa juhudi za mteja wake ulihitajika ili kushughulikia hatari na athari za CSA kulingana na mahitaji chini ya PS1, PS4**

#### *4.2.1.2.* Katika mwaka wa 2017, IFC haikuchukua hatua za kutosha za usimamizi kwa kuzingatia malalamishi zaidi kutoka kwa wazazi na wanafunzi kuhusu GBV inayohusiana na mradi dhidi ya watoto.

Katika mwaka wa 2017, IFC iliarifiwa kuhusu wasiwasi unaoendelea kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika shule za Bridge. Wazazi na wanafunzi wa kike walitoa madai haya katika muktadha wa shughuli ya usimamizi inayohusiana na tathmini ya shule za Bridge nchini Kenya.

Kwa mjibu wa tathmini hiyo, IFC ilifanya ziara za usimamizi katika shule tisa za Bridge nchini Kenya kuanzia tarehe 18 hadi 20 Julai mwaka wa 2017. Wakati wa ziara hii, IFC iliarifiwa kwamba baadhi ya wazazi na wanafunzi wa kike wa Bridge walikuwa wametoa maoni yao kuhusu unyanyasaji wa kingono na GBV dhidi ya watoto wa kike wakati wa tathmini. Hata hivyo, CAO haikupata dalili kwamba IFC ilichukua hatua kupendekeza au kumtaka mteja wake kuchukua hatua za kushughulikia masuala haya.

Ikizingatiwa kwamba, kati ya mwaka wa 2013 na mwaka wa 2016, IFC ilikuwa tayari imearifiwa kuhusu visa vitano vya unyanyasaji wa watoto kingono vinavyohusiana na shule za Bridge, ilihitajika chini ya Sera ya Uendelevu kuhakikisha kuwa mpango wa mteja wa usimamizi wa E&S ulikuwa unashughulikia ushahidi unaojitokeza na malalamishi yanayoongezeka kuhusu visa na hatari za CSA.[141] Ingawa hakuna shule inayoweza kutarajiwa kuzuia visa vyote vya CSA na GBV inavyokumbana navyo, Kiwango cha Utendakazii cha 1 kinawahitaji wateja kutambua hatari kama hizo, kufanya juhudi kuzuia CSA, na kushughulikia kwa haraka visa vyoyote vinayotokea.[142] Hakuna ushahidi kwamba IFC ilichukua hatua kuthibitisha kwamba mteja wake alifanya hivyo.

CAO inaona ukweli uliothibitishwa kwamba kutoripoti vya kutosha kwa CSA dhidi ya watoto ni jambo la kawaida. IFC wakati wa usimamizi ilionekana kukubali kwamba visa vinne vya CSA vilivyoripotiwa na Bridge mwaka wa 2016 viliakisi jumla ya idadi ya wanafunzi wa Bridge waliopitia unyanyasaji wa kingono unaohusiana na mradi. Hata hivyo, kuripoti kwa kiwango cha chini kama jambo la kawaida kwa aina zote za CSA kunaonyesha kwamba idadi ya jumla ya waathirika ilikuwa na uwezekano kuwa kubwa zaidi. Haijalishi, ripoti moja ya CSA inapaswa kuwa imesababisha IFC kufuatilia, kutathmini, na kufuatilia visa vilivyoripotiwa na hatari zinazohusiana navyo.

[141] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, aya ya 16.
[142] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS1, aya za 5 na 14. Tazama pia IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya za 6 na 20. Vinapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/2023/ifc-performance-standards-2012-en.pdf, na hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/sp-english-2012.pdf.

CAO iligundua kuwa kushindwa kwa IFC kufanya hivyo baada ya kupokea ripoti tano kama hizo kati ya mwaka wa 2013 na mwaka wa 2016, pamoja na madai ya ziada katika mwaka wa 2017, kunawakilisha kushindwa wazi kufanya usimamizi chini ya majukumu yake ya E&S (Sera ya Uendelevu, 2012, aya za 7 na 45).

#### *4.2.1.3.* **Kati ya mwaka wa 2018 na mwaka wa 2019, IFC haikusimamia hatari za CSA na zile zinazoingiliano na GBV dhidi ya watoto**

Baada ya mwaka wa 2016, hakuna stakabadhi za kurekodi visa vya wanafunzi au vya usimamizi wa Bridge ziliripoti visa vyoyote vya unyanyasaji wa watoto kingono. Licha ya kufahamu kuhusu angalau visa vitano vya awali vya CSA, stakabadhi za usimamizi za IFC zilionyesha kuwa IFC haikuhoji mbona zilikosekana wala kuomba rekodi zozote za CSA kutoka kwa Bridge hadi baada ya ujumbe wa CAO wa Februari mwaka wa 2020 wakati ziara ya Bridge-01 ulipofichua visa viwili vya ziada vinavyohusisha watoto 15 walioathirika. Kwa kuongezea, IFC haikujadili hatari za CSA na GBV katika stakabadhi zake zozote za usimamizi wa mradi mwaka wa 2018 na mwaka wa 2019. Katika mwezi wa Januari mwaka wa 2020, IFC ilikubali kulikuwa na mafunzo kuhusu CSA na GBV yaliyoripotiwa katika stakabadhi za usimamizi za Bridge za mwaka wa 2018, lakini haikuuliza Bridge kwa nini iliamua kufichua kuhusu mafunzo haya kwa mara ya kwanza. Ni dhahiri kwamba hakuna masasisho ya ESAP au ESMS yaliyokubaliwa na IFC na mteja wake na kutolewa katika kipindi cha uwekezaji wa IFC yaliyojadili kuhusu ulinzi wa watoto, utunzaji wa watoto, hatari za CSA, hatari za GBV, au masuala/hatua zinazohusiana na mambo haya haswa kuhusiana na PS4 (Afya na Usalama wa Jamii).[143] Uchunguzi wa CAO unaonyesha kuwa IFC haikuwahi kuomba hatari za CSA au hatari zinazoingiliana za GBV kushughulikiwa katika stakabadhi hizi. CAO imegundua kuwa mapungufu haya ya usimamizi ni kinyume cha majukumu ya IFC ya usimamizi wa kijamii chini ya Sera ya Uendelevu (aya za 7, 25, na 45).

#### *4.2.1.4.* **Kuanzia mwaka wa 2017 hadi Februari mwaka wa 2020, IFC haikutathmini mfumo wa Bridge wa utunzaji na ulinzi wa watoto wala kuhakikisha kuwa mteja anachukua hatua zinazorandana na hali na ukubwa wa hatari za CSA**

Uchunguzi wa CAO unaonyesha kuwa IFC ilishindwa kufuatilia na kutathmini taarifa muhimu iliyotolewa na Bridge kupitia maandishi kuhusu sera, mikakati, mikataba na mafunzo ya utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto, kati ya mwaka wa 2017 na mwishoni mwa mwaka wa 2019. Kwa kutopitia stakabadhi hizi katika mwaka wa 2019, haileweki wazi jinsi IFC ilivyoweza kufikia uamuzi kuwa stakabadhi zilizoandikwa na Bridge kuhusu utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto zilikidhi Viwango vya Utendakazi na GIIP inayohusiana na hatari za GBV dhidi ya watoto. Hasa, usimamizi wa IFC haujaonyesha jinsi IFC ilivyobaini kuwa sera, taratibu, makubaliano na mafunzo ya utunzaji wa watoto na ulinzi wa watoto za mteja wake zinavyokidhi PS1 na 4 na GIIP husika. Hasa, hakuna ushahidi kwamba IFC ilimtaka mteja wake:

- Kushughulikia madhara yanayosababishwa na CSA
- Kuwasiliana kuhusu sera za CSA na wanafunzi, wazazi, machifu wa eneo, na watu wengine wasio wafanyakazi wao walio na wajibu wa utunzaji wa watoto
- Kutekeleza taratibu za wazi za utunzaji na ulinzi wa watoto kwa wafanyakazi na taratibu zozote za kuripoti kuhusu CSA kwa wazazi na watu wengine wasio wafanyakazi wao
- Kutoa mafunzo ya lazima ya uendeshaji wa uchunguzi wa CSA ndani ya kampuni
- Kutoa ulinzi wa kutosha kwa waathiriwa wa CSA ili kuwalinda dhidi ya kulipiza kisasi na kusumbuliwa tena kimawazo.

[143] Ibid. PS4 inavyotumika inatambuliwa katika uk. 3 wa stakabadhi hii. Bridge, Machi 22, 2019, Mfumo wa Kushughulikia Mazingira na Jamii (ESMS) (Matumizi ya PS4 yanatambuliwa katika ukurasa wa 6 wa stakabadhi hii).

Viwango vya Utendakazi vya IFC vilihitaji hatua za kupunguza CSA za Bridge zirandane na hali na ukubwa wa hatari na athari za CSA (PS4, aya ya 5). Kuhusiana na hitaji hili, CAO inabainisha kuwa serikali ya Kenya na washirika wake walichapisha data mwaka wa 2019 kutokana na ufuatiliaji wake wa uchunguzi wa mwaka wa 2010 wa Ukatili Dhidi ya Watoto nchini Kenya (VAC). Stakaadhi za usimamizi za IFC hazirejelei data hii wala utafiti uliotangulia wa mwaka wa 2010. Hata hivyo, data ya mwaka wa 2019 ilitoa ushahidi zaidi kwamba CSA nchini Kenya ziliendelea kuenea, huku wasichana wakiwa hatarini zaidi kukabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia.[144] Zaidi ya hayo, CAO inaona kwamba idadi ya shule zinazojumuishwa katika mradi huo kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2019 imesalia kuwa kubwa—hasa nchini Kenya—na kuongeza kiwango cha hatari kwa wanafunzi.

Kwa kuzingatia madhara makubwa, ambayo kwa kiasi kikubwa hayawezi kubadilishwaa, na yayonayoweza kushuhudiwa kizazi hadi kizazi na waathirika wa unyanyasaji wa watoto kingono, uwezekano mkubwa wa kuathirika kwa wanafunzi wa Bridge kutokana na hali zao za kijamii na kiuchumi, na kuwepo kwa hatari za CSA shuleni, na kiwango kikubwa cha shughuli za shule za Bridge katika jamii  kati ya mwaka wa 2014 na 2019, CAO inatambua kwamba hali na ukubwa wa uwezekano wa kutokea kwa hatari na athari za CSA ulikuwa mkubwa na uwezekano wa kuwa mbaya zaidi katika kipindi hiki.

### 4.2.2. Uchanganuzi wa usimamizi wa IFC wa mradi: Tangu mwaka wa 2020 hadi Februari mwaka wa 2022 IFC ilipojiondoa

Kuanzia Machi mwaka wa 2020, kulikuwa na uboreshaji mkubwa katika usimamizi wa IFC, lakini mapungufu katika usimamizi yaliendelea kuwepo.  Baada ya uchunguzi wa CAO wa Bridge-01 nyanjani mwezi wa Februari mwaka wa 2020 kuripoti matukio kadhaa ya madai ya CSA kwa IFC, IFC ilifanya ziara ya usimamizi nyanjani kwa shule za Bridge nchini Kenya iliyolenga hatari za kudhulumiwa kwa watoto na usalama wa watoto katika Bridge Academies. Kwa mara ya kwanza, IFC ilichunguza kwa makini na kuzingatia mbinu na uwezo wa Bridge kushughulikia CSA. Tathmini hii ilijumuisha uwezo wa mteja wa utunzaji na ulinzi wa watoto, mfumo wa usimamizi, taratibu (ikiwa ni pamoja na kushughulikia matukio, michakato ya uchunguzi wa ndani na taratibu za kuajiri zilizo salama kwa watoto), na mafunzo. IFC ilitambua na kuwasilisha maeneo muhimu ya kuboreshwa kwa Bridge na kupendekeza mipango ya kushughulikia pamoja maswala yanayohusu afya ya mtoto, usalama, na ushughulikiaji wa matukio ya CSA. Hata hivyo, juhudi za usimamizi za IFC ziliendelea kuwa na mapungufu ya mahitaji ya Sera ya Uendelevu kwa njia kadhaa kama inavyoonyeshwa hapo chini:

#### *4.2.2.1. Ufikiaji wa IFC kwa taarifa za mteja kuhusu ulinzi na usalama wa watoto ulikuwa muhimu kwa kazi yake ya usimamizi, lakini IFC ilishindwa kuhakikisha kwamba ilipokea na kukagua taarifa zote zinazohitajika*

Kufuatia kupokea taarifa za matukio ya ziada ya CSA mwezi wa Februari mwaka wa 2020, IFC ilifanya jitihada kushirikiana na Bridge ili kuboresha ulindaji na utunzaji wake wa watoto. Pendekezo la IFC la kukabiliana na hatari za CSA na GBV lilisisitiza haja ya uwazi kamili na kutoa taarifa kwa IFC kuhusu suala nyeti na lililo na changamoto la unyanyasaji wa watoto kingono. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO unaonyesha kuwa IFC ilisumbuka kupata taarifa za kutosha kuhusu mfumo wa kutunza na kulinda watoto wa Bridge. Ni wazi,  IFC ilishindwa kuhakikisha kwamba inapokea taarifa zote zinazohitajika. Taarifa zilizopokelewa na CAO zinaonyesha kuwa, kabla ya kuondoka, IFC haikupitia stakabadhi muhimu za kutekeleza wajibu wake wa usimamizi licha ya kuzitisha mara kadhaa. Hii ilijumuisha taarifa mpya kuhusu kuripoti visa, sera, mipango na miongozo ya kukabiliana na matukio ya CSA pamoja na maelezo mengine muhimu kwa usimamizi wa uwekezaji.

[144] UNICEF, 2019, Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Nchini Kenya (VACS), uk. 35. Unapatikana hapa: https://www.unicef.org/kenya/reports/The-2019-Violence-Against-Children-Survey.

IFC ilipokea taarifa kidogo na mara nyingi kwa kuchelewa kuhusu utekelezaji wa mteja wake wa mfumo wake wa kulinda na kutunza watoto. Bila maelezo haya, ilikuwa vigumu kwa IFC kufuatilia na kutathmini ufanisi wa mfumo wa CSA wa Bridge na kutoa mapendekezo yoyote kwa mteja kuuboresha ili ushughulikie vyema hatari za CSA na GBV kwa kuzingatia Viwango vya Utendakazi. Hata hivyo, licha ya mapungufu ya wazi na makubwa katika ukaguzi wa IFC wa utendakazi wa utunzaji na ulinzi wa watoto wa Bridge, IFC iliarifu Bridge mwezi Juni mwaka wa 2021 na tena mwezi wa Septemba mwaka wa 2021 kuwa upitiaji wake wa stakabadhi ulibainisha kuwa uwekezaji uliridhia wajibu wa Viwango vya Utendakazi vinavyohusiana na GBV na dhuluma na ukatili wa unyanyasaji wa kingono (SEAH). CAO imegundua kuwa uamuzi wa IFC kuhusu kuridhia kwa mteja wake kwa PS1 na 4 haukutokana na ukaguzi kamili na tathmini kamili ya stakabadhi muhimu zinazohitajika kufanya uamuzi kama huo.

Zaidi ya hayo, IFC ilishindwa kufuata hatua zilizopo ili kurekebisha mapungufu yake ya taarifa. Kwa mfano, Sera ya Uendelevu ya IFC inabainisha kuwa IFC inaweza kuchukua hatua za kurekebisha mambo iwapo mteja hataridhia hatua za kuripoti (aya ya 45) au IFC ingeweza kuchukulia Bridge hatua chini ya Makubaliano ya Nne ya Haki za Wawekezaji. Sera ya Uendelevu na stakabadhi za shughuli ziliruhusu IFC kuchukua hatua za kurekebisha hali pale ambapo Bridge ilikosa kuridhia kwa E&S kwa muda mrefu. [145]

### *4.2.2.2. IFC haikusimamia ushughulikiaji wa mteja wa hatari na athari zinazohusiana na CSA kwa kuzingatia mahitaji ya Viwango vya Utendakazi vya IFC vya 1 na 4*

IFC ilieleza Bridge Mwezi wa Septemba mwaka wa 2021 kuwa iliridhia Viwango vya Utendakazi vinavyohusiana na GBV na dhuluma na ukatili wa unyanyasaji wa kingono (SEAH). CAO inabainisha kuwa IFC ilifanya uamuzi huu ingawa hakuna rekodi zozote za usimamizi wa IFC zinazoonyesha mteja alishindwa kutekeleza mapendekezo yote ya kushughulikia hatari za CSA/GBV ambayo IFC ilipendekeza mwaka wa 2020-2021. Zaidi ya hayo, uamuzi wa IFC haukuungwa mkono na ukaguzi kamili wa stakabadhi muhimu ili kufanya uamuzi kuhusu kuridhia.

Uchunguzi wa CAO umepata kuwa stakabadhi za usimamizi za IFC zinaonyesha kuwa kuridhia kwa mradi na Viwango vya Utendakazi vinavyohusiana na GBV na ukatili na unyanyasaji wa kingono haukutokana na tathmini ya stakabadhi iliofuata utaratibu maalum wala kwenda nyanjani. IFC haikuipatia CAO uchanganuzi wowote ulioandikwa ambao ungeunga mkono uamuzi wao kwamba mradi huo uliridhia PS za IFC kuhusiana na kushughulikia hatari na athari za CSA. CAO haikupata ushahidi kwamba IFC ilizingatia GIIP au sheria husika za kitaifa za Kenya katika mapitio yake ya mfumo wa CSA ambao Bridge ilikuwa imeunda wakati huo.

CAO inabaini kwamba IFC ilikuwa na ufahamu mdogo kuhusu mfumo huu wakati wa usimamizi wa mradi. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO unaonyesha kuwa kati ya mwaka wa 2020 na Machi mwaka wa 2022 IFC ilikuwa imepokea dalili za kutosha kuhusu kuendelea kwa hatari na athari za CSA lakini haikuchukua hatua za kutosha ili kuhakikisha na kuthibitisha kuwa mbinu ya Bridge ya utunzaji na ulinzi wa watoto iliendana na GIIP na hivyo kuridhia PS husika kama inavyotakiwa chini ya Sera ya Uendelevu (aya za 7 na 45).

IFC iliarifu CAO kwamba uamuzi wake kwamba Bridge ilikuwa imeridhia haukutokana na tathmini ya mfumo wa mteja kwa kuzingatia matendo mazuri ya kimataifa kwa sababu mbili. Mwanzo, IFC ilizingatia GIIP inayohusiana na CSA na GBV na inayotumika kwa sekta binafsi ya elimu ya K–12 katika mazingira ya kipato cha chini kama "kiwango muhimu" ambacho hakikuhitajika kwa "ridhaa msingi" na PS1 na 4. Pili, tathmini ya kina zaidi ya IFC ya utendakazi wa utunzaji na ulinzi wa watoto wa Bridge ulifanyika baada ya Juni mwaka wa 2021, wakati ambapo lengo kuu la IFC lilikuwa kuondoka kwa njia njema kushughulikia uhusiano wake mgumu na Bridge. Kwa hivyo IFC iliamua kuwa kuendeleza uboreshaji zaidi wa utendakazi wa E&S wa Bridge kungehitaji kazi

---

[145] IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya ya 45. Inapatikana hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/sp-english-2012.pdf.

kubwa kutoka kwa IFC na kuaminiwa kwingi na mteja kuliko hali ilivyokuwa. Baada ya Septemba mwaka wa 2021, IFC haikutoa mapendekezo zaidi ya kuboresha hali kwa Bridge.

CAO imepata kuwa mbinu ya IFC ya kukagua stakabadhi za utunzaji na ulinzi wa watoto wa Bridge ilikuwa kinyume na wajibu wake wa E&S chini ya Mfumo Endelevu (aya ya 7).[146] Hasa, IFC haikutathmini na kuthibitisha kwamba:[147]

- Utendakazi wa utunzaji na ulinzi wa watoto wa Bridge (pamoja na mfumo wake) uliridhia GIIP inayohusiana na hatari za CSA na GBV za mradi.[148]
- Shughuli za Bridge ziliridhia sheria za kitaifa zinazohusiana na hatari za mradi za GBV na CSA.[149]

#### *4.2.2.3. IFC ilishindwa kumsimamia mteja vya kutosha kushughulikia athari za CSA zilizojitokeza wakati wa mradi*

Mapungufu ya usimamizi wa IFC pia yalionekana kupitia kushindwa kufanya kazi na mteja ili kushughulikia kikamilifu athari zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi. Kwa mfano, Kiwango cha Utendakazi cha 1 kinahitaji mteja kulipa fidia kwa athari zilizobaki kwa jamii zilizoathiriwa — katika hali hii, waathirika wa CSA na GBV. Hasa, PS1 inawataka wateja "kufidia/kulipia" athari kwa mazingira na jamii (E&S) ambazo mradi hauwezi kuepuka au kupunguza.[150] IFC pia inalazimika kumsimamia mteja ili kuhakikisha kwamba anaridhia mahitaji haya.[151] Kama ilivyoelezwa hapo awali, CAO iliarifiwa kwamba wafanyakazi wa mradi wa IFC walikosa kupata rekodi za Bridge zinazonakili matukio ya CSA baada ya mwaka wa 2016, na kwa upande wake hii ilitinga uwezo wake wa kufuatilia matukio haya na maslahi ya waathirika.[152] Wakati uo huo, CAO inabaini kuwa ingawa mwezi Machi mwaka wa 2020 IFC ilijaribu kukagua taratibu za mteja wake kuhusiana na matukio yaliyoripotiwa na mafunzo kwa wafanyikazi, IFC haikuuliza haswa juu ya hali ya watoto waathirika na CSA iliyojulikana kwa IFC wakati huo. [153]

Kushindwa huku kwa usimamizi kulitokea licha ya ukweli kwamba IFC ilikuwa na sababu ya kushuku kwamba ushughulikiaji wa Bridge wa waathirika unaweza kuwa usio wakutosha.[154] Wakati wa ziara yake ya usimamizi mwezi Machi 2020 nyanjani, IFC ilionyesha wasiwasi kwamba gharama za matibabu zinazohusiana na CSA zinazohusiana na mradi zililipwa na familia za waathirika na wala sio Bridge. Uchunguzi wa CAO ulibainisha kuwa IFC haikufuatilia kama hali hii ilibadilika kati ya mwaka wa 2020 na mwezi wa Machi mwaka wa 2022.

CAO imepata kwamba kutofuata kwa vitendo vilivyoelezwa hapo juu ni kutoridhia wajibu wa IFC wa kusimamia utambuaji wa mteja wake wa athari mbaya zilizosalia za CSA zinazoingiliana na GBV na kufidia athari zozote kama hizo, kama inavyotakiwa na PS1.[155]

---

[146] IFC, 2012, Viwango vya Utendakazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii, PS4, aya ya 5 huhitaji mteja kutathmini hatari na athari kwa afya na usalama wa Jamii Zilizoathiriwa wakati mzima wa mradi na kuanzisha hatua za kuzizuia na kuzidhibiti kulingana na mazoea mazuri ya tasnia ya kimataifa (GIIP), PS1 aya ya 5 inahitaji wateja kuridhia sheria za kitaifa zinazotumika.
[147] IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya ya 7.
[148] PS1, 2012, aya ya 7; na PS4, 2012, aya ya 5.
[149] PS1, 2012, aya ya 6.
[150] PS1, 2012, malengo na aya ya 14.
[151] IFC, 2012, Sera ya Uendelevu wa Mazingira na Jamii, aya ya 7.
[152] Hata hivyo, mwanzoni mwa mwaka wa 2020, IFC ilipokea rekodi kutoka kwa Bridge iliyoripotiwa kunasa kiasi kikubwa cha visa (70) vya CSA lakini haikuchukua hatua zozote za kumfuatilia mteja.
[153] Tazama sehemu ya Madhara Husika ya ripoti hii.
[154] CAO inabainisha zaidi kwamba IFC iliarifu Bridge mara kwa mara kwamba, kwa kuzingatia ukubwa wa shughuli za Bridge kati ya mwaka wa 2020 na mwaka 2022, ikihusisha mamia ya shule nchini Kenya pekee, ukosefu wa rekodi za mteja zinazonasa matukio ya CSA baada ya mwaka wa 2016 ilikuwa dhahiri.
[155] PS1, 2012, malengo na aya ya 14.

# 5. Sababu Kuu za Kutoridhia

CAO inazingatia zifuatazo kuwa sababu za kutoridhia zilizobainishwa katika uchunguzi huu. Kushindwa kwa IFC kutathmini athari kwa mazingira na jamii (ESDD) kabla ya uwekezaji, hii ni sababu ya kutoridhia wakati wa ESDD na sababu ya msingi ya kutofuata sheria na kupelekea madhara wakati wa usimamizi wa mradi.

## 5.1. Kushindwa kwa IFC kutathmini athari kwa mazingira na jamii

Mchakato wa ESDD wa IFC haukutosha. Ulizingatia zaidi ukaguzi wa stakabadhi chache zilizotolewa na mteja na mahojiano mawili na wasimamizi wakuu wa Bridge badala ya kufanya ukaguzi unaofuata utaratibu maalum kuhusu kiwango na ubora wa tathmini ya hatari na athari za mteja. Kutegemea kupita kiasi taarifa za mteja, pamoja na uamuzi wa IFC wa kutofanya ziara nyanjani wakati wa utafiti wa kabla ya mradi—licha ya kuwepo kwa shule nyingi za Bridge nchini Kenya—kulichangia kupuuza kiasi cha hatari za uwekezaji kwa jamii, ikiwa ni pamoja na hatari kubwa ya unyanyasaji wa watoto kingono. Zaidi ya hayo, IFC haikuuliza mteja wake kutayarisha au kutoa tathmini ya athari kwa mazingira na jamii (E&S) ambazo zingerandana na hatari na athari zinazoweza kutokea, hali ambayo ingebainisha hatari ya unyanyasaji wa watoto kingono. Mwanzo huu ulio na mapungufu ukawa, kwa upande wake, sababu kuu iliyofanya majaribio ya baadaye ya kufanya uwekezaji kuridhia E&S kutoa changamoto kubwa kwa IFC. Hakukuwa na uchambuzi wa uwezo wa mteja kushughulikia hatari hizi na hakuna ujumuishaji wa hatua zozote za kukabiliana nazo au za kuzipunguza katika Mpango wa Utekelezaji wa Mazingira na Jamii uliokubalika kati ya IFC na mteja wake. Mapungufu haya yalidhoofisha uwezo wa IFC wa kumsimamia mteja wake vyema na pia inaweza kuwa ilichangia mteja kusisitiza kwamba CSA na GBV hazikushughulikiwa na Mfumo wa Uendelevu wa IFC.

## 5.2. Ukosefu wa Wataalamu wa Usimamizi wa Hatari za Kijamii wakati wa Usimamizi

Kikosi cha IFC cha kushughulikia mradi kilikosa wataalamu muhimu wa kiufundi wa kufuatilia CSA na hatari zinazoingiliana za GBV mara kwa mara na vya kutosha. Kuzingatia kauli za IFC, wataalamu wawili wenye maarifa ya GBV (mmoja wao pia alikuwa na maarifa ya CSA) walifanya kazi kama sehemu ya kikosi cha uwekezaji kwa kipindi kifupi, kwa kazi tofauti, mapema mwaka wa 2020 na Juni mwaka wa 2021, mtawalia. Kushiriki kwao katika kikosi kulitokea takriban miaka minne baada ya Bridge kuripoti matukio manne ya unyanyasaji wa watoto kingono kwa IFC mwaka wa 2016, na miezi 16 baada ya ziara ya CAO nyanjani kufanya uchunguzi wa Bridge-01 ulipobaini matukio 15 ya visa vilivyohusisha watoto 15. Ukosefu wa wataalamu wa usimamizi wa hatari za kijamii wakati mwingi wa uwekezaji ulitinga uwezo wa IFC kutambua na kufuatilia ipasavyo hatari na malalamishi kuhusu hatari za CSA na GBV, na kufuatilia hatua za kuzuia CSA zilizopendekezwa na IFC kwa Bridge.

## 5.3. Ugumu wa Kupata Taarifa

CAO iliarifiwa mara kadhaa wakati wa uchunguzi wake kwamba ugumu wa IFC kupata taarifa kuhusu shughuli za Bridge za utunzaji na ulinzi wa watoto ulipunguza uwezo wa IFC wa kumsimamia mteja wake ipasavyo. Katika matukio kadhaa, IFC ilipokea taarifa iliyoitisha kwa kuchelewa kuliko ilivyotarajiwa, na wakati mwingine haikupokea taarifa iliyoitisha.[156] Stakabadhi nyingi za E&S, zikiwemo hatari za CSA na GBV, zilitolewa tu kupitia

[156] Tazama Sehemu ya 1.6.1 ya ripoti hii.

mtindo salama wa data za kielektroniki unaozuia watumiaji kupakua au kuchapisha stakabadhi. Upatikanaji wa data za kielektroniki wakati mwingine zilipatikana kwa muda tu kwa watumiaji mahususi. Majina ya watumiaji na tarehe na muda uliotumiwa kwa stakabadhi ulifuatiliwa na kukaguliwa. Ingawa baadhi ya mbinu hizi zinajumuisha mazoezi ya kawaida ya kibiashara, katika hali hii, iliathiri uwezo wa IFC wa kupata habari muhimu inayohitajika kwa ufanisi na kufanya kukagua na kuchambua stakabadhi za mteja kuwa kazi ngumu.[157]

## 5.4. Ukosefu wa Maarifa kuhusu Mienendo Mipana ya Kitaasisi

Mradi ulipoelekea katika mwaka wake wa pili wa utekelezaji, maswali kuhusu jinsi ya kushughulikia GBV na SEAH yalikuwa yanaibuliwa ndani ya Kundi pana la Benki ya Dunia. Hata hivyo, inaonekana kwamba IFC haikuzingatia "hatari" iliyotolewa na uamuzi wa Rais wa WBG Jim Yong Kim mwaka wa 2016 wa kuzindua kikosi kazi cha GBV/SEAH na kukagua hatari na athari zinazoweza kutokea katika Benki ya Dunia. Katika mwaka wa 2017, Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Unyanyasaji wa Kijinsia kilitoa matokeo ambayo yalionyesha shule kama maeneo ambayo watoto wako hatarini kunyanyaswa kingono. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO haupati ushahidi wowote kwamba IFC ilizingatia jinsi maamuzi haya yanavyoweza kuwa muhimu kwa miradi yake yenyewe. Sababu za ukosefu huu wa maarifa hazieleweki.

## 5.5. Ukosefu wa Uwazi kuhusu Kujiondoa kwa mradi

Uchunguzi wa CAO umegundua kuwa ukosefu wa kuelewa kuhusu mahitaji ya kufuata E&S kwa kikosi cha mradi cha IFC wakati wa kujiondoa kwa mradi huu inaweza kuwa iliathiri jinsi IFC ilivyoendesha usimamizi wake wa Bridge. IFC iliachana na uwekezaji mwezi Machi mwaka wa 2022 bila kupata uhakikisho kutoka kwa Bridge au kampuni yake kuu kwamba, baada ya kuondoka, Bridge itatii mahitaji ya E&S ya IFC yanayotumika kwa hatari na athari za CSA. Hata hivyo, wakati wa kuondoka, Bridge iliahidi kutumia Viwango vya Utendakazi vya IFC kama "zana" na kudumisha mfumo wa usimamizi wa E&S kwa kuzingatia PS inayotumika. Hakuna ahadi mahususi iliyofanywa kuhusu kushughulikia hatari za GBV na CSA.

[157] CAO ilikumbana na changamoto sawia katika juhudi za kupata stakabadhi.

# 6. Madhara

Matokeo ya uchunguzi wa ridhaa huamua iwapo IFC imeridhia sera zake za E&S na kama kuna madhara yanayohusiana na kutoridhia kwa IFC (Sera ya CAO, aya ya 112). Sehemu hii inachanganua na kuangazia madhara yanayohusiana na kutoridhia, pamoja na hali zinazofanya madhara kuwa na uwezekano wa kutokea katika siku zijazo, yanayohusiana na kutoridhia kwa IFC wakati wa utafiti wake wa kabla ya mradi na wakati wa kusimamia Bridge, kama ilivyobainishwa hapo juu.

Kwa muhtasari, kufikia wakati wa kuondoka kwa IFC mwezi wa Machi mwaka wa 2022, IFC ilikuwa na habari kuhusu matukio mengi ya unyanyasaji wa watoto kingono, ikiwa na waathirika 23. CAO inabainisha kuwa, katika visa vyote isipokuwa kimoja, unyanyasaji huo ulitokea baada ya IFC kuwekeza katika Bridge na wakati wa kipindi cha usimamizi wakati ambapo IFC ilipaswa kufanya kazi na mteja ili kukuza na kutekeleza mikakati ya kutathmini na kudhibiti hatari na athari zinazohusiana na usalama na ulinzi wa watoto, ikiwa ni pamoja na CSA.

Mbali na waathirika 23 wanaojulikana, kuanzia mwaka wa 2014 hadi mwaka wa 2021, IFC ilifahamu kuhusu visa zaidi vya CSA. Madhara ya CSA kwa mwili na ya kisaikolojia yanafahamika vizuri.

## 6.1. Mambo Yanayohusiana na Madhara

Sera ya CAO inafafanua "madhara" kama "athari yoyote mbaya ya kimazingira na kijamii kwa watu au mazingira inayotokana moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na Mradi au Mradi Mdogo. Madhara yanaweza kuwa halisi au yanayoweza kutokea katika siku zijazo" (Sera ya CAO, faharasa). Madhara yaliozingatiwa katika uchunguzi huu wa ridhaa yanahusu hasa unyanyasaji wa watoto kingono (CSA), ambao uko chini ya unyanyasaji wa kijinsia (GBV) dhidi ya watoto. Katika kazi ya semina “Wazi ila Fiche: Uchambuzi wa Kitakwimu wa Ukatili Dhidi ya Watoto,” UNICEF inatoa maelezo ya kina kuhusu madhara yanayosababishwa na unyanyasaji wa watoto kingono:

> “Matukio ya unyanyasaji wa kingono utotoni hudhuru vipengele vyote vya ukuaji: kimwili, kisaikolojia na kijamii.” Mbali na majeraha kwa mwili yanayoweza kukutokea, kuambukizwa virusi vya ukimwi (HIV) na magonjwa mengine ya zinaa, pamoja na ujauzito wa mapema, pia vinaweza kutokea. Madhara mengine kwa mwili ya unyanyasaji wa kingono ni pamoja na aina mbalimbali za tabia za kujidhuru, kama vile mienendo mibaya ya ulaji, kama vile bulimia na anorexia. Watoto ambao wamenyanyaswa pia wana uwezekano mkubwa wa kujaribu kujiua; kadiri unyanyasaji unavyozidi kuwa mbaya, ndivyo hatari zinavyoongezeka.
>
> Watafiti wamegundua mara kwa mara kuwa unyanyasaji wa watoto kingono husishwa na athari nyingi za afya ya akili, pamoja na dalili za msongo wa mawazo na shida ya hofu. Wasiwasi na ndoto mbaya pia hushuhudiwa kwa watoto wadogo ambao wamepitia ukatili kama huu. Athari za kisaikolojia za unyanyasaji wa kingono zinaweza kuwa mbaya kutokana na aibu, usiri na unyanyapaa unaoandamana nao, huku waathiriwa watoto mara nyingi wakilazimika kutafuta njia za kukabiliana na hali hiyo bila kumwambia yeyote. Uwezekano wa kupata athari mbaya za afya ya akili inaonekana kuongezeka kutegemea umaratokezi na kiwango ambacho watoto huathiriwa na unyanyasaji wa kingono na kuwa na madhara ya kudumu.
>
> Mbali na madhara kwa mwili na madhara ya kisaikolojia, matukio ya utotoni ya unyanyasaji wa kingono husababisha madhara makubwa katika jamii. Hasa wanapolawitiwa na mlezi au mtu wanayemwamini, watoto wanaweza kuwa na mahusiano ya kutohisi salama au wa kutisha na wengine wanaweza

kukabiliwa na ugumu wa kujenga na kudumisha uhusiano baadaye maishani. Watoto ambao wamefanyiwa unyanyasaji wa kingono wanaweza kupata viwango vya juu vya woga na kukerwa na kuhisi kutishiwa au uadui kutoka kwa watu wengine."[158]

Kwa kuzingatia Sera ya CAO, "ushahidi wa kutosha na mwafaka unahitajika ili kuwa msingi bora wa matokeo ya CAO kuridhia na kufikia uamuzi" (Sera ya CAO, aya ya 117). Kuhusiana na kesi hii, CAO imeona kuwa kulikuwa na madhara pale ambapo kuna ushahidi wa kutosha na unaohitajika ili kufikia uamuzi kuwa CSA ilitokea kutokana na mradi huu moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. CAO pia ilibainisha taarifa zilizoripotiwa kuashiria visa zaidi vya unyanyasaji wa watoto kingono ambavyo vinaweza kuwa vilisababisha madhara.[159]

## 6.2. Matukio ya Kudhuriwa

IFC na CAO kwa pamoja wanafahamu kuhusu matukio mengi yanayohusisha waathirika 23 watoto. Lifuatayo ni jedwali linalotoa muhtasari wa matukio yanayojulikana, watoto walioathirika na wanaodaiwa kuyatekeleza.

### Matukio ya CSA yanayojulikana na IFC na CAO

| Tarehe | Idadi ya Tukio/Matukio | Tarehe na Njia Ambazo IFC Ilifahamu Kuhusu Matukio | Idadi ya Watoto (waathirika) na Maelezo kuhusu CSA (iwapo yanapatikana) – Jumla ya 23 | Anayedaiwa kuyatekeleza |
|---|---|---|---|---|
| Januari 2013<br>(Kabla ya Uwekezaji wa IFC) | 1 (moja) | -Desemba 2013<br>-Shughuli za tathmini ya IFC | **Mwanafunzi 1 (mmoja) wa Bridge** | mwalimu 1 (mmoja) wa Bridge<br>Mwalimu huyo alipatikana na hatia mwaka wa 2014 na kuachiliwa huru mwaka wa 2015 na mahakama ya rufaa.[160] |
| a) Oktoba 8, 2014<br>b) Januari 21, 2015<br>c) Februari 19, 2015<br>d) Mei 16, 2016 | 1 (moja)<br>1 (moja)<br>1 (moja)<br>1 (moja) | -Aprili 2016: Shughuli za usimamizi wa IFC | **Wanafunzi 4 (wanne) wa Bridge**<br>(a) Tukio 1 (moja) la unyanyasaji wa kingono nje ya shule<br>(b) Uhusiano 1 (mmoja) wa kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwalimu<br>(c) Tukio 1 (moja) la unyanyasaji wa kingono na jamaa wa mlezi wa shule wakati wa kwenda shuleni<br>(d) Dai 1 (moja) la unyanyasaji wa kingono na mwalimu | -Walimu 2 (wawili) wa Bridge<br>- Wanafunzi kutoka shule nyingine (idadi isiyojulikana)<br>-Jamaa 1 (mmoja) wa mlezi wa shule |

[158] Tazama, UNICEF, 2014, Wazi ila Fiche: Uchambuzi wa Takwimu za Ukatili Dhidi ya Watoto, uk. 62. ("Matukio ya unyanyasaji wa kingono utotoni hudhuru vipengele vyote vya ukuaji: kimwili, kisaikolojia na kijamii."); na IFC, EBRD, CDC, na Maendeleo ya Jamii Moja kwa Moja (2020), *Kushughulikia Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (GBVH) katika Sekta ya Elimu* uk.1. (unaonyesha kwamba "GBVH ni suala nyeti na la kimfumo katika sekta ya elimu" ambalo hutokea katika mazingira yote ya elimu na lina "madhara ya kudumu kwa uwezo wa kujifunza, kwa afya, ustawi na kupata ajira kwa mwanafunzi," pamoja na athari zinazoweza kutofautiana kijinsia kwa wavulana na wasichana). Unapatikana hapa: https://data.unicef.org/resources/hidden-in-plain-sight-a-statistical-analysis-of-violence-against-children/#:~:text=Publications-,Hidden%20in%20Plain%20Sight%3A%20A%20statistical%20analysis%20of%20violence%20against,and%20data%20from%20190%20countries na hapa: https://www.ifc.org/content/dam/ifc/doc/mgrt/gpn-addressinggbvh-july2020.pdf.

[159] Mchakato wa kuridhia wa CAO hauhusiki na ushahidi, sio wa kimahakama, na "haujaundwa wala kukusudiwa kutumiwa katika kesi mahakamani au kutoa hukumu au kwa makusudi ya kuhusisha uhalifu kisheria au kuwajibikia hali." Sera ya CAO katika ibara ya 9 na 117. Inapatikana hapa https://www.cao-ombudsman.org/sites/default/files/documents/CAO%20Policy/ifc-miga-independent-accountability-mechanism-cao-policy.pdf.

[160] Kutokana na kiwango tofauti, na cha chini, kinachotumiwa na CAO kuliko ilivyo kawaida katika kesi za uhalifu, matokeo ya vikao hivyo hayaonyeshi ushahidi wa kutosha kuunga mkono matokeo ya CAO kuhusiana na tukio hili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) Juni hadi Agosti mwaka wa 2019<br>(b) 2016-2017 | Haijulikani | c) Februari 19, 2020 -Taarifa za CAO kwa IFC | **Wanafunzi 15 (kumi na tano)**<br>(a) Wanafunzi 2 (wawili) wa kike<br>(b) Wanafunzi 13 (kumi na tatu): Wasichana 11 na wavulana 2 | (a) Mwalimu 1 (mmoja) wa Bridge. Mwalimu aliachishwa kazi kutokana na hali hii<br>(b) Mwalimu 1 (mmoja) wa Bridge |
| April 30, 2019, or au mapema (tarehe kamili haijulikani) | Haijulikani | - Machi 12, 2020 Shughuli za usimamizi wa IFC | **Wanafunzi 3 (watatu) wa Bridge** | Mwalimu 1 (mmoja) wa Bridge |

Aidha, CAO inabainisha kuwa kuna taarifa zinazoonyesha kuwa matukio zaidi ya kudhuriwa yanaweza kuwa yalitokea. Taarifa hii ni pamoja na:

- Idadi isiyojulikana ya ripoti zilizowasilishwa kwa IFC wakati wa kuunda ripoti iliyoidhinishwa kama sehemu ya shughuli zake za usimamizi Julai mwaka wa 2017. Hata hivyo, IFC wala CAO hazina maelezo ya kina kuhusu ripoti hizi na kwa hivyo CAO inazingatia kwamba hakuna taarifa ya kutosha kubainisha kama kuna madhara yanayohusiana nazo.

- Idadi inayoweza kuwa kubwa ya ripoti za CSA (70) ambazo zilishirikiwa na IFC Machi mwaka wa 2020. Hata hivyo, IFC wala CAO hazina maelezo ya kina kuhusu ripoti hizi na kwa hivyo CAO inazingatia kwamba hakuna taarifa ya kutosha kubainisha kama kuna madhara yanayohusiana nazo.

# 7. Mapendekezo ya CAO kwa IFC

Kwa kuzingatia Sera ya CAO, Menejimenti ya IFC itaandaa Ripoti ya Menejimenti ambayo inaweza kujumuisha Mpango Kazi wa Menejimenti (MAP) ili kushughulikia matokeo yanayopatikana katika ripoti hii. Kwa kufanya hivyo, CAO inapendekeza kwamba IFC izingatie hatua zifuatazo kwa kuzingatia mradi na hatua za kitaasisi.[161]

## 7.1. Mapendekezo Kutegemea Mradi Mahususi

Kwa kuzingatia mradi, mapendekezo ya CAO yanalenga kuwezesha kutoa suluhisho kwa waathirika wa unyanyasaji wa watoto kingono na familia zao na kusaidia kushughulikia hatari zozote zinazoweza kuendelea kutokea.

**a. Kushughulikia waathirika wa CSA zinazohusiana na mradi.** IFC inapaswa kushirikiana na Bridge kuanzisha kituo cha Dharura cha Kulinda Watoto (ECPR) ili kusaidia mchakato wa kuwezesha waathirika na familia zao kuweza kushughulikiwa. CAO inabainisha kuwa Benki ya Dunia ilisaidia kukuza ECPR chini ya Mpango Kazi wa Menejimenti (MAP) uliotokana na Jopo la Kufanya Uchunguzi katika Sekta ya Uchukuzi nchini Uganda.[162] ECPR inapaswa, angalau, kutoa yafuatayo kwa waathirika wa mradi unaofadhiliwa na IFC:

- Ushauri wa mabadiliko ya kijinsia kwa waathirika na familia zao
- Msaada wa huduma za afya, ikiwa ni pamoja na huduma za afya ya sehemu nyeti na huduma za afya ya uzazi na matibabu ya magonjwa ya zinaa
- Msaada wa ujumuishaji wa jamii ili kuwezesha waathirika kuendelea na elimu au juhudi za waathirika kutafuta ajira nzuri pale ambapo CSA imetinga shughuli kama hizo
- Ufadhili na kuelekezwa kwa huduma za kisheria kwa familia zinazotafuta sheria kuchukuliwa dhidi ya wahalifu
- Mfumo unaowezesha waathirika kujitokeza, kujitambulisha ikiwa wanataka, na kukubali hatua yoyote ya kurekebisha mambo ambayo itatolewa kwao
- Fidia ya kifedha, kwa msingi wa 'bila kosa,' inavyofaa.

Hatua za kukabiliana na hali zinapaswa kulinda usiri wa walalamishi na kuwalinda walalamishi na familia zao dhidi ya hatari yoyote ya vitisho au kulipiza kisasi. Katika kuendeleza ECPR yake, CAO inahimiza sana IFC kuzingatia kushirikiana na mashirika yasiyo ya serikali ambayo yana maarifa mwafaka kuhusu eneo, uwezo na yanayoaminiwa na jamii husika ili kufanikisha utekelezaji wa mchakato wa kufidiwa.

**b. Kuimarisha ushughulikiaji wa jamii wa CSA na GBV dhidi ya watoto katika jamii ambazo mradi unatekelezwa.** IFC inapaswa kushirikiana na Bridge ili kusaidia kuzuia madhara ya baadaye yanayohusiana

[161] Chini ya Sera ya CAO: *"Ambapo CAO inapata kutoridhia na Madhara yanayohusiana na kutoridhia, CAO* ***inatoa mapendekezo kwa IFC/MIGA kuzingatia wakati wa kuunda Mpango Kazi wa Menejimenti*** *(MAP).* Mapendekezo yanaweza kuhusiana na **kushughulikia kutoridhia kwa** kiwango cha **Mradi**- … na Madhara yanayohusiana na kutoridhia, na/au **hatua zinazohitaji kuchukuliwa ili kuzuia kutoridhia katika siku zijazo**, kama inavyohitajika kuzingatia hali hii." (aya ya 113, msisitizo umeongezwa).

[162] Jopo la Kufanya Uchunguzi la Kundi la Benki ya Dunia, January 8, 2016, Ripoti na Mapendekezo. Inapatikana hapa: https://www.inspectionpanel.org/sites/default/files/ip/PanelCases/98-Inspection%20Panel%20Report%20and%20Recommendation.pdf.

na mradi kwa kuwezesha utoaji wa mafunzo kupitia hatua za mabadiliko ya tabia za jamii ili kupunguza kukubalika kwa CSA na GBV dhidi ya watoto katika jamii. Mafunzo yanapaswa kutafuta kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa Bridge na watoto wa eneo hilo kujikinga dhidi ya hatari za CSA na GBV na kutafuta msaada wa kutosha ikiwa watapitia hali hii. Kwa kuongezea, mafunzo ya kukabiliana na CSA na GBV dhidi ya watoto yanapaswa kujumuisha wazazi; vikosi vya afya vya eneo husika; watoa huduma za afya ya akili; machifu wa eneo husika na viongozi wengine wa jamii; polisi, majaji, na maafisa wengine wa utekelezaji wa sheria; na viongozi wa kidini na kitamaduni. Mafunzo na aina hii yanapaswa kutolewa katika jamii zote zilizo na shule za Bridge.

## 7.2 Mapendekezo ya Ngazi ya Taasisi

Uchunguzi huu ulionyesha sababu kadhaa za msingi za kutoridhia ambazo zinaweza kunufaika na hatua za IFC za kushughulikia hali, kama ifuatavyo.

**c. Kupitia miradi yake yote ili kutambua miradi yote ambapo watoto wako hatarini zaidi na wanaweza kuathiriwa katika jamii zinazoathirika ili kutambua na kutathmini ikiwa hatua mwafaka za ushughulikiaji wa hatari katika jamii zipo na zinatekelezwa.** Mahali ambapo hazipo, IFC inapaswa kufanya kila juhudi ili kuwezesha mradi uliofadhiliwa kuridhia, ikiwa ni pamoja na:

- Kushirikiana na mteja husika kutambua hatua za kushughulikia CSA na GBV ambazo hazijatekelezwa au ambazo hazikutambuliwa wakati wa utafiti wa kabla ya mradi, na kumsaidia mteja kubuni na/au kutekeleza hatua hizo.
- Kupitia upya mikataba ya uwekezaji ili kubaini: (1) kwamba hatua za usalama wa watoto na ulinzi wa watoto ni sharti zizingatiwe ndani ya wigo wa majukumu yote ya E&S ya wateja; na (2) kwamba sababu zozote za kuaminika za kuamini kuwa unyanyasaji wa watoto kingono kutokana na mradi umetokea lazima ziripotiwe mara moja kwa IFC.
- Kufanyia Marekebisho Vielelezo vya Ukaguzi vya Ufuatiliaji wa Kila Mwaka ili kujumuisha taarifa na kushughulikia maswala yanayohusiana na dhuluma dhidi ya watoto-ikiwa ni pamoja na CSA na GBV.

**d. Kuimarisha na kufafanua vifungu vya E&S vinavyohusiana na watoto, pamoja na madhara tofauti ya kijinsia na kingono, ndani ya Mfumo wa Uendelevu.** IFC inapaswa kufanyia marekebisho Mfumo wake wa Uendelevu ili kujumuisha yafuatayo:

- Vifungu vipya katika Viwango vya Utendakazi ambavyo vinalenga na kuelezea zaidi wateja majukumu yao ya kulinda na kutunza watoto na na kuwataka kushughulikia na kurekebisha madhara yoyote kwa watoto yanayohusiana na mradi kwa kuzingatia GIIP, kwa kuzingatia kuwa wanawake, wasichana, wavulana, na jinsia mbalimbali wamo hatarini zaidi kukumbana na aina zote za unyanyasaji wa kijinsia. Hatimaye, IFC inapaswa kuwataka wateja wake kushughulikia vipengele vingine vinavyoingiliana vinavyochangia hatari ambazo waathirika wa ubaguzi wa kingono na kijinsia wanaweza kukabiliana nazo, ikiwa ni pamoja na vile vinavyohusiana na utambulisho wa kijinsia, umri, umaskini, rangi, kabila, asili na ulemavu.

- Vifungu vipya katika Sera ya Uendelevu vinavyohusu watoto tu na madhara yanayotofautishwa ya kijinsia na kingono vinaelezea majukumu ya IFC kwa suala la kutambua, kuepuka, kupunguza, na kukabiliana na hatari za mradi na athari mbaya kwa watoto na watu wengine walio hatarini zaidi kuathiriwa, ikiwa ni pamoja na wanawake na wasichana, watu wa LGBT+, watu maskini, wazee, watu

wenye ulemavu, makabila madogo, watu wa kiasili, na watu wengine walio hatarini zaidi kudhulumiwa, kubaguliwa kijinsia, au aina nyingine za madhara yanayotokana na miradi inayofadhiliwa na IFC.

**e. Kufanya juhudi za kujengea uwezo taasisi nzima ili kuzuia CSA na aina zinazoingiliana za GBV kutokea katika miradi yake ya uwekezaji, ikiwa ni pamoja na:**

- Kutoa mafunzo na uhamasishaji kuhusu uzuiaji wa GBV na CSA kwa wafanyikazi wote wa IFC wanaoshughulikia mradi. Mafunzo ya aina hii yanapaswa kufanywa mara kwa mara; kusasishwa kama GIIP inayohusiana na ulinzi wa watoto, usalama wa watoto, na mabadiliko ya kuzuia GBV; na yalioundwa ili kushughulikia kwa haraka na na kwa njia mwafaka masuala yoyote yanayoibuliwa kuhusiana na GBV na CSA wakati wa uwekezaji.
- Ukuzaji wa nyenzo za mwongozo wa kutambua, kutathmini na kushughulikia dhuluma dhidi ya watoto unaorandana na mbinu zilizosawazishwa za WBG. IFC inapaswa kuandaa mwongozo mahususi wa kudhibiti hatari za dhuluma dhidi ya watoto katika miradi yake yote, kwa kuzingatia sana CSA, kwa kutumia uzoefu wa Benki ya Dunia wa kushughulikia CSA na GBV zinazoingiliana.

**f. Kuanzisha kikosi kazi cha kimataifa cha GBV ili** kushauri IFC kuhusu kuimarishwa kwa mbinu yake ya kutambua na kushughulikia GBV katika uwekezaji wake wote, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono utekelezaji wa mapendekezo yaliyofafanuliwa hapo juu. Kikosi kazi kinapaswa kuwa na wataalamu madhubuti kuhusiana na uzuiaji wa unyanyasaji wa watoto kingono na kinapaswa kujumuisha wataalamu anuwai wa ndani na nje ya taasisi.

**g. Kufafanua matarajio ya mradi kuridhia Viwango vya Utendakazi wakati IFC inapopanga kujiondoa.** Vigezo vya kujiondoa kwenye mradi wakati PS haijaridhia Viwango vya Utendakazi vinapaswa kujumuishwa katika Rasimu ya Kanuni za Kujiondoa za IFC.

Katika kuwasilisha mapendekezo yaliopo hapo juu, CAO inasisitiza kwamba mapendekezo ya ngazi ya taasisi na mafunzo kutokana na matokeo ya ripoti hii ni muhimu kwa utendakazi wa jumla wa E&S za IFC hata nje ya sekta ya elimu. Kwa hivyo, yanabaki kuwa muhimu licha ya tangazo la IFC la Mei mwaka wa 2022 kwamba itaepuka kufanya uwekezaji wowote katika sekta ya elimu ya kibinafsi ya K–12 katika siku zijazo.

## Hatua zinazofuata

Baada ya kukamilisha uchunguzi wake, IFC imetuma ripoti hii kwa Menejimenti ya IFC. Kwa kuzingatia Sera ya CAO, IFC itaandaa Ripoti ya Menejimenti ambayo inaweza kujumuisha Mpango Kazi wa Menejimenti (MAP) ili kuidhinishwa na Bodi kama sehemu ya kushughulikia uchunguzi huu wa ridhaa itakayozingatia mapendekezo yanayopatikana katika ripoti hii.  Ripoti ya uchunguzi wa ridhaa na Ripoti ya Menegimenti, zitatolewa kwa umma, na CAO itafuatilia utekelezaji kikamilifu wa MAP.